SILSILA YA HOTUBA ZA AL-MASJID AN-NABAWI 2

# NGUZO ZA UISLAMU

KATIKA HOTUBA ZA AL-MASJID AN-NABAWI




**UTUNZI WA**

DKT. ABDUL-MUHSIN IBNU MUHAMMAD AL-QAASIM

IMAMU NA HATIBU WA AL-MASJID AN-NABAWI SH-SHARIIF


باللغة السواحيلية

# Nguzo Za Uisilamu

## Kutoka Hotuba Za Al-Masjid An-Nabawi


Utunzi Wa

**Dkt. Abdul-Muhsin Ibn Muhammad Al-Qaasim**

Imamu Na Hatibu Wa Msikiti Mtukufu Wa Mtume

# NGUZO ZA UISILAMU

## KUTOKA HOTUBA ZA AL-MASJID AN-NABAWI

Abdul-Muhsin ibnu Muhammad Al-Qasim,
©1444h
Uorodheshaji wa Maktaba ya Kitaifa ya King Fahd Wakati wa uchapishaji
AL-QASIM, ABDUL-MUHSIN IBNU MUHAMMAD
Nguzo za Uislamu Kutoka Hotuba za Al-Masjid An-Nabawi : Lugha ya Kiswahili. / ABDUL-MUHSIN IBNU MUHAMMAD AL-QASIM – chapisho1. .- Al-Madina Al-Munawwarah, 1444h
Kurasa 167 ; ..cm
Redmark: 978-603-04-2803-8
Hotuba za kidini   A. Anwani -1
DIWI 213                    1444/1017
Nambari ya amana: 1444/1017
Redmark: 978-603-04-2803-8

**KODI KWA KUTEREMSHA KITABU HICHI PANGUSA**

a-alqasim.com

# NGUZO ZA UISILAMU

## KUTOKA HOTUBA ZA AL-MASJID AN-NABAWI


UTUNZI WA

**DKT. ABDUL-MUHSIN IBN MUHAMMAD AL-QAASIM**

IMAMU NA HATIBU WA MSIKITI MTUKUFU WA MTUME

Yamkini kupakuwa hotuba hizi au kuzisikiliza
kupitia kiunganishi hiki
a-alqasim.com/khotab/

# UTANGULIZI

Sifa njema zote anastahiki Allah Mola mlezi wa viumbe wote, na swala na salamu zimshukie Nabii wetu Muhammad, watu wake na masahaba wake wote.

Ama baada [ya himdi hii]:

Basi kwa hakika nguzo tano za Uisilamu ndio misingi ambayo Uislamu umejengwa juu yake, wala haiwi sahihi imani ya mja ila kwa kuzitekeleza kikauli, kivitendo na kiitikadi, na nguzo hizi ni: shahada mbili, swala, zaka, saumu na hija.

Na kwa ajili ya umuhimu wake (nguzo hizi) nilitoa hotuba kuhusu kila nguzo miongoni mwazo ndani ya Msikiti wa Mtume, kisha nikaziandika, na nikazipangilia katika kitabu hiki, zikafika hotuba kumi na tisa (19), na nikakiita: «**NGUZO ZA UISILAMU KUTOKA HOTUBA ZA AL-MASJID AN-NABAWI**».

Namuomba Allah awanufaishe [watu] nacho, na akijaalie [ni amali] iliotakaswa kwa ajili ya Uso wake Mkarimu.

Na swala na salamu za Allah zimshukie Nabii wetu Muhammad, watu wake na masahaba zake wote.

Dkt. Abdul-Muhsin ibn Muhammad Al-Qaasim
Imamu na Hatibu wa Masjid An-Nabawi Ash-Shariif.

# Shahada Mbili

# UBORA WA NENO LA TAWHIDI[1]

Sifa njema zote ni za Allah, twamuhimidi, twamtaka msaada, na msamaha, na twajilinda Naye kutokana na shari za nafsi zetu, na amali zetu mbovu, yule atakayeongozwa na Allah basi hakuna wa kumpoteza, na atakaye mpoteza basi hakuna wa kumuongoza, na nashuhudia kuwa hakuna apasaye kuabudiwa isipokuwa Allah peke Yake, hana mshirika Naye, na nashuhudia kuwa Muhammad ni mja wake na Mtume wake, swala za Allah ziwe juu yake, na juu ya watu wake na sahaba zake, na awateremshie salamu nyingi.

Ama baada [ya himdi hii]

Basi mcheni Allah - enyi waja wa Allah - haki ya kumcha, na kamateni Uisilamu katika kishikio madhubuti,

Enyi waisilamu:

Utukufu wa kiumbe uko katika kumtii Allah, na kudumu katika ibada zake, na hiyo ni hekima ya kuumba [kwa Allah] na amri [Yake], na kwayo ndio yanapatikana mafanikio na kufaulu duniani na akhera:

﴿وَمَن يُطِعِ ٱللَّهَ وَرَسُولَهُۥ فَقَدۡ فَازَ فَوۡزًا عَظِيمًا﴾

{Na anayemtii Allah na Mtume wake, bila ya shaka amefanikiwa mafanikio makubwa} (Al-Ahzab: 71),

Na hakika si mengine furaha, ladha, uzuri wa umri na neema yanakuwa ndani ya kumtambua Allah, kumpwekesha na kumuamini.

Na maneno bora kabisa, na yanayopendeza zaidi kwa Allah ni yale yaliokuwa ya kumsifu Yeye, na sifa bora zaidi kwa Allah ni Neno la tawhidi «laa ilaaha illa llah», Neno ambalo kwa ajili yake zimesimama mbingu na ardhi, na kwa ajili yake ndio waliumbwa viumbe, na kwa ajili yake ndio Allah aliteremsha Vitabu vyake na akawatumiliza Mitume wake, [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿وَمَآ أَرۡسَلۡنَا مِن قَبۡلِكَ مِن رَّسُولٍ إِلَّا نُوحِيٓ إِلَيۡهِ أَنَّهُۥ لَآ إِلَٰهَ إِلَّآ أَنَا۠ فَٱعۡبُدُونِ﴾

{Na hatukumtuma kabla yako Mtume yeyote ila tulimfunulia ya kwamba hapana apasaye kuabudiwa isipokuwa Mimi. Basi niabuduni Mimi tu} (Al-

[1] [Hutuba hii] imetolewa siku ya ijumaa, tarehe sita ya mwezi wa jumaadal uulaa, mwaka wa elfu moja mia nne na thelathini na nane hijria, ndani ya msikiti wa Nabii (Al-Masjidi Nnabawi).

Anbiya: 25),

Nao Mitume waliwaonya nalo kaumu zao [waliwaonya kulikeuka Neno hilo]; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿أَنْ أَنذِرُوٓاْ أَنَّهُۥ لَآ إِلَٰهَ إِلَّآ أَنَا۠ فَٱتَّقُونِ﴾

{ili nyinyi muonye kwamba hapana apasaye kuabudiwa ila Mimi, basi nicheni Mimi}. ( An-Nahl: 2).

Allah amelishuhudia Neno hili kwa nafsi yake, na akawashuhudiza viumbe vyake walio bora zaidi; amesema aliyetakasika:

﴿شَهِدَ ٱللَّهُ أَنَّهُۥ لَآ إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ وَٱلْمَلَٰٓئِكَةُ وَأُوْلُواْ ٱلْعِلْمِ قَآئِمَۢا بِٱلْقِسْطِۚ لَآ إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ ٱلْعَزِيزُ ٱلْحَكِيمُ﴾

{Allah na Malaika na wenye elimu, wameshuhudia kuwa hakika hapana apasaye kuabudiwa ila Yeye, ndiye Mwenye kusimamisha uadilifu; hapana apasaye kuabudiwa ila Yeye Mwenye nguvu na Mwenye hekima}. (Al-Imran: 18).

Asema ibnul Qayyim Allah amrehemu: "huu ndio ushahidi mkubwa zaidi, mtukufu zaidi, muadilifu zaidi, na wa ukweli zaidi, kutoka kwa Shahidi mkubwa zaidi, juu ya jambo kubwa zaidi la kushuhudiwa".

Sheria zote [za Uisilamu] zimejengwa juu ya Neno hili, na dini yote ni miongoni mwa haki zake, na thawabu zote ni katika kulitekeleza, na adhabu zote ni katika kuliacha au kufanya upungufu katika kulitekeleza, na nguzo [za dini] zote zinasimama juu yake, ni Neno lenye daraja za juu, lenye fadhila nyingi, kwani [Neno] hili ndio kichwa cha Uisilamu wote, na ndio ya kwanza kati ya nguzo zake na majengo yake makubwa, na juu yake ndio zinasimama nguzo zote [za Uisilamu zilizo baki], nalo ndio nguzo ya kumuamini Allah na sehemu yake kubwa zaidi, basi haiwi sahihi imani bila [kulitekeleza neno] hili, wala hainyooki [imani] ila [inapojengwa] juu yake.

Mila [ya Uisilamu] imejengwa juu ya [Neno hili], na kibula kimewekwa [kwa ajili yake], nalo ndio haki ya Allah juu ya waja wote. Ni Neno la Uisilamu, na ufunguo wa nyumba ya salama [Pepo]. Kwa ajili yake watu wamegawanyika wakawa [baina ya] waovu na wema, waliokubaliwa [katika rehema za Allah] na waliofukuzwa, [Neno hili] ni lenye kutofautisha baina ya ukafiri na Uisilamu, kati ya matamshi watu hawajatamka Neno zuri zaidi kuliko [Neno] hili, na kati ya matendo hawajatenda yaliyo mazuri zaidi kuliko yale yanayotendwa kwa mujibu wa [Neno] hili, Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**maneno yanayopendeza zaidi kwa Allah ni manne: 'sub-haana**

**llaah', 'al-hamdu lillah', 'laa ilaaha illa llaah' na 'Allahu ak-bar'**». Imepokewa na Muslim.

Hili ndilo Neno la kuchamngu ambalo Allah kalifanya maalum kwa vipenzi vyake; [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿وَأَلْزَمَهُمْ كَلِمَةَ ٱلتَّقْوَىٰ﴾

{na akawalazimisha Neno la kuchamngu}, (Al-Fat-h: 26)

Nalo ndio kishikio madhubuti ambacho atakaye shikamana nacho ataokoka; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿فَمَن يَكْفُرْ بِٱلطَّٰغُوتِ وَيُؤْمِنۢ بِٱللَّهِ فَقَدِ ٱسْتَمْسَكَ بِٱلْعُرْوَةِ ٱلْوُثْقَىٰ لَا ٱنفِصَامَ لَهَا﴾

{Basi anaye mkufuru Shet'ani na akamuamini Allah, bila shaka amekamata kishikio madhubuti, kisicho vunjika}. (Al-Baqarah: 256).

Ujuu ndio sifa yake [Neno hili], na kubaki kunaambatana nalo, [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿وَكَلِمَةُ ٱللَّهِ هِىَ ٱلْعُلْيَا﴾

{na Neno la Allah kuwa ndilo juu}. (At-Taubah: 40).

Ni Neno zuri, Allah kalipigia mfano katika kitabu chake, akasema:

﴿أَلَمْ تَرَ كَيْفَ ضَرَبَ ٱللَّهُ مَثَلًا كَلِمَةً طَيِّبَةً كَشَجَرَةٍ طَيِّبَةٍ أَصْلُهَا ثَابِتٌ وَفَرْعُهَا فِى ٱلسَّمَآءِ﴾

{Je hukuona vipi Allah alivyo piga mfano wa Neno zuri? Ni kama mti mzuri, mizizi yake ni imara, na matawi yake yako mbinguni}. (Ibrahim: 24).

Kwalo kunapatikana ukunjufu wa kifua:

﴿فَمَن يُرِدِ ٱللَّهُ أَن يَهْدِيَهُۥ يَشْرَحْ صَدْرَهُۥ لِلْإِسْلَٰمِ﴾

{Basi yule ambaye Allah anataka kumuongoza humfungulia kifua chake kwa Uislamu}. (Al-An'am: 125).

Ibnu Juraij Allah amrehemu amesema: "humfungulia kwa [Neno la] (laa illaaha illa llaah). Kwalo kunapatikana salama ya moyo,

﴿يَوْمَ لَا يَنفَعُ مَالٌ وَلَا بَنُونَ ۞ إِلَّا مَنْ أَتَى ٱللَّهَ بِقَلْبٍ سَلِيمٍ﴾

{Siku ambayo kwamba mali hayatofaa kitu wala wana. Isipokuwa mwenye kumjia Mwenyezi Mungu na moyo uliyo salimika} (Ash-Shuaraa: 88-89).

,

Ibnu Abbaasi -Allah amridhie yeye na babake- amesema: "Moyo uliosalimika ni ashuhudie kuwa hakuna apasaye kuabudia isipokuwa Allah".

Nalo ndio ulinganizi wa haki ambao hauna batili ndani yake, ni kauli ya haki ambayo haina kombo ndani yake, na ni ushahidi wa ukweli usio na

uongo ndani yake, nalo ndio Sifa ya juu kabisa ambayo Allah ameifanya maalum kwake pasina viumbe vyake, nalo ndilo Neno lililobaki baada kuondoka kwa Ibrahim salamu zimshukie; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿وَجَعَلَهَا كَلِمَةًۢ بَاقِيَةً فِي عَقِبِهِۦ لَعَلَّهُمۡ يَرۡجِعُونَ﴾

{Na akalifanya Neno hili liwe ni lenye kubaki katika vizazi vyake ili warejee [kwa hili neno, kwa kuliamini na kuitekeleza]} (Az-Zukhruf: 28).

Ibnu Kathiir Allah amrehemu amesema: "nalo [Neno hilo] ni: laa ilaaha illa llaah: alilifanya ni lenye kudumu katika kizazi cha Ibrahim, wale walioongozwa na Allah katika kizazi chake wanamuiga yeye katika kulitekeleza [Neno hili]".

"Laa ilaaha illa llaah" ni neema kubwa zaidi juu ya viumbe; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿وَأَسۡبَغَ عَلَيۡكُمۡ نِعَمَهُۥ ظَٰهِرَةً وَبَاطِنَةً﴾

{na akaeneza kwenu neema zake, za dhaahiri na za siri} (Luqman: 20).

Sufyan ibnu U'yeina Allah amrehemu amesema: «Allah hajawaneemesha waja wake kwa neema kubwa kuliko [hii] ya kuwatambulisha: laa ilaala illa llaah»

Nalo ni Neno linalotoshana na dunia pamoja na vilivyomo ndani yake; Mtume swala na salamu zimshukie alisema:

«**Kusema kwangu: 'Sub-haana llaah', 'wal-hamdu lillaah', 'wa laa ilaaha illa llaah', 'wa llaahu akbar'; kunapendeza zaidi kwangu kuliko kila kilicho chomozewa na jua**», imepokewa na Muslim.

Nalo [Neno hili] ndio wajibu wa kwanza -kuwa na elimu nalo na kulitekeleza- juu ya waja; [Allah] aliyetakasika anasema:

﴿فَٱعۡلَمۡ أَنَّهُۥ لَآ إِلَٰهَ إِلَّا ٱللَّهُ﴾

{Basi jua ya kwamba hapana apasaye kuabudiwa ila Allah}. (Muhammad: 19).

Sheikhul Islaam Allah amrehemu amesema: "Wema waliotangulia na Maimamu wameafikiana ya kuwa jambo la kwanza wapasalo kuamrishwa waja ni Shahada mbili". Nalo pia ni wajibu wa mwisho; Mtume swala na salamu zimshukie alisema:

«**Yule ambaye mazungumzo yake ya mwisho yatakuwa ni: 'laa ilaaha illa llaah', ataingia Peponi**», imepokewa na Abu Daaud.

Mwenye kulijua Neno hili na kulitekeleza ndiye aliyenyooka sawa

[katika dini] kihakika, [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿إِنَّ ٱلَّذِينَ قَالُواْ رَبُّنَا ٱللَّهُ ثُمَّ ٱسۡتَقَٰمُواْ﴾

{Hakika waliosema: Mola wetu ni Allah! Kisha wakanyooka sawa}, (Al-Ahqaf: 13).

Ibnu Abbaas Allah amridhie yeye na babake amesema: yaani: juu ya shahada ya 'laa ilaaha illa llaah',

﴿فَلَا خَوۡفٌ عَلَيۡهِمۡ وَلَا هُمۡ يَحۡزَنُونَ﴾

{hawatakuwa na khofu, wala hawatahuzunika}. (Al-Baqara: 38)

Pindi Neno hili litasadiki basi moyo utatwahirika kutokana na kila asiyekuwa Allah, na atakayekuwa mkweli katika Neno hili basi hatampenda isipokuwa Allah, hatamuona isipokuwa Yeye, hatamcha ila Yeye, hatatumai ila kwake, na hakutabakia [moyoni mwake] athari za [kuitanguliza] nafsi yake na matamanio yake [mbele ya Allah na amri yake].

Neno hili ni kinga ya mali na damu; Mtume swala na salamu zimshukie alisema:

«**Atakayesema: 'laa ilaaha illa llaah', na akawakufuru wanaoabudiwa kinyume na Allah; basi mali yake na damu yake zitakuwa haramu, na hesabu yake ni jukumu la Allah aliye na nguvu na aliyetukuka**», imepokewa na Muslim.

Nalo [Neno hili] ndilo jambo linaloanzwa nalo katika ulinganizi [daawah], Nabii swala na salamu zimshukie alianza nalo ulinganizi wake, na juu yake ndio alikuwa akichukua 'bai-ah' [ahadi ya kuinusuru dini] kutoka kwa sahaba zake, na alikuwa akiwatuma walinganizi katika miji na kulilingania Neno hili, akasema kumuambia Muadh Allah amridhie pindi alipomtuma kuenda Yemen:

«**Hakika wewe unawaendea watu waliopewa Kitabu; basi walinganie katika shahada ya 'laa ilaaha illa llaah' na kuwa mimi ni Mtume wa Allah**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea [hadith] hii.

Nalo ndilo Neno la Tawhidi, Neno lilio sawa, [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿قُلۡ يَٰٓأَهۡلَ ٱلۡكِتَٰبِ تَعَالَوۡاْ إِلَىٰ كَلِمَةٖ سَوَآءِۭ بَيۡنَنَا وَبَيۡنَكُمۡ أَلَّا نَعۡبُدَ إِلَّا ٱللَّهَ وَلَا نُشۡرِكَ بِهِۦ شَيۡـٔٗا﴾

{Sema: Enyi Watu wa Kitabu! Njooni kwenye Neno lilio sawa baina yetu na nyinyi: Ya kwamba tusimuabudu yeyote ila Allah, wala tusimshirikishe na chochote} ( Al- Imran: 64).

Atakayelisema kwa haki [kwa kulisema hali ya kulifahamu maana yake halisi na kulitekeleza] amefaulu; Nabii swala na salamu zimshukie alisema:

«**Enyi watu! Semeni 'laa ilaaha illa llaah' mtafaulu**» imepokewa na Ahmad.

Mwenye kushikamana nalo basi amekamata tagaa la juu kabisa la imani; Nabii swala na salamu zimshukie alisema:

«**Imani ni matagaa sabini na, basi bora kabisa kati yao ni kauli ya: 'laa ilaaha illa llaah'**», imepokewa na Muslim, na aya iliolikusanya [Neno hili] ndio aya adhimu kabisa katika Qur-ani, na istighfari bora kabisa imelikusanya.

Nalo ndio amali inayozidishwa zaidi na yenye ujira zaidi, kwani:

«**Atakayesema katika siku mara mia moja: *'laa ilaaha illa llaah, wah-dahuu laa shariika lah, lahul mulk, walahul hamd, wa huwa a'laa kulli shay-in qadiir'*, yatakuwa [malipo yake] kwake ni sawa na kuacha huru watumwa kumi, na ataandikiwa thawabu mia moja, atafutiwa dhambi mia moja, na yatakuwa [maneno haya] kwake ni kinga kutokana na shetani siku yake ile hadi jioni, na hatakuja mtu [siku ya Kiyama] na bora kuliko aliokuja nayo yeye, ila mtu aliyetenda zaidi ya hilo [alilotenda yeye]**», imepokewa na Bukhari na muslim.

Na: «**atakayesema: *'laa ilaaha illa llaah, wahdahuu laa shariika lah, lahul mulk, walahul hamd, wa huwa alaa kulli shay-in qadiir'*, mara kumi; atakuwa ni kama aliyeacha huru nafsi nne miongoni mwa wana wa Ismail**», imepokewa na Muslim.

Neno hili ndio sadaka kubwa zaidi bila kutoa mali; Mtume swala na salamu zimshukie alisema:

«**Na kauli ya *'laa ilaaha illa llaah'* ni sadaka**», imepokewa na Muslim, nalo [kulitekeleza Neno hili] ndio sababu ya mja kuokoka ndani ya kaburi yake, na [kuishi] juu yake [duniani] ndiko kutamthibitisha pindi atakapohojiwa [kaburini], Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**Anapoulizwa Muisilamu ndani ya kaburi: atashuhudia kuwa hapana apasaye kuabudiwa ila Allah, na kuwa Muhammad ni Mtume wa Allah; na hiyo ndio [tafsiri ya] kauli ya Allah: {Allah huwatia imara wenye kuamini kwa kauli ya imara katika maisha ya dunia na katika Akhera}**» wameafikiana Bukhari na Muslim.

Na sajili [jalada] za madhambi zinakuwa nyepesi [katika mizani ya amali] kwa ajili ya uzito wa Neno hili - hilo ni kwa neema ya Allah -,

Mtume swala na salamu zimshukie alisema:

«**Hakika Allah mwenye nguvu na utukufu atamtoa mtu miongoni mwa ummah wangu mbele ya viumbe siku ya Kiyama, amfungulie sajili [za dhambi zake] tisaini na tisa, [ukubwa wa] kila sajili moja ni upeo wa macho, kisha atolewe kibahasha, mnao ndani yake: *'ash-hadu an laa illaaha illa llaah, wa ash-hadu anna Muhammadan rasuulu llaah'*, basi ziwekwe sajili zile katika mkono wa mizani, sajili zikawa nyepesi na kibahasha kikawa kizito**», imepokewa na Ahmad.

Na «**lau mbingu saba na ardhi saba zitawekwa katika mkono wa mizani, na ikawekwa *'laa ilaaha illa llaah'* katika mkono mwingine; 'laa ilaaha illa llaah' itazishinda, na lau mbingu saba na ardhi saba zitakuwa ni duara liliofungwa [lisilo na njia ya kutokea, au amali kupanda kwa Allah], basi [amali ya] *'laa ilaaha illa llaah'* ingezipasua [na inyanyuke kuenda kwa Allah]** », imepokewa na Ahmad.

Watu wake [Neno hili] ndio wenye shafa'a (uombezi) siku ya Kiyama, na wenye ahadi mbele ya Ar-Rahmaan [Allah mwingi wa rehema]; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿لَّا يَمۡلِكُونَ ٱلشَّفَٰعَةَ إِلَّا مَنِ ٱتَّخَذَ عِندَ ٱلرَّحۡمَٰنِ عَهۡدٗا﴾

{Hawatakuwa na mamlaka ya kufanya uombezi ila wale waliochukua ahadi kwa Ar-Rahmani Mwingi wa Rehema}. (Maryam: 87)

Na watakaofaidika zaidi na uombezi wa Nabii swala na salamu zimshukie ni wenye ikhlasi walio wakweli katika kulisema [Neno hili], Nabii swala na salamu zimshukie alisema:

«**Mtu atakayefaidika zaidi na uombezi wangu siku ya Kiyama ni aliyesema: *'laa ilaaha illa llaah'* kwa ikhlasi kutoka ndani ya nafsi yake», imepokewa na Bukhari.**

Na Pepo ni malipo ya aliyelisema [Neno hili] kwa ukweli [yaani moyo wake na vitendo vyake vilisadikishe Neno hili], kwa ikhlasi ndani ya moyo wake, na akiwa na yakini nalo bila kuwa na shaka [hata ndogo], akawa mwenye kulitendea kazi, mwenye kuepuka kila lenye kuliharibu; Mtume swala na salamu zimshukie alisema:

«**Hakuna mja yeyote atasema *'laa ilaaha illa llaah'*, kisha afariki juu ya hilo; isipokuwa ataingia Peponi**» wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

[Neno hili] ni lenye kumfungulia anayelisema milango minane ya Pepo,

aingie kupitia wowote anaotaka; bali aliyekuwa mkweli katika kulisema, mtenda kazi wa yanayowajibishwa nalo; Moto wa Jahannam hautamgusa, Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**Hakuna yeyote anayeshuhudia kuwa hapana apasaye kuabudiwa ila Allah, na kuwa Muhammad ni Mtume wa Allah, [ashuhudia hilo] hali yakuwa mkweli ndani ya moyo wake, isipokuwa Allah ataharamisha yeye kuingia Motoni**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea, na Allah atamtoa kutoka Motoni kila atakayelisema na hali ya kuwa ndani ya moyo wake mna imani uzito wa chungu mdogo kabisa;

«Allah mwenye Ushindi na Utukufu amesema: **Naapa kwa ushindi wangu, Utukufu wangu, Kiburi changu na Ukuu wangu; hakika nitamtoa kutoka [Motoni] kila aliye sema *'laa ilaaha illa llaah'***», imepokewa na Bukhari.

Na kwa ajili ya umuhimu wa tawhidi katika kila punde ya maisha ya mja; ndio Sheria imekuja kuhimiza kushikamana nayo [tawhidi] katika hali zake [mja] zote na mambo yake yote;

basi «**atakayesema pindi inapoingia asubuhi: *'laa ilaaha illa llaah, wah-dahu laa shariika lah, lahul mulku, walahul hamdu, wa huwa alaa kulli shay-in Qadiir';* atakuwa [na ujira wa] kama aliyeacha huru mtumwa miongoni mwa wana wa [Nabii] Ismail, na ataandikiwa mema kumi, atafutiwa maovu kumi, atanyanyuliwa daraja kumi, na atakuwa ndani ya ulinzi kutokana na Shetani hadi iingie jioni, na anaposema hayo jioni, basi atapata [malipo] mfano wa hayo hadi iingie asubuhi**», imepokewa na Abu Daaud,

Na akilisema [Neno hili] pindi anapomaliza kujitwahirisha kwake, basi atafunguliwa milango ya Pepo [yote] minane, Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**Hakuna yeyote kati yenu atatawadha, akakamilisha udhu wake, kisha akasema: *'ash-hadu an laa ilaaha illa llaah, wa ash-hadu anna Muhammadan abduhu wa rasuuluh'*, isipokuwa atafunguliwa milango ya Pepo minane**», imepokewa na Muslim.

Nalo [Neno hili] ndio kianzio cha adhana na kimalizio chake, Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**Pindi muadhini atakaposema: 'Allahu ak-bar, Allahu ak-bar', na mmoja wenu akasema: 'Allah ak-bar, Allah ak-bar', kisha muadhini akasema: 'ash-hadu an laa ilaaha illa llaah', [naye] akasema: 'ash-hadu**

**an laa ilaaha illa llaah', kisha muadhini akasema: 'ash-hadu anna Muhammadan rasuulu llaah', [naye] akasema: 'ash-hadu anna Muhammadan rasuulu llaah', kisha muadhini akasema: 'hayya alaa sswalaa', [naye] akasema: 'laa hawla walaa quwwata illaa billaah', kisha muadhini akasema: 'hayya alal falaah', [naye] akasema: 'laa hawla walaa quwwata illaa billaah', kisha muadhini akasema: 'Allah ak-bar, Allah ak-bar', [naye] akasema: 'Allah ak-bar, Allah ak-bar', kisha muadhini akasema: 'laa ilaaha illa llaah', [naye] akasema: 'laa ilaaha illa llaah', [yote hayo akayasema] kutoka moyoni mwake, basi ataingia Peponi**», imepokewa na Muslim.

Na «**atakaye sema pindi atakapomsikia muadhini:** ***'ash-hadu an laa ilaaha illa llaahu wahadahuu laa shariika lah, wa ash-hadu anna Muhammadan abduhu wa rasuuluh, radwitu bi llaahi rabaa, wa bi Muhammadin rashuulaa, wa bil islaami diinaa*; atasamehewa dhambi zao'**», imepokewa na Muslim.

Na pindi Muisilamu anaposimama kuswali anaifungua swala na tawhidi, na wala Swala haisihi ila kwa [kupatikana] 'tashahhud' [ndani yake], na kabla mwenye kuswali atoe salamu kutoka kwenye Swala anaomba akitawasali kwa Allah kwa Neno hilo la Tawhidi.

«**Ewe Allah, nisamehe [dhambi] nilizozitanguliza, na [amali] nilizoziacha, na [dhambi] nilizozifanya kwa siri, na zile nilizozidhihirisha, na yale niliofanya israfu ndani yake na kuvuka mipaka, na yale ambayo Wewe ndiye unayajua zaidi kuliko mimi, Wewe ndiye mwenye kutanguliza [baadhi ya waja wako unaowataka na kuwanyanyua daraja za ukamilifu], na Wewe ndiye mwenye kuwacheleweshа [baadhi ya waja wako unaowataka na kuwaangusha katika tabaka za chini na udunifu],** ***'laa ilaaha illa anta'***», imepokewa na Muslim,

Na mwisho wa kila Swala anasema:

«***'laa ilaaha illa llaahu wahadahuu laa shariika lah, lahul mulku, walahul hamd, wa huwa alaa kulli shay-in qadiir'***», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Na [mja] anahitimisha nalo Neno hili] 'Tasbihi', 'Tahmidi' na 'Takbira', basi: «akasamehewa [kwalo] dhambi zake, hata kama ni mfano wa povu la bahari», imepokewa na Muslim.

Na katika ibada za hija anaambatana nayo [katika hali zote]; «Nabii

swala na salamu za Allah zimshukie alikuwa pindi anapopanda [kilima] cha Swafaa na Marwa; anaelekea kibla, anamsifu Allah na upweke [kwa Neno hili la tawhidi], na anamuadhimisha [kwa kuleta takbira]» imepokewa na Muslim,

Na walipokuwa Muzdalifah: «Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alikuja 'Al-Mash-ar' [kiwanja cha Muzdalifah], akapanda juu yake, akamuhimidi Allah, na akamsifu na tawhidi, akamuadhimisha [kwa kuleta takbira], na akasema 'laa ilaaha illa llaah'», imepokewa na Nasai.

Na [alikuwa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie] anaporudi kutoka vitani au hija au umrah, analeta takbiira mara tatu kila akipanda sehemu ya juu ya ardhi, kisha anasema: *'laa ilaaha illa llaahu wah-dahu laa shariika lah, lahul mulku wa lahul hamd, wa huwa alaa kulli shay-in qadiir*» wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Na katika misimu ya kheri - kama kumi la kwanza la dhul hijja - inapendekezwa kulikithirisha [kulisema Neno hili], na katika hotuba, mwanzo wake unafunguliwa na tawhidi, na katika kutangamana kwake [mja] na watu, pindi amekaa kikao kilichokithiri ndani yake kelele, kisha mja akasema kabla kusimama kutoka kikao chake kile:

«***Sub-haanaka llaahumma wa bihamdik, ash-hadu anlaa ilaaha illaa anta, astaghfiruka wa atuubu ilaik*; ila atasamehewa yalitokea kwenye kikao chake kile**», imepokewa na Tirmidhi.

Na «**atakayezinduka usiku** - akasema Neno hili- **kisha akaomba; maombi yake ataitikiwa, na akitawadha na kuswali; swala yake itakubaliwa**», imepokewa na Bukhari.

Na katika hali ya msiba na huzuni anasema:

«***'laa ilaaha illa llaahul A'dhwiimul Haliim, laa ilaaha illa llaahu Rabbu ssamaawaati wal ardwi wa Rabbul a'rshil kariim***», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Na kumsifu Allah nalo [Neno hili] kabla ya maombi ni sababu ya kuitikiwa; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿وَذَا ٱلنُّونِ إِذ ذَّهَبَ مُغَٰضِبٗا فَظَنَّ أَن لَّن نَّقۡدِرَ عَلَيۡهِ فَنَادَىٰ فِي ٱلظُّلُمَٰتِ
أَن لَّآ إِلَٰهَ إِلَّآ أَنتَ سُبۡحَٰنَكَ إِنِّي كُنتُ مِنَ ٱلظَّٰلِمِينَ ۞ فَٱسۡتَجَبۡنَا لَهُۥ وَنَجَّيۡنَٰهُ مِنَ ٱلۡغَمِّ﴾

{Na [Mtaje] Dhun-Nun alipoondoka hali ameghadhibika, na akadhani ya kwamba hatutakuwa na uwezo juu yake. Basi aliita katika giza: Hapana apasaye kuabudiwa isipokuwa Wewe *Sub-hanaka* Uliye takasika. Hakika

mimi nilikuwa miongoni mwa wenye kudhulumu [nafsi zao]. Basi tukamwitikia na tukamwokoa kutokana na dhiki} .(Al-Anbiya: 87-88),

Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**katu hajawahi Muisilamu yeyote kuomba kwa dua hii; ila Allah humuitikia**» imepokewa na Tirmidhi.

Nalo ndio kafara ya kikao; Mtume swala na salamu za zimshukie alisema:

«**Atakayeapa akasema katika kiapo chake: Naapa kwa lata na u'zza; basi aseme: *'laa ilaaha illa llaah'***» wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Na inapendekezwa kumtamsisha aliyefikwa na kifo Neno hili; Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**watamsheni maiti zenu: 'laa ilaaha illa llaah'**», imepokewa na Muslim.

Na aliyekuwa nje ya mila [ya Uisilamu] analinganiwa katika Neno hili hata akiwa katika wakati wa mwisho wa maisha yake; Abu Twalib alifikwa na mauti, basi Mtume swala na salamu za Allah zimshukie akasema kumuambia:

«**Ewe ami yangu, sema *'laa ilaaha illa llaah'*, Neno ambalo nitakutolea ushahidi nalo mbele ya Allah**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

**Na baada ya yaliyotangulia, enyi waisilamu:**

Basi [jueni kuwa] nguvu na ushindi ni ndani ya tawhidi, Umar Allah amridhie alisema: "Sisi ni watu ambao Allah ametupa nguvu na ushindi kwa Uisilamu", na shahada ndio anuani yake [Uisilamu] na kitambulishi chake, na kauli yenye kuvunjwa na vitendo hainufaishi, na asiyelitamka [Neno] hili basi atakosa ladha na raha za dunia na akhera, na nguvu na udhaifu wa waisilamu zinategemea kulitekeleza kwao Neno hili kimatamshi na kimatendo, basi hili ndio mizani yao mbele ya Allah na mbele ya watu, linapopata nguvu kwao basi Allah atawaridhia, watapata ushindi, na watanyanyuka, na linapodhoofika watakuwa mbali na Allah, watadhoofika na watadhalilika.

***'Audhu billaahi mina sh-shaitwaani rrajiim':***

﴿فَٱعۡلَمۡ أَنَّهُۥ لَآ إِلَٰهَ إِلَّا ٱللَّهُ وَٱسۡتَغۡفِرۡ لِذَنۢبِكَ وَلِلۡمُؤۡمِنِينَ وَٱلۡمُؤۡمِنَٰتِۗ وَٱللَّهُ يَعۡلَمُ مُتَقَلَّبَكُمۡ وَمَثۡوَىٰكُمۡ﴾

{Basi jua ya kwamba hapana apasaye kuabudiwa ila Allah, na omba

maghufira kwa dhambi zako na za Waumini wanaume na Waumini wanawake. Na Allah anajua mahali penu pa kwenda na kurudi, na mahali penu pa kukaa.} (Muhammad: 19).

Allah anibarikie mimi na nyinyi katika Qur-ani tukufu...

## HOTUBA YA PILI

Sifa njema zote anastahili Allah kwa wema Wake [kwetu], na shukrani zote anastahili Yeye kwa kutuafikia na kutuneemesha, na nashuhudia ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake hana mshirika; ili kuadhimisha shani yake, na nashuhudia ya kwamba Nabii wetu Muhammad ni mja Wake [Allah] na Mtume wake, swala na salamu nyingi za Allah zimshukie yeye, watu wa nyumba yake na Masahaba wake.

**Enyi waisilamu:**

Elimu ya maana ya Neno 'laa ilaaha illa llaah', kuitendea kazi, na kuwa mbali na yenye kulipinga [Neno hili] na yenye kulivunja; [yote hayo] ni sharti ya kupata yanayo wajibu kwalo [Miongoni mwa malipo na mazuri ya Neno hili] yaliokuja katika dalili, basi maana yake [Neno hili]: ni kukanusha kustahiki kuabudiwa kwa asiyekuwa Allah, na kulithibisha hilo kwa Allah pekee, na hili ndilo walilolipinga makafiri wa kikureshi, [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿إِنَّهُمْ كَانُوٓاْ إِذَا قِيلَ لَهُمْ لَآ إِلَٰهَ إِلَّا ٱللَّهُ يَسْتَكْبِرُونَ﴾

{Wao walipokuwa wakiambiwa 'laa ilaaha illa llah' [Hapana apasaye kuabudiwa ila Allah tu], wanafanya kiburi}, .″ (As-Swaaffaat: 35). na kuikiri kwao tawhidi ya rubuubiyyah peke yake hakukuwanufaisha kitu.

Kila aliyekuwa mjuzi zaidi wa maana yake, na mtekeleza zaidi wa mahitaji yake; basi mizani [ya mema] yake itakuwa nzito zaidi, na kutofautiana kwa watu ndani yake [Neno hili] ni kwa kiwango cha kuhakikisha kwao masharti yake, nayo roho na siri ya Neno hili: Ni kumpwekesha Allah kwa ibada, basi atakaye mshirikisha kiumbe katika haki ya Allah na ibada zake, hilo linakuwa ni lenye kuvunja kauli yake: "laa ilaaha illa llaah".

Na mwenye kuneemeka [na maisha mema] ni yule aliyeihifadhi tawhidi yake na akafariki juu yake, wala asijichafue na yoyote yenye kuivunja, au yenye kuitia dosari, au yenye kulivunja, na [maisha] haya ndio matamanio ya waja wa Allah wakweli:

﴿تَوَفَّنِي مُسْلِمًا وَأَلْحِقْنِي بِٱلصَّٰلِحِينَ﴾

{Nifishe hali ya kuwa ni Muislamu [aliyejisalimisha kwa Allah na tawhidi] na nikutanishe na waja wema}. (Yusuf: 101).

Kisha jueni ya kuwa Allah amewaamuru kumswalia na kumsalimia Nabii wake...

# MJUE NABII WAKO SWALA NA SALAMU ZA ALLAH ZIMSHUKIE[1]

Sifa za ukamilifu zote ni za Allah, tunamhimidi, tunamuomba msaada, tunamuomba msamaha, na tunajilinda na Allah kutokana na shari za nafsi zetu, na kutokana na amali zetu mbovu, yule ataongozwa na Allah, basi hakuna wa kumpoteza, na atakayempoteza hakuna wa kumuongoza, nashuhudia ya kwamba hapana apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake, hana mshirika, na nashuhudia kuwa Nabii wetu Muhammad ni mja wake na Mtume wake, swala na salamu za Allah nyingi zimshukie yeye, watu wake, na masahaba wake.

**Ama baada ya himdi hii:**

Basi mcheni Allah - enyi waja wa Allah - haki ya kumcha; kwani atakaye mcha Mola wake Mlezi ataokoka, na atakaye muepuka ataangamia.

**Enyi waisilamu:**

Allah amechagua katika sehemu na miji ile bora zaidi, na miongoni mwa nafsi zile tukufu zaidi, amechagua miongoni mwa watu mitume, akajaalia kuwa kauli zao, matendo yao, na tabia zao, ni mizani za kila kauli, tabia na matendo.

Na kumjua Nabii wetu Muhammad swala na salamu za Allah zimshukie, ni miongoni mwa misingi mitatu ambayo ni wajibu kwa kila mtu kuijua, na kila mja ataulizwa hilo ndani ya kaburi lake, ibn Al-Qayyim Allah amrehemu amesema: "Kuhitajia kwa waja kumjua Mtume, kuyajua aliyokuja nayo, kumsadikisha katika aliyoyatolea habari, na kumtii katika aliyoamrisha; kuko juu ya kila mahitaji".

Yeye ni Bwana wa wanadamu, na fahari yao duniani na akhera: Muhammad ibn Abdillahi ibn Abdil Mut-twalib, Allah kamchagua kutoka katika [ukoo wa] Bani Hashim, na akawachagua Bani Hashim kutoka katika [kabila la] Qureishi, nao ni miongoni mwa kizazi cha Nabii wa Allah Ibrahim salamu zimshukie.

Mteule wa viumbe, yeye ni mbora zaidi wa nasaba kati ya watu wa ardhini kiujumla, [Nabii] swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

---

[1] [Hutuba hii] imetolewa siku ya ijumaa, tarehe ishirini na saba ya mwezi wa Shawwali, mwaka elfu moja mia nne na ishirini na tano hijria, katika Al-Masjid An-Nabawi.

**«Mimi ni mbora wao zaidi kinafsi na kinyumba»,** imepokewa na Tirmidhi.

Ameinukia akiwa ni yatima wa wazazi wawili, amekosa malezi yao na mapenzi yao:

﴿أَلَمْ يَجِدْكَ يَتِيمًا فَـَٔاوَىٰ﴾

{Kwani hakukukuta yatima akakupa makaazi?}, (Ad-Dwuha: 6).

Akawa anazunguka baina ya walezi akiwa na utunzaji na hifadhi kutoka kwa Allah. Alichukiziwa ibada na kunyenyekea masanamu. Mola wake mlezi alimuhifadhi kutoka udogoni mwake, na akamlinda katika ubarobaro wake, hakukamata sanamu, wala kuligusa.

Kabla ya kupewa utume alimuoa mwanamke mtukufu mwerevu, alikuwa mwanamke mwenye heshima na mwenye akili zaidi; naye ni Khadijah Allah amridhie.

Allah alimtumiliza hali ardhi imejaa ibada za masanamu, habari za makuhani, umwagaji wa damu, na ukataji kizazi; basi akalingania katika kumuabudu Allah peke yake, akisubiri juu ya yote yaliomkumba miongoni mwa kukadhibishwa, kuepukwa na kuchukiwa.

Allah alinyanyua utajo wake na shani yake. Miujiza yake ni mikubwa sana, na dalili zake [za ukweli wake] ni za wazi kabisa, amenusuriwa kwa uoga [uliojazwa ndani ya nyoyo za maadui zake], amesamehewa dhambi zote, ni wa kwanza litakalopasuka kaburi lake [siku ya kufufuliwa], ni wakanza atakaye kubaliwa uombezi wake siku ya Kiyama, ni Nabii aliye na wafuasi wengi zaidi, wa kwanza atakayegonga mlango wa Pepo, na atakayevuka 'Swiraat' [daraja lembamba kuliko nywele juu ya Moto wa Jahanamu].

Alikuwa ni mwingi wa shukurani kwa Allah, anasimama usiku [kuswali] hadi miguu yake inafura, utulivu wa jicho lake uko kwenye swala, humsimamia Allah [kuswali] akiwa na ikhlaas na utulivu, Abdallah ibn Ash-Shikhiir Allah amridhie amesema: «Nilimuona Mtume swala na salamu za Allah zimshukie akiswali, na hali mnatoka kifuani mwake sauti mfano wa sauti ya kuchemka kwa maji sufuriani kutokana na kulia», imepokewa na Ahmad. [Mtume] Alisema kuhusu nafsi yake:

**«Naapa kwa Allah, hakika mimi ni mchamngu zaidi»,** imepokewa na Muslim.

Ni mwenye kumuadhimisha Mola wake mlezi, mwenye adabu ya juu na

aliyemuumba, hajidaii nafsi yake chochote kati ya vitu asiovimilika yeyote ila Allah; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿قُل لَّآ أَمۡلِكُ لِنَفۡسِي نَفۡعٗا وَلَا ضَرًّا إِلَّا مَا شَآءَ ٱللَّهُۚ
وَلَوۡ كُنتُ أَعۡلَمُ ٱلۡغَيۡبَ لَٱسۡتَكۡثَرۡتُ مِنَ ٱلۡخَيۡرِ وَمَا مَسَّنِيَ ٱلسُّوٓءُۚ إِنۡ أَنَا۠ إِلَّا نَذِيرٞ وَبَشِيرٞ لِّقَوۡمٖ يُؤۡمِنُونَ﴾

{Sema: Siimilikii nafsi yangu manufaa wala madhara, ila apendavyo Allah. Na lau kuwa ninayajua ya ghaibu ningejizidishia mema mengi, wala ovu lisingenigusa. Mimi si chochote ila ni mwonyaji na mbashiri kwa watu wanao amini}. (Al-A'raf: 188).

Na mtu mmoja alimjia akamwambia: «[Jambo] ni alitakalo Allah na unalolitaka wewe, basi [akajibu] kumwambia: **Hivi umenifanya mimi ni mshirika wa Allah?! Sema: [Jambo] alitakalo Allah peke yake**», imepokewa na Nasai.

Na Allah alisema kumuambia [Mtume]:

﴿قُلۡ إِنِّي لَآ أَمۡلِكُ لَكُمۡ ضَرّٗا وَلَا رَشَدٗا﴾

{Sema: Mimi sina mamlaka ya kukudhuruni wala kukuongozeni}, (Al-Jinn: 21).

Ibnu Kathiir Allah amrehemu amesema [akitafsiri aya hii]: "yaani: Hakika si mengine, mimi ni mtu kama nyinyi, ninaletewa Wahyi, na ni mja miongoni mwa waja wa Allah, sina amri yoyote katika kuongoka kwenu wala kupotea kwenu, bali marudio ya hayo yote ni kwa Allah».

Ni Mtume mwenye unyeyekevu zaidi, na mwenye ngozi mzuri zaidi, anakaa na mafukara, na anakula na maskini. Anapangusa viatu vyake, na anawahudimia watu wake na nafsi yake, alikunywa katika kiriba kilicho chakaa, na alibeba matofali pamoja na masahaba wake wakati wa kujenga msikiti, hawatii aibu watumishi wala hawakejeli. Anas Allah amridhie amesema: «Nilimtumikia Mtume wa Allah swala na salamu zimshukie miaka tisa, hakuwahi katu kuniambia: kwa nini umefanya kadha na kadha? Wala katu hakunitia aibu katika kitu chochote», imepokewa na Muslim.

Anawaheshimu wakubwa, na ananyenyekea kwa vijana, akipita kwa watoto anawasalimia.

Alimuona Abu Umeyr Allah amridhie - na alikuwa mdogo -, akasema akicheza naye: «**Ewe Abu U'meyr, amefanya nini 'nughair'**?», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Anas Allah amridhie anasema: «Sijaona yeyote aliyekuwa mwenye

huruma zaidi kwa familia kuliko Mtume wa Allah swala na salamu zimshukie», imepokewa na Muslim.

Alikuwa mwingi wa unyenyekevu, aliye mbali kutokana na kujifakhiri, kiburi na ubabe, [Mtume] asema:

«**Hakika si mengine mimi ni mja wake [Allah], basi [mnapo nitaja] semeni: Mja wa Allah na Mtume wake**», imepokewa na Bukhari.

Alikuwa mkarimu wa nafsi, mwenye mkono wa kutoa sana, mwingi wa utoaji; anatoa kwa ukarimu na kumtegemea Allah, hajawahi kuombwa kitu katika manufaa ya kidunia ambacho anakimiliki kisha akamkatalia aliyemuomba; Anas Allah amridhie amesema:

«Mtume wa Allah swala na salamu zimshukie hajawahi kuombwa kitu ila anakitoa», imepokewa na Muslim.

Dunia na mambo ya kidunia hayamfanyi kughadhibika. Aliiepuka nyumba hii [dunia], na akatenda amali kwa ajili ya nyumba ya utulivu [akhera], alikuwa akisema:

«**Ni nani mimi na dunia?! Mimi siko katika dunia ila ni kama msafiri aliyepumzika chini ya kivuli cha mti, kisha akaondoka na akakiwacha**», imepokewa na Tirmidhi.

Alikuwa akipitiwa na mwezi na mwengine bila kuwashwa moto ndani ya nyumba zake, na akilala usiku wa kufuatana bila familia zake kuwa na chakula cha usiku, Umar ibnul Khatwaab amesema: «Nilimuona Mtume wa Allah swala na salamu zimshukie akikaa siku nzima anainamia tumbo lake [kwa ajili ya njaa], hapati hata tende mbovu kujaza tumbo lake», imepokewa na Muslim.

Na alitoka nyumbani kwa kwa ajili ya harara ya njaa, na alifunga tumbo lake kwa ajili ya uchungu wa njaa, na Masahaba zake Allah awaridhie walikuwa wakiitambua njaa yake kutokana na kubadilika kwa sauti yake, Abu Twalha Allah amridhie amesema: «Niliisikia sauti ya Mtume wa Allah swala na salamu zimshukie ikiwa dhaifu, nakaitambua njaa alionayo»,

Na yanapita masiku katika nyumba za Nabii na hamna ndani yake ila maji, «mtu alikuja kwa Mtume wa Allah swala na salamu zimshukie akasema: hakika mimi nimelemewa na njaa, [Mtume] akatumana kwa baadhi ya wake zake, akasema: Naapa kwa aliyekutumiliza kwa haki hakuna kitu kwangu ila maji, kisha [Mtume] akatumana kwa [mke] mwengine, naye akasema mfano wa alioyasema yule wa mwanzo, hadi [wake zake] wote wakasema mfano wa hayo», wameafikiana Bukhari na

Muslim kuipokea.

Alikuwa mkamilifu wa hofu ya Mola wake mlezi, pamoja na njaa aliyopata, alikuwa akipata tende katika tandiko lake, asema:

«**basi nainyanyua ili kuila, kisha naiacha kwa kuogopea isije ikawa ni sadaka**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Alipata mazito ya kimaisha, na mambo magumu zaidi, amekulia akiwa yatima, aliyekosa mapenzi ya mama, na babake alikufa wala jicho lake halikupata pumbao kwa kumuona. Kaumu yake ilimuudhi kwa kauli na vitendo, Anas Allah amridhie amesema: «Mara moja walimpiga Mtume wa Allah swala na salamu zimshukie hadi akapoteza fahamu», imepokewa na Ahmad.

Walimtuhumu na wazimu, uchawi, na wakamsifu na urongo:

﴿وَقَالَ ٱلۡكَٰفِرُونَ هَٰذَا سَٰحِرٞ كَذَّابٌ﴾

{na makafiri wakasema: Huyu ni mchawi, mwongo}, (Swaad: 4).

na katika pango [alikumbwa na] janga, hamu, hofu na huzuni,

﴿إِذۡ يَقُولُ لِصَٰحِبِهِۦ لَا تَحۡزَنۡ إِنَّ ٱللَّهَ مَعَنَا﴾

{naye akamwambia sahibu yake: Usihuzunike. Hakika Mwenyezi Mungu yu pamoja nasi}, (At-Taubah: 40).

na katika vita vya Uhud jino lake la mbele lilivunjwa, uso wake ukajuruhiwa, na damu yake ikatiririka.

Alikumbana na harara ya njaa, na uovu wa adui, walimtilia sumu katika chakula chake, wamfanyia uchawi katika familia yake. Misiba iliandamana juu yake, na mitihani [ya kimaisha] ilimvamia, na Mola wake anamwambia:

﴿فَٱصۡبِرۡ كَمَا صَبَرَ أُوْلُواْ ٱلۡعَزۡمِ مِنَ ٱلرُّسُلِ﴾

{Basi subiri, kama walivyosubiri Mitume wenye stahmala kubwa}. (Al-Ahqaf: 35).

Alimueleza mke wake Aisha huzuni zake; akasema:

«**Hakika nimekumbwa kutoka kaumu yako yalionikumba!**», imepokewa na Bukhari.

Alifiliwa na wanawe sita katika uhai wake, wala majanga hayo hayakumkatizia ulinganizi wake kwa Allah, alisubiri huzuni na shida za kimaisha, alisema kuhusu nafsi yake:

«**Hakika niliudhiwa katika [kulingania kwa] Allah, wakati haudhiwi yeyote mwengine, na nilihofishwa katika [kulingania kwa] Allah,**

**wakati hahofishwi yeyote mwengine**», imepokewa na Ahmad.

Alikuwa mwenye moyo laini uliojaa huruma, alikuwa akiskia kilio cha mtoto akiwa ndani ya swala, anahafifisha swala yake, kwa ajili ya kujua uzito anaoupata mamake mtoto kutokana na kilio chake. Alikuwa akizuru makaburi ya baqi'i, basi akikumbuka akhera na akilia, «Alikuwa akimzuru mwanawe Ibrahim kwa mnyonyeshaji wake hali akiwa mdogo wa kunyonya, na Ibrahim akimjia akiwa na athari ya vumbi, basi Nabii swala na salamu zimshukie akimkumbatia, akimbusu, na akimnusa, kutokana na huruma za ubaba» imepokewa na Bukhari,

Na [Ibrahim] alipofariki, macho yake yalibubujika machozi, na akasema:

«**Hakika jicho linatoa machozi, na moyo unahuzunika, wala hatusemi ila ya kumridhisha Mola wetu mlezi, hakika sisi tumehuzunika kukuepuka ewe Ibrahim**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Alikuwa mwenye akili kamili, mwenye tabia za juu, hajawahi kumpiga mtu yeyote kwa mkono wake; Aisha Allah amridhie amesema: «Mtume swala na salamu zimshukie katu hakupiga chochote kwa mkono wake, wala mwanamke, wala mtumishi», imepokewa na Muslim.

Alikuwa mwenye heshima zaidi kati ya watu, mtukufu zaidi, mkono wake katu haukugusa mwanamke asiye halali kwake.

Alikuwa mkamilifu wa utekelezaji kwa familia yake na Masahaba wake Allah awaridhie, alikuwa akichinja mbuzi, akimkata vipande, kisha akiwapelekea marafiki za [mkewe] Khadija Allah amridhie baada ya kufa kwake ili kumtekelezea [mkewe] wema. Aliwaswalia mashahidi wa [vita vya] Uhud miaka minane baada ya vita hivyo, kama kuwa anawaaga. Alikiwakirimu masahaba wake, wala haipendelei nafsi yake chochote pasina wao, Uthman ibnu Affan Allah amridhie amesema: «Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alikuwa akitupumbaza kwa kichache na kingi»,

Aliwaenea watu kwa tabia zake, mwenye busara, halipishi maovu, bali husamehe, tena bila kulaumu, haghadhibiki kwa ajili ya nafsi yake, wala halipishi kuinusuru. Alikuvutwa nguo na mbedui aliyetaka kupewa mali, basi akamgeukia na tabasamu, na akimpa anachoomba.

Alimsamehe aliyemfanyia uchawi, wala hakumlaumu na kumkejeli aliyemtilia sumu katika chakula, na aliwasamehe waliompiga vita, na akawaambia siku ya kuftahi Makkah:

«**Ondokeni, kwani nyinyi [leo hii] mumeachiwa**»,

Aisha Allah amridhie amesema: «katu hakukosewa chochote akawa ni mwenye kumuadhibu aliyemkosea», imepokewa na Muslim.

Alikuwa mlaini, mwenye uso mkunjufu daima; Jariir ibn Abdillah Allah amridhie amesema: «wala Mtume swala na salamu za Allah zimshukie hakuwahi kuniona ila alitabasamu», imepokewa na Bukhari.

Anawajulia Masahaba wake, na katika adabu yake anawatanguliza [Masahaba] wabora. Alikuwa mwenye tangamano zuri, mwenye usuhuba mwema, anawaunga watu wa kizazi chake, wala hakuwa na tabia nzito na yeyote.

Alikuwa mwenye kujihifadhi ulimi wake, hakuwa mwenye maneno machafu, wala hakuwa akijikalifisha maneno machafu, bali alikuwa mwingi wa haya, hata kuliko mwanamwali ndani ya sitara yake, sifa zake ni kimaumbile, hapendi kukuza matamshi, wala kupotosha mdomo ili kulazimisha ufasaha;

«Walikuja watu kwa Nabii swala na salamu za Allah zimshukie wakasema [kumwambia]: Ewe Mtume wa Allah, ewe mbora wetu, na mwana wa mbora wetu, ewe bwana wetu, na mwana wa bwana wetu, [Mtume] akasema: **Enyi watu, semeni kauli zenu, wala shetani asiwavute, mimi ni Muhammad, mja wa Allah na Mtume wake, sipendelei mninyanyue zaidi ya cheo changu alichoniweka Allah mwenye ushindi na utukufu**», imepokewa na Nasai.

Na katika chakula anachompa mgeni wake, hajikalifishi kilichoko, wala hataki kisicho kuweko, Masahaba wake walimpenda sana, akisema wanasikiliza kauli yake, na akiamrisha wanakimbilia kutekeleza amri yake, Anas Allah amridhie amesema: «Hakuna mtu yeyote aliyependeza zaidi kwao [Masahaba] zaidi ya Mtume wa Allah swala na salamu zimshukie», imepokewa na Ahmad.

Amekusanya tabia nzuri na adabu takatifu zaidi, Sheikhul Islaam Allah amrehemu amesema: "Hakuhifadhiwa uongo hata mmoja, wala dhulma hata moja, wala kuvunja maagano na yeyote, bali alikuwa mkweli zaidi wa watu, muadilifu wao zaidi, na mtekelezaji zaidi wa ahadi, pamoja na hali tofauti tofauti zilizompitia - miongoni mwa amani, hofu, uwezo na udhaifu -».

Anawaadhimisha watu wa nyumba yake na anaamiliana nao vizuri:

Pindi binti yake Fatma Allah amridhie anapomjia, alisimama kumpokea, na kumuambia: «**karibu**», na kumkalisha ubavuni mwake. [Na Mtume] alisema: «**Mbora wenu ni yule aliyebora kwa watu wake, nami ni mbora**

**wenu zaidi kwa watu wangu**», imepokewa na Tirmidhi.

Aliyemuumba alimtolea ushahidi kwa tabia zake tukufu, akasema:

﴿وَإِنَّكَ لَعَلَىٰ خُلُقٍ عَظِيمٍ﴾

{Na hakika wewe una tabia tukufu} ( Al-Qalam: 4).

Ni mtu mwenye uso unaong'ara zaidi; uso wake unamemetuka kumemetuka kwa mwezi usiku wa kamilika [wa kumi na tano], Al-Bara-u Allah amridhie amesema: «Katu sijaona kitu kizuri kumliko», imepokewa na Bukhari.

Mzuri wa mwili, mwenye harufu nzuri; Anas Allah amridhie amesema: «katu sijanusa ambari, wala miski, wala chochote chenye harufu nzuri zaidi kuliko harufu ya Mtume wa Allah swala na salamu zimshukie», imepokewa na Muslim.

Ni mfasaha na mwenye ubainifu mkuu, maneno yake yanamiliki nyoyo, wakati wake wote umeimarishwa katika kumtii Allah na kumridhisha:

﴿قُلْ إِنَّ صَلَاتِي وَنُسُكِي وَمَحْيَايَ وَمَمَاتِي لِلَّهِ رَبِّ ٱلْعَالَمِينَ ۞ لَا شَرِيكَ لَهُۥ﴾

{Sema: Hakika Swala yangu, na ibada zangu, na uhai wangu, na kufa kwangu, ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa viumbe vyote * Hana mshirika}. (Al-An'am: 162-163).

Kutoka apewe utume hadi kufa kwake analingania katika kuabudiwa Mola wake, na anaukataza umma wake kuingia katika ushirikina. Hakuna kheri ila aliwajulisha umma wake, wala hakuna shari ila aliwatahadharisha nayo.

Basi jilazimisheni njia yake, na mushikamane na uongofu wake na sunnah yake, na chungeni na kumhalifu, hivyo mtafaulu duniani na akhera.

***'Audhu billaahi mina sh-shaitwaani rrajiim'***

﴿لَقَدْ جَآءَكُمْ رَسُولٌ مِّنْ أَنفُسِكُمْ عَزِيزٌ عَلَيْهِ مَا عَنِتُّمْ حَرِيصٌ عَلَيْكُم بِٱلْمُؤْمِنِينَ رَءُوفٌ رَّحِيمٌ﴾

{Hakika amekwisha kujieni Mtume kutokana na nyinyi wenyewe; yanamhuzunisha yanayo kutaabisheni; anakuhangaikieni sana. Kwa Waumini ni mpole na mwenye huruma}. (At-Taubah: 128).

Allah anibarikie mimi na nyinyi katika Qur'ani tukufu...

## HUTUBA YA PILI

Sifa njema zote anastahili Allah kwa wema Wake [kwetu], na shukrani zote anastahili Yeye kwa kutuafikia na kutuneemesha, na nashuhudia ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake hana mshirika; ili kuadhimisha shani yake, na nashuhudia ya kwamba Nabii wetu Muhammad ni mja Wake [Allah] na Mtume wake, swala na salamu za Allah zimshukie yeye, watu wa nyumba yake na Masahaba wake.

**Ama baada ya himdi, enyi Waislamu:**

Nabii wetu Muhammad swala na salamu za Allah zimshukie ni mtu miongoni mwa watu, anagonjeka na anashikwa na njaa, anafikwa na huzuni na analala, hana chochote miongini mwa Sifa za Uola wala za kuabudiwa, na hakika si mengine, yeye ni Mtume anayefikisha ujumbe wa Mola wake mlezi; [Allah] mwenye Ushindi na utukufu amesema:

﴿قُلۡ إِنَّمَآ أَنَا۠ بَشَرٞ مِّثۡلُكُمۡ يُوحَىٰٓ إِلَيَّ أَنَّمَآ إِلَٰهُكُمۡ إِلَٰهٞ وَٰحِدٞۖ

فَمَن كَانَ يَرۡجُواْ لِقَآءَ رَبِّهِۦ فَلۡيَعۡمَلۡ عَمَلٗا صَٰلِحٗا وَلَا يُشۡرِكۡ بِعِبَادَةِ رَبِّهِۦٓ أَحَدَۢا﴾

{Sema: Mimi ni mwanaadamu kama nyinyi. Ninaletewa Wahyi kwamba muabudiwa wenu ni muabudiwa mmoja tu. Mwenye kutaraji kukutana na Mola wake Mlezi [akitarajia thawabu zake na kuogopa adhabu yake] basi na atende vitendo vyema, wala asimshirikishe yeyote katika ibada ya Mola wake Mlezi} (Al-Kahf: 110).

Haijuzu kunyanyuliwa zaidi ya cheo chake, wala kuteremshwa chini ya daraja yake, ni wajibu kumfuata na kutekeleza amri zake, amesema [mtunzi wa] 'fat-hi al-majiid': "Kumuadhimisha Mtume swala na salamu za Allah zimshukie kunapatikana kwa kuadhimisha amri yake na katazo lake, kuandama uongofu wake, na kufuata sunnah yake".

Na rehema zinateremka na kheri kuandamana kwa kumtii yeye,

﴿وَأَطِيعُواْ ٱللَّهَ وَٱلرَّسُولَ لَعَلَّكُمۡ تُرۡحَمُونَ﴾

{Na mtiini Allah na Mtume ili mpate kurehemewa}, (Al- Imran: 132).

na kumpenda kwa utiifu kwake ni jambo lenye kutangulizwa kuliko kumpenda mtoto na mzazi; [Mtume] swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**Hawi muumini mmoja wenu mpaka niwe napendeza zaidi kwake**

**kuliko mtoto wake, mzazi wake, na watu wote**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Na kwa kumfuata yeye maisha yanakuwa bora, watu wote wanapata furaha, [Allah] mwenye ushindi na utukufu amesema:

﴿مَنۡ عَمِلَ صَٰلِحٗا مِّن ذَكَرٍ أَوۡ أُنثَىٰ وَهُوَ مُؤۡمِنٞ فَلَنُحۡيِيَنَّهُۥ حَيَوٰةٗ طَيِّبَةٗۖ

وَلَنَجۡزِيَنَّهُمۡ أَجۡرَهُم بِأَحۡسَنِ مَا كَانُواْ يَعۡمَلُونَ﴾

{Mwenye kutenda mema, mwanamume au mwanamke, naye akawa ni muumini, tutamhuisha maisha mema; na tutawapa ujira wao kwa bora ya waliyokuwa wakiyatenda}. (An-Nahl: 97).

Na maisha bora ya mja duniani na akhera yameambatanishwa na kushikamana na uongofu wake [Mtume], na ushindi unakuwa kwa kadri ya kumfuata yeye, na kufaulu ni kwa kuiandama athari yake.

Kisha jueni ya kwamba Allah amewaamrisheni kumswalia na kumsalimia Nabii wake...

# SWALA

# CHEO CHA SWALA KATIKA UISILAMU[1]

Sifa njema zote ni za Allah mwenye ushindi, mwenye kukahiri majabari na kuwaunga madhaifu, asiyedirikwa na mawazo wala macho, namuhimidi Yeye aliyetukuka himdi inayolingana na neema zake kubwa, na namshukuru shukurani inayozidi kila hisani, na nashuhudia ya kwamba hapana apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake, hana mshirika naye, Mmoja mwenye kukahiri majabari na kuwaunga madhaifu, na nashuhudia kuwa Nabii wetu Muhammad swala na salamu za Allah zimshukie ni mja wake na Mtume wake, aliyeboreshwa kwa Ujumbe mtukufu zaidi, na dalili zilizo wazi zaidi, alikuja na kulitangaza jambo hili [Uislamu], akiwa ni mwenye kumuogopa Allah, na mwenye kuwaombea umma wake. Swala na salamu za Allah zimshukie yeye, jamaa zake, Masahaba wake - wenye bidii na uchangamfu katika utiifu -, na kila anayeifuata njia yake hadi siku ya marejeo.

**Ama baada ya himdi hii:**

Basi enyi waja wa Allah mcheni Allah, na muabuduni haki ya kumuabudu, ni mtakasieni kila kauli na amali.

**Enyi Waislamu:**

Hakika Allah ametuwekea Sheria iliyo nyepesi na sahali zaidi kuitenda, na iliyo na thawabu kubwa zaidi, na akausimamisha Uislamu juu ya misingi na nguzo, pindi zitakapoingia dosari basi jengo litabomoka, na Uisilamu utaondoka.

Enyi waja wa Allah, swala ndio nguzo ya pili kati ya hizo nguzo, nayo ndio tegemeo la Uisilamu, ambayo [Uislamu] unasimama juu yake, na ndio inayonyanyua jengo lake na kusimamisha kingo zake.

Manabii na Mitume waliamrishwa kuitekeleza; [Allah] mwenye ushindi na utukufu amesema kumuambia Musa salamu zimshukie:

﴿إِنَّنِيٓ أَنَا ٱللَّهُ لَآ إِلَٰهَ إِلَّآ أَنَا۠ فَٱعۡبُدۡنِي وَأَقِمِ ٱلصَّلَوٰةَ لِذِكۡرِيٓ﴾

{Hakika Mimi ndiye Allah. Hapana apasaye kuabudiwa ila Mimi tu. Basi niabudu Mimi, na usimamishe swala kwa ajili ya kunikumbuka Mimi}, (Twa-ha: 14),

---

[1] Ilitolewa siku ya Ijumaa, tarehe kumi na mbili ya mwezi wa Shawwali, mwaka wa elfu moja mia nne na kumi na tisa hijria, katika ya al-Masjid An-Nabawi.

Nabii Ibrahim salamu zimshukie alimuomba Mola wake Mlezi kwa kauli yake:

﴿رَبِّ ٱجۡعَلۡنِي مُقِيمَ ٱلصَّلَوٰةِ وَمِن ذُرِّيَّتِي﴾

{Mola wangu Mlezi! Nijaalie niwe mwenye kusimamisha Swala, na katika kizazi changu pia} (Ibrahim: 40),

Allah alimsifu Ismai’l salamu zimshukie akasema:

﴿وَكَانَ يَأۡمُرُ أَهۡلَهُۥ بِٱلصَّلَوٰةِ وَٱلزَّكَوٰةِ وَكَانَ عِندَ رَبِّهِۦ مَرۡضِيّٗا﴾

{Na alikuwa akiwaamrisha watu wake Swala na Zaka, na alikuwa mbele ya Mola wake Mlezi ni mwenye kuridhiwa}, (Maryam: 55).

Nabii Isa salamu zimshukie alijivunia swala, akasema:

﴿وَأَوۡصَٰنِي بِٱلصَّلَوٰةِ وَٱلزَّكَوٰةِ مَا دُمۡتُ حَيّٗا﴾

{Na ameniusia Swala na Zaka maadamu ni hai}, ( Maryam: 31).

Allah akamuamrisha nayo Nabii wetu Muhammad Swala na salamu zimshukie, akasema:

﴿أَقِمِ ٱلصَّلَوٰةَ لِدُلُوكِ ٱلشَّمۡسِ إِلَىٰ غَسَقِ ٱلَّيۡلِ﴾

{Simamisha Swala jua linapopinduka mpaka giza la usiku}, (Al-Isra`: 78)

Nayo ni miongoni mwa nyasia za waja wema wa Allah kwa watoto wao:

﴿يَٰبُنَيَّ أَقِمِ ٱلصَّلَوٰةَ وَأۡمُرۡ بِٱلۡمَعۡرُوفِ وَٱنۡهَ عَنِ ٱلۡمُنكَرِ﴾

{Ewe mwanangu! Shika Swala, na amrisha mema, na kataza maovu}, (Luqman: 17) na [Allah] akawaamrisha nayo Waumini kwa jumla; Akasema:

﴿وَأَقِيمُواْ ٱلصَّلَوٰةَ وَءَاتُواْ ٱلزَّكَوٰةَ وَٱرۡكَعُواْ مَعَ ٱلرَّٰكِعِينَ﴾

{Na simamisheni Swala, na toeni Zaka, na rukuuni pamoja na wanao rukuu} (Al-Baqarah: 43).

Nayo ndio nidhamu ya Dini na nguzo yake, atakayeisimamisha atakuwa amesimamisha Dini yake, na mwenye kuipoteza atakuwa amebomoa Dini yake, nayo ni dalili ya imani na anwani ya kunyooka sawa [katika Dini],

Na ndio ibada ya kwanza iliowajibishwa na Allah miongoni mwa ibada za dhahiri, na ya kwanza atakayoheshabiwa mja siku ya Kiyama, na ya mwisho itakayokosekana katika Dini, na ya mwisho aliyousia Nabii - swala na salamu za Allah zimshukie - umma wake, Mola wenu Mlezi aliifaradhisha juu ya mbingu ya saba bila ya ukati [wa Jibrili].

Ni ibada isiyoingia ndani yake niyaba kwa hali yoyote; basi hawezi yeyote kuswali kwa niaba ya mwengine yeyote; si kwa kuwepo udhuru wala bila udhuru.

Allah aliiwajibisha mwenyewe kwa njia ya kuzungumza na Mtume wake swala na salamu zimshukie katika usiku wa miraji, kuiadhimisha kwake Allah ndani ya Kitabu chake kunazidi ibada zote. Ni mwendani wa Shahada mbili, mara anaihusu kwa kuitaja, na mara nyengine anaiambatisha na Zaka. Alizianza [kuzitaja] amali njema nayo, na akazihitimisha nayo.

Allah aliitaja ndani ya Kitabu chake kwa kuihusu baada ya kutaja [ibada] kwa jumla:

﴿ٱتْلُ مَآ أُوحِىَ إِلَيْكَ مِنَ ٱلْكِتَـٰبِ وَأَقِمِ ٱلصَّلَوٰةَ﴾

{Soma na kuyatekeleza uliyofunuliwa katika Kitabu [hichi], na usimamishe Swala}. (Al-`Ankabut :45).

Inabainika ndani yake ukuu wa Muumba na udhalilifu wa viumbe, ni maandalizi ndani wakati wa hofu, na ni kinga dhidi ya maadui, ni pumbao na raha, inaufunika na kuujaza moyo na utulivu na radhi, kwayo zinatengea amali na kauli.

Kisimamo chake ni kuadhimisha, rukuu yake ni unyenyekevu, na sujudu yake ni kujidhalilisha [kwa Allah], Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**Swala ni nuru**», imepokewa na Muslim, Nuru ndani ya nyoyo na akili, inaondosha giza la upotevu na batili, na inaingiza moyoni uongofu na haki, na inaleta nuru kwenye giza la kaburi, kwayo paji la uso linametameta kwa kung'aa siku ya Kiyama.

Ni yenye kufuta dhambi, na kunyanyua daraja, Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**Hakuna mtu yeyote Muisilamu atakayeingiliwa na Swala ya faradhi, basi akaboresha udhu wake, na unyenyekevu wake na rukuu yake; ila itakuwa [Swala hiyo] ni yenye kufuta dhambi za kabla yake, madamu hajafanya ovu kubwa, na hili ni katika maisha yote**», imepokewa na Muslim.

Mnao ndani yake [Swala] unyenyekevu, maombi, kujidhalilisha [mbele ya Allah], kunong'ona Naye, na ukaribu na Ar-Rahmaan; Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**Mja anakuwa karibu zaidi na Allah hali anapokuwa ndani ya**

**sujudu**», imepokewa na Muslim.

Kutekeleza kwa wakati wake ni amali inayopendeza kwa Ad-Dayyaan [mwenye kuwalipa watu matendo yao]; Ibnu Mas-uud Allah amridhie amesema:

«nilimuuliza Mtume wa Allah swala na salamu zimshukie: ni amali gani inayopendeza zaidi kwa Allah? Akasema: **Swala kwa wakati wake**, nikasema: kisha ni gani? Akasema: **Kutenda wema wazazi wawili**, nikasema: kisha ni gani? Akasema: **Jihadi katika njia ya Allah**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Ni yenye kuleta furaha siku ya malipo; ibnu Mas-uud Allah amridhie amesema: «Anaye furahia kukutana na Mola wake Mlezi kesho [siku ya Qiyama] hali yeye ni Muisilamu, basi azihifadhi kweli kweli hizi Swala kwa kuzitekeleza pale zinapoitiwa, kwani kwa hakika Allah amempa Nabii wenu Sheria ya sunnah za uongofu, nazo [hizi Swala] ni katika Sunnah za uongofu», imepokewa na Muslim.

Kuimarisha misikiti kwa kuitekeleza [Swala] ndio amali yenye kutangulizwa na Mitume wenye stahmala kubwa pindi wanaposhukia katika miji:

﴿وَإِذۡ يَرۡفَعُ إِبۡرَٰهِـۧمُ ٱلۡقَوَاعِدَ مِنَ ٱلۡبَيۡتِ وَإِسۡمَٰعِيلُ﴾

{Na kumbukeni Ibrahim na Ismail walipoinyanyua misingi ya ile Nyumba [Kaaba]}, (Al-Baqarah: 127) na Nabii wetu Muhammad swala na salamu za Allah zimshukie, punde tu alipowasili Madina wakati alipohajiri, alianza kujenga msikiti wake.

**Enyi Waislamu:**

Binadamu ni mwenye umbile dhaifu, ni mwepesi wa kupaparika na kupapatika, ni mwingi wa makosa na madhambi, atembelea katika maisha haya katikati ya njia ya machungu na mazito:

﴿لَقَدۡ خَلَقۡنَا ٱلۡإِنسَٰنَ فِي كَبَدٍ﴾

{Hakika tumemuumba mtu ndani ya taabu}, (Al-Balad: 4).

Na mnapatikana ndani ya Swala uwepesishaji wa mambo, ukunjufu wa vifua, kuondoka hamu na ghamu, usaidizi juu ya mambo ya kimaisha na kukidhiwa mahitaji. Ni mangapi yenye kufurahisha, ya kheri aina tofauti, na ya baraka kubwa kubwa yamepatikana kwa ajili ya Swala?! [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿وَٱسۡتَعِينُواْ بِٱلصَّبۡرِ وَٱلصَّلَوٰةِ﴾

{Na tafuteni msaada kwa kusubiri na kwa kuswali}, (Al-Baqarah: 45).

Na: «Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie alikuwa akiswali anapokumbwa na jambo», imepokewa na Ahmad.

Swala ni nguvu ya Muisilamu akiwa ndani ya mtihani [wa kimaisha], inamhimiza kusubiri na kuvumilia, inatia nguvu azimio lake, inaushikanisha moyo wake, inaipumzisha fikra yake na kiwiliwili chake kutokana na shughuli za kidunia na mateso ya kuchuma, Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alikuwa akisema:

«**Tufurahishe na Swala ewe Bilal**», imepokewa na Ahmad.

Na ilikuwa ndio utulivu wa jicho lake swala na salamu za Allah zimshukie, na Allah alipotaka kumtahini bikira Maryam kwa kumjaalia mtoto bila ya kuwa na mume, alimuamrisha aelekee kwa swala; ili kumhafifishia uzito wa mtihani huo:

﴿يَٰمَرۡيَمُ ٱقۡنُتِي لِرَبِّكِ وَٱسۡجُدِي وَٱرۡكَعِي مَعَ ٱلرَّٰكِعِينَ﴾

{Ewe Maryamu! Mnyenyekee Mola Mlezi wako na usujudu na urukuu pamoja na wanao rukuu} (Al- Imran: 43).

Swala huvuta riziki na hukunjua pato, [Allah] aliyetakasika:

﴿وَأۡمُرۡ أَهۡلَكَ بِٱلصَّلَوٰةِ وَٱصۡطَبِرۡ عَلَيۡهَاۖ لَا نَسۡـَٔلُكَ رِزۡقٗاۖ نَّحۡنُ نَرۡزُقُكَ﴾

{Na waamrishe watu wako kusali, na uendelee mwenyewe kwa hayo. Sisi hatukuombi wewe riziki, bali Sisi ndio tunakuruzuku}, (Twaha: 132).

Ibnu Kathiir Allah amrehemu amesema: "utakaposimamisha Swala riziki itakujia kwa njia usizozitarajia".

Nayo [swala] ni mashukio ya rehema, na sehemu ya kujibiwa maombi; [Allah] alitakasika amesema:

﴿فَنَادَتۡهُ ٱلۡمَلَٰٓئِكَةُ وَهُوَ قَآئِمٞ يُصَلِّي فِي ٱلۡمِحۡرَابِ أَنَّ ٱللَّهَ يُبَشِّرُكَ بِيَحۡيَىٰ

مُصَدِّقَۢا بِكَلِمَةٖ مِّنَ ٱللَّهِ وَسَيِّدٗا وَحَصُورٗا وَنَبِيّٗا مِّنَ ٱلصَّٰلِحِينَ﴾

{Alipokuwa kasimama chumbani akisali, Malaika walimnadi: Hakika Allah anakubashiria Yahya, atayekuwa mwenye kusadikisha Neno litokalo kwa Allah, na ni bwana na mtawa na Nabii anayetokana na watu wema.} ." (Al- 'Imran: 39).

**Enyi Waisilamu:**

Sifa za waumini waliofaulu zimeanzwa na Swala, na kustahiki mirathi

ya [Pepo ya] Firdaus kunatimia kwa kuihifadhi. Kudumu juu yake ndio sifa ya kwanza ya wakirimiwa miongoni mwa watu wa Peponi, pia kuihifadhi ni hatima ya sifa zao.

Allah ameikusanya kheri yote ndani ya swala; kwa kauli fasaha zaidi na matamshi machache zaidi; akasema:

﴿إِنَّ ٱلصَّلَوٰةَ تَنْهَىٰ عَنِ ٱلْفَحْشَآءِ وَٱلْمُنكَرِ﴾

{Hakika Swala inazuilia mambo machafu na maovu}. (Al-'Ankabut: 45).

Hayabaki madoa ya uchafu na uovu pamoja na Swala; inatengeneza sifa na tabia, na inazikinga na upotofu,

Mnao ndani yake matendo mema na sifa tukufu, na anayo mwenye kuitekeleza sera njema. imekusanya faida na manufaa aina tofauti, na sampuli miongoni mwa mazuri.

**Enyi Waislamu:**

Hakika kuacha Swala na kuichukulia dharau ni katika misiba mikuu na aibu mbaya, wala haiachi ila mwenye [kustahiki] adhabu kubwa, na hasara na majuto marefu, na mwenye kuikanusha amemuepuka Allah, ametoka nje ya duara la Uisilamu, ameharamishiwa kuirithi [Pepo ya] Al-Firdaus, na kukirimiwa ndani ya Pepo zenye neema, mashukio yake ni 'saqar' [Moto], na ni lipi linakujulisha 'saqar' ni nini?!

Na yule hatakuwa miongoni mwa watu wa kumsujudia [Allah] Mmoja mwenye kuabudiwa, basi Allah atamchoma na Moto; Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**Hakika Moto utamla binadamu kila kitu isipokuwa athari ya kusujudu**»,

Na [Nabii] swala na salamu za Allah zimshukie alisema [tena]:

«**Baina ya mtu na baina ya ushirikina na ukafiri ni kuacha Swala**», imepokewa na Muslim.

Sheikhul Islaam Allah amrehemu amesema: "Na mtu aliyebaleghe lau ataacha kuswali Swala moja tu, miongoni mwa Swala tano [za faradhi], basi atatakwa kutubia, endapo atatubia [arudi kuswali, basi ataachwa], laa sivyo huuliwa [na kiongozi wa taifa]». Ibnu Al-Qayyim Allah amrehemu amesema: "Waislamu hawahitalifiani ya kuwa kuacha Swala ya faradhi kusudi ni miongoni mwa madhambi makubwa kabisa, na kuwa dhambi zake [jambo hili] mbele ya Allah ni kubwa kuliko dhambi za kuua nafsi, kuiba mali, na kuliko dhambi za zinaa, wizi, na kunywa vileo, na kuwa mtu huyu

[anayeacha Swala ya faradhi] amejipeleka katika adhabu ya Allah, hasira zake, na hizaya kutoka kwake; duniani na akhera", na haachi yeyote Swala ila huwa na maisha maovu, na haitekelezi ila hufaulu na hupata [mazuri].

***'Audhu billaahi mina sh-shaitwaani rrajiim'***

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ ٱرۡكَعُواْ وَٱسۡجُدُواْۤ وَٱعۡبُدُواْ رَبَّكُمۡ وَٱفۡعَلُواْ ٱلۡخَيۡرَ لَعَلَّكُمۡ تُفۡلِحُونَ﴾

{Enyi mlioamini! Rukuuni na msujudu, na muabuduni Mola wenu Mlezi, na tendeni mema, ili mfanikiwe}. (Al-Hajj: 77).

Allah anibarikie mimi na nyinyi katika Qur’ani tukufu...

## HUTUBA YA PILI

Sifa njema zote anastahiki Allah Aliye juu na mbali kutokana na kuwa washirika na mifano, aliyetasika kutokana na kuwa mke na watoto, namhimidi Yeye aliyetukuka kwa sababu ya neema zake nyingi.

Nashuhudia ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake, hana mshirika Pamoja naye, tena ushahidi uliotakaswa kutokana na uchafu wa ushirikina na upotevu, na nashuhudia ya kwamba Nabii wetu Muhammad ni mja wake [Allah] na Mtume wake, Nabii na Mtume mteule, aliyetumilizwa na rehema na uongofu, swala na salamu za Allah zimshukie yeye, watu wake na Masahaba wake; walio viongozi wa uongofu, na miezi yenye kung'aa usiku.

**Ama baada ya himdi hii, enyi Waislamu:**

Allah Aliyetukuka amewaamrisha Waumini wote Swala ya jamaa; akasema:

﴿وَأَقِيمُوا۟ ٱلصَّلَوٰةَ وَءَاتُوا۟ ٱلزَّكَوٰةَ وَٱرْكَعُوا۟ مَعَ ٱلرَّٰكِعِينَ﴾

{Na simamisheni Swala, na toeni Zaka, na rukuuni pamoja na wanao rukuu}, (Al-Baqarah: 43).

Na [Allah] aliyetakasika amewaamrisha nayo Waumini walio kwenye jihadi, hata kama wamekabiliana na adui, na Nabii hakumpa udhuru wa kutohudhuria Swala ya jamaa chongo aliyekosa wa kumuongoza njia wa kudumu naye.

Kupitia Swala ya jamaa mjinga anajifunza, aliyeghafilika anapata ukumbusho, na kwayo Waislamu wanasaidiana katika kumpenda Allah, kumuabudu, na kunyenyekea mbele yake, na [kwayo] safu zao [Waumini] zinaungana kuwa kitu kimoja.

Abu Huraira Allah amridhie amesema: "kujaa masikioni mwa mwanadamu madini ya risasi ilioyayushwa ni afadhali kwake kuliko aisikie [mwito wa Swala]: 'hayya ala sswalaah, hayya alal falaah' kisha asiitikie". Na ibnu Al-Qayyim Allah amrehemu amesema: "Sifa sita [kuwa nazo] ndani ya Swala ni katika alama za unafiki: Uvivu wakati wa kuiendea, kuonyesha watu wakati wa kuitekeleza, kuicheleweshа, kuswali bila utulivu, uchache wa kumdhukuru Allah ndani yake, na kuiacha jamaa yake".

**Enyi Waisilamu:**

Ni katika ukarimu wa Allah kuwa amezidisha ujira maradufu kwa yule atakayehifadhi Swala ya jamaa misikitini;

Basi «**atakaye swali Ishai katika jamaa ni kana kwamba amesimama**

**nusu usiku** [kwa ibada]**, na atakaye swali Alfajiri katika jamaa ni kana kwamba amesimama usiku wote**»

Na «**atakayeenda Msikitini asubuhi au jioni; Allah humuandalia mashukio yake Peponi kila anapoenda asubuhi au jioni**».

Na kukamilisha Udhu pamoja na kuwepo machukivu [mfano wa baridi kali, kuwepo maumivu mwilini na kadhalika], na wingi wa hatua kwa kuenda Misikitini, na kuisubiri Swala baada ya kukamilisha Swala [asitoke baada kuswali hadi Swala nyingine iingie]; ni [kama] jihadi ya kulinda mipaka, kwayo Allah anawafutia dhambi na kwayo anawanyanyua daraja.

Na atakayetawadha akakamilisha udhu, kisha akatembea kuenda kutekeleza Swala ya faradhi, akaiswali pamoja na jamaa; atasamehewa dhambi zake,

Na atakayetawadha vizuri, kisha akatoka kuenda Msikitini, hakuna lililomtoa ila ni Swala tu, [huyo] hatapiga hatua ila atanyanyuliwa daraja na atafutiwa dhambi, na atakaposwali hawataacha Malaika kumuombea madamu yupo ndani ya sehemu aliyoswali, na kwa kila hatua unayopiga unapoenda kuswali ni Sadaka.

Mazuri haya [ya swala] na mengineo ameahidiwa yule atakayeisimamisha Swala [kwa jamaa] pamoja na Waisilamu, basi mhimidi Allah aliyetukuka, kule kuwa amekuongoza kupata mazuri haya, na akakuhusu miongoni mwa viumbe vyake na mambo mazuri.

**Enyi waja wa Allah:**

Baba mwenye upole wa hakika kwa wanawe, na mwenye rehema kikweli kwa jamaa zake: ni yule anayewasaidia juu ya kusimama kuswali; basi usitoke nyumbani kwako kwa ajili ya Swala ila na watoto wako wako mbele yako, kuliani kwako, kushotoni kwako, na mbavuni mwako, wanashindana mbele yako kuenda katika nyumba za Allah na sehemu za kuteremka rehema zake.

Basi mcheni Allah katika Dini yenu kiujumla, na hasa katika Swala yenu, kwani amri yake ni adhimu, na shani yake ni kubwa, basi ijieni kwa kupenda, na kwa ajili ya kutekeleza amri ya Mola wenu Mlezi.

Kisha jueni kuwa Allah amewaamrisha kumswalia na kumsalimia Nabii wake...

## CHEO CHA SWALA KATIKA DINI[1]

Sifa za ukamilifu zote ni za Allah, tunamhimidi, tunamuomba msaada, tunamuomba msamaha, na tunajilinda na Allah kutokana na shari za nafsi zetu, na kutokana na amali zetu mbovu, yule ataongozwa na Allah, basi hakuna wa kumpoteza, na atakayempoteza hakuna wa kumuongoza, nashuhudia ya kwamba hapana apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake, hana mshirika, na nashuhudia kuwa Nabii wetu Muhammad ni mja wake na Mtume wake, swala na salamu za Allah nyingi zimshukie yeye, watu wake, na masahaba wake.

**Ama baada ya himdi hii:**

Basi mcheni Allah - enyi waja wa Allah - haki ya kumcha; kwani uchamngu ndio zuri zaidi kati ya mnayoyadhihirisha, na tukufu zaidi kati ya mnayoyaficha.

**Enyi Waislamu:**

Amali adhimu zaidi mbele ya Allah ni: Kumpwekesha Allah kwa ibada, na mja hajawahi jikurubisha kwa Allah na mfano wa hilo, na utiifu bora baada ya tawhidi ni: nguzo ya pili ya Uisilamu [Swala], mna ndani yake Utajo wa Allha, kumuadhimisha, kumdhalilikia na kumnyenyekea, Allah aliita imani; akasema:

﴿وَمَا كَانَ ٱللَّهُ لِيُضِيعَ إِيمَـٰنَكُمْ﴾

{Na Allah hakuwa mwenye kuipoteza Imani yenu}. (Al-Baqarah: 143).

Nayo ni nguzo na tegemeo la Uisilamu, na ni sifa ya kwanza ya wachamngu katika Kitabu cha Allah baada ya sifa ya imani ya kuamini ghaibu, na ni utulivi wa jicho la Nabii swala na salamu za Allah zimshukie, na alikuwa akiwatuma nayo wajumbe wake katika miji, [Mtume] swala na salamu za Allah zimshukie alisema kumuambia Muadh Allah amrehemu:

«**Basi liwe la kwanza kuwalingania nalo: ni kumuabudu Allah mwenye Ushindi na ukubwa; wakwisha kumtambua Allah, basi wajulishe kuwa Allah amewafaradhishia Swala tano katika mchana**

---

[1] Ilitolewa siku ya ijumaa, tarehe ishirini na saba, mwezi wa Jumaadal ulaa, mwaka wa elfu moja mia nne na thalathini na tano, ndani ya Msikiti wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie.

**wao na usiku wao**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea, na Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alikuwa jambo la kwanza analolishuritisha baada ya tawhidi ni kusimamisha Swala; kwa sababu hiyo ndio kichwa cha ibada za kiwiliwili, na wasia wake kwa umma wake mwisho wa maisha yake:

«[Hifadhini] **Swala!** [Hifadhini] **Swala! Na** [chungeni haki za] **waliomilikiwa na mikono yenu ya kiume**» , imepokewa na Ahmad.

Atakayeikamilisha atakuwa amesimama kutekeleza Dini yake, na atakayeipoteza atakuwa kwa mengine [kati ya wajibu wa Dini] ni mwenye kupoteza zaidi, nayo ni amani kwa yule aliyekuwa mshirikina kabla kisha akasilimu:

﴿فَإِن تَابُوا۟ وَأَقَامُوا۟ ٱلصَّلَوٰةَ وَءَاتَوُا۟ ٱلزَّكَوٰةَ فَخَلُّوا۟ سَبِيلَهُمْ﴾

{Lakini wakitubu, wakasimamisha Swala, na wakatoa Zaka, basi waachilieni}. (At-Taubah: 5).

Nayo ni kinga ya damu na mali, [Nabii] swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**Nimeamrishwa kuwapiga vita watu hadi washuhudie ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah, na kuwa Muhammad ni Mtume wa Allah, na wasimamishe Swala, na watoe Zaka; basi pindi wakifanya hayo watakuwa wamekinga damu zao na mali yao isipokuwa kwa haki ya Uisilamu, na kuwahesabu ni juu ya Allah**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea, na ni yenye kuwajibisha undugu katika Dini:

﴿فَإِن تَابُوا۟ وَأَقَامُوا۟ ٱلصَّلَوٰةَ وَءَاتَوُا۟ ٱلزَّكَوٰةَ فَإِخْوَٰنُكُمْ فِى ٱلدِّينِ﴾

{Kama wakitubu na wakasimamisha Swala na wakatoa Zaka, basi ni ndugu zenu katika Dini}. (At-Taubah: 11).

Na kwa ajili ya ukubwa wa cheo chake, na kutofautiana kwake na amali zilizobaki: ndio Allah aliiwajibisha kwa Manabii na Mitume wake, akamteremshia Ibrahim, Is-haaq na Ya'qub amri ya kuisimamisha; akasema:

﴿وَأَوْحَيْنَآ إِلَيْهِمْ فِعْلَ ٱلْخَيْرَٰتِ وَإِقَامَ ٱلصَّلَوٰةِ وَإِيتَآءَ ٱلزَّكَوٰةِ﴾

{Na tukawafunulia watende kheri, na washike Sala, na watoe Zaka}, (Al-Anbiya`: 73).

Na Ibrahim salamu zimshukie alimuomba Mola wake kizazi cha miongoni mwa wenye kusimamisha Swala, na Allah alimsifu Ismail salamu zimshukie kwa kuwa na hamu nayo; akasema:

﴿وَكَانَ يَأۡمُرُ أَهۡلَهُۥ بِٱلصَّلَوٰةِ وَٱلزَّكَوٰةِ وَكَانَ عِندَ رَبِّهِۦ مَرۡضِيّٗا﴾

{Na alikuwa akiwaamrisha watu wake Swala na Zaka, na alikuwa mbele ya Mola wake Mlezi ni mwenye kuridhiwa}. (Maryam: 55).

Na faradhi ya kwanza aliyoifaradhisha Allah kwa Musa baada ya tawhidi ni: Kusimamisha Swala, [Allah] akamzungumzisha nazo [Tawhidi na Swala] Musa bila ya ukati:

﴿إِنَّنِيٓ أَنَا ٱللَّهُ لَآ إِلَٰهَ إِلَّآ أَنَا۠ فَٱعۡبُدۡنِي وَأَقِمِ ٱلصَّلَوٰةَ لِذِكۡرِيٓ﴾

{Hakika Mimi ndiye Allah. Hapana apasaye kuabudiwa ila Mimi tu. Basi niabudu Mimi, na usimamishe Swala kwa ajili ya kunikumbuka}, (Twaha: 14).

Na Allah aliwafunulia hilo Musa na Haaruun salamu ziwashukie, wawaamrishe kaumu yao hilo [la kusimamisha Swala]:

﴿وَأَوۡحَيۡنَآ إِلَىٰ مُوسَىٰ وَأَخِيهِ أَن تَبَوَّءَا لِقَوۡمِكُمَا بِمِصۡرَ بُيُوتٗا وَٱجۡعَلُواْ بُيُوتَكُمۡ قِبۡلَةٗ وَأَقِيمُواْ ٱلصَّلَوٰةَ﴾

{Na tukampelekea Musa na ndugu yake wahyi kwamba: Watengenezeeni majumba watu wenu katika Misri na zifanyeni nyumba zenu ndio mahali pa ibada, na msimamishe Swala} (Yunus: 87).

Na Zakariyya salamu zimshukie alikuwa ni mwenye kudumu juu ya kuitekeleza:

﴿فَنَادَتۡهُ ٱلۡمَلَٰٓئِكَةُ وَهُوَ قَآئِمٞ يُصَلِّي فِي ٱلۡمِحۡرَابِ﴾

{Basi Malaika wakamnadi hali kasimama akisali ndani sehemu yake ya ibada} ( Al- Imran: 39).

Daud swala na salamu zimshukie alikuwa mpenzi wa Swala, akisimama thuluthi ya usiku kuswali, na kaumu ya Shu'ayb walipoona kuwa Nabii wao [Shu'ayb salamu zimshukie] anawalingania katika Tawhidi na kuadhimisha Swala, walisema kumuambia:

﴿أَصَلَوٰتُكَ تَأۡمُرُكَ أَن نَّتۡرُكَ مَا يَعۡبُدُ ءَابَآؤُنَآ أَوۡ أَن نَّفۡعَلَ فِيٓ أَمۡوَٰلِنَا مَا نَشَٰٓؤُاْ﴾

{Ni sala zako ndizo zinazokuamrisha [utuamrishe] tuyaache waliyokuwa wakiyaabudu baba zetu, au tuache kufanya tupendavyo katika mali zetu?}. (Hud: 87).

Na Isa salamu zimshukie aliizungumza [Swala] hali yeye bado yumo katika mlezi:

﴿وَأَوۡصَٰنِي بِٱلصَّلَوٰةِ وَٱلزَّكَوٰةِ مَا دُمۡتُ حَيّٗا﴾

{Na ameniusia Swala na Zaka maadamu ni hai}, (Maryam: 31).

Allah aliwasifu Manabii swala na salamu ziwashukie akasema:

﴿إِذَا تُتۡلَىٰ عَلَيۡهِمۡ ءَايَٰتُ ٱلرَّحۡمَٰنِ خَرُّواْۤ سُجَّدٗا وَبُكِيّٗا﴾

{Wanaposomewa Aya za Mwingi wa Rehema huanguka kusujudu na kulia}, (Maryam: 58).

Na walichukuliwa wana wa Israili ahadi ya kuitekeleza:

﴿وَلَقَدۡ أَخَذَ ٱللَّهُ مِيثَٰقَ بَنِيٓ إِسۡرَٰٓءِيلَ وَبَعَثۡنَا مِنۡهُمُ ٱثۡنَيۡ عَشَرَ نَقِيبٗاۖ

وَقَالَ ٱللَّهُ إِنِّي مَعَكُمۡۖ لَئِنۡ أَقَمۡتُمُ ٱلصَّلَوٰةَ﴾

{Na kwa hakika Allah alichukua ahadi kwa wana wa Israili, na tukawateulia kutokana nao wakuu kumi na mbili. Na Allah akasema: Kwa yakini Mimi ni pamoja nanyi kama mkiswali}. (Al-Maidah: 12).

Na Luqman alimuusia mwanawe, akasema kumuambia:

﴿يَٰبُنَيَّ أَقِمِ ٱلصَّلَوٰةَ﴾

{Ewe mwanangu! Simamisha Swala}, (Luqman: 17).

Na [Allah] aliyetakasika aliamrisha umma zilizokuwa kabla yetu, akasema:

﴿وَمَآ أُمِرُوٓاْ إِلَّا لِيَعۡبُدُواْ ٱللَّهَ مُخۡلِصِينَ لَهُ ٱلدِّينَ حُنَفَآءَ وَيُقِيمُواْ ٱلصَّلَوٰةَ﴾

{Nao hawakuamrishwa ila wamuabudu Allah kwa kumtakasia Dini, wawe waongofu, na wasimamishe Swala}. (Al-Bayyinah: 5).

Na [Allah] aliyetukuka alimuamrisha Nabii wetu Muhammad swala na salamu zimshukie, akasema kumuambia:

﴿وَأَقِمِ ٱلصَّلَوٰةَ طَرَفَيِ ٱلنَّهَارِ وَزُلَفٗا مِّنَ ٱلَّيۡلِ﴾

{Na simamisha Swala katika ncha mbili za mchana na nyakati za usiku zilizo karibu na mchana} ,( Hud: 114).

Na akasema kuambia umma huu:

﴿وَأَقِيمُواْ ٱلصَّلَوٰةَ﴾

{Na simamisheni Swala}.( Al-Baqarah: 43).

Tumeamrishwa nayo katika hali ya hofu na amani, tukiwa safarini na mjini, hali ya uzima na ugonjwa, wala [uwajibu wa Swala] hauanguki kwa mukallaf kwa hali yoyote, ila kwa aliye na hedhi na damu ya uzazi, na mtoto huamrishwa kuitekeleza akifika miaka saba, na huchapwa kwa kuiwacha afikapo miaka kumi, na alikuwa [Mtume] swala na salamu «akichukia kulala kabla ya Swala ya ishai - ili asilale ikampita -, na akichukia

kuzungumza baada yake - ili kukesha kusije kumtia uzito kuiteleza [ya alfajiri] -» wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea. Allah aliwasifu waja wake waumini na sifa, alizianza na [sifa ya kuswali] Swala:

﴿قَدْ أَفْلَحَ ٱلْمُؤْمِنُونَ ۞ ٱلَّذِينَ هُمْ فِي صَلَاتِهِمْ خَٰشِعُونَ﴾

{Hakika wamefanikiwa Waumini * Ambao ni wanyenyekevu katika Swala zao}, (Al-Mu'minun: 1-2).

na akazihitimisha na Swala:

﴿وَٱلَّذِينَ هُمْ عَلَىٰ صَلَوَٰتِهِمْ يُحَافِظُونَ﴾

{Na ambao Sala zao wanazihifadhi}. (Al-Mu'minun: 9).

Nayo ni amali ipendezayo kwa Allah, Nabii swala na salamu za Allah zimshukie aliulizwa:

«Ni amali gani inayopendeza zaidi kwa Allah? Akasema: **Swala kwa wakati wake**, ikasemwa: kisha ni gani? [Nabii] Akasema: **Kisha ni kuwatenda wema wazazi wawili**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea. Ibnu Hajar Allah amrehemu amesema: «Kusubiri juu ya kuhifadhi Swala na kuzitekeleza ndani ya wakati wake, na kuhifadhi utenda wema kwa wazazi wawili, ni mambo ya lazima yenye kujikariri na kudumu, hasubiri katika kuchunga amri ya Allah ndani ya mambo haya isipokuwa *'Asswiddiquun'* [Waumini wa kweli kabisa]».

Allah kaihusu baina ya ibada zote kwa kuifaradhisha juu ya mbingu, na [katika kuifaradhisha] kamzungumzisha Nabii wetu Muhammad swala na Salamu za Allah zimshukie bila ya ukati, nazo ni tano kiidadi, lakini ni hamsini kiujira, na haikubaliwi ila kwa twahara ya kiwiliwili, mavazi na sehemu [unaposwali], na inakatazwa kutaharaki, kula na kuzungumza ndani yake, na hilo [la kukatazwa hayo] halipatikani katika ibada nyenginezo; kwa kuwa mja anapokuwa ndani yake huwa anazungumza kwa ukaribu na Mola Mlezi aliye Mkubwa kabisa, basi hapaswi kuchanganya jambo la kuzungumza na aliye adhimu na mambo mengine, na Allah yupo mbele ya uso wa anayeswali, na mja huwa karibu zaidi sana na Mola wake wakati amemsujudia.

Kuitekeleza ni katika sababu za kuingia Peponi, na kuuona Uso wa Allah Mkarimu, [Nabii] swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**Hakika mtamuona Mola wenu Mlezi kama mnavouona huu mwezi, hamtadhuriana katika kuuona** [wakaona baadhi bila wengine] **wala hamtapata tabu** [kwa kusongamana]**, basi mkiweza msishindwe kuswali**

**kabla ya kuchomoza jua** [Swala ya Al-Fajiri] **na kabla ya kuchwa kwake** [Swala ya Alasiri] **basi fanyeni**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea. Ibnu Rajab Allah amrehemu amesema: "[Neema] ya juu zaidi ndani ya Pepo ni kumuona Allah, na amali tukufu zaidi za duniani ni [Swala ya] Alfajiri na Alasiri; basi kwa kuzihifadhi [Swala hizi] inatarajiwa kuingia Peponi na kumuona Allah ndani yake ".

Ujira wake [Swala] hata kabla ya kuitekeleza ni mkubwa; kwani udhu unafuta dhambi,

na «**anayeenda Msikiti asubuhi au jioni; Allah humuandalia mashukio Peponi kila anapoenda wakati wa asubuhi au jioni**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea,

Na kila hatua unayopiga kuenda kuswali ni amali njema, na inakunyanyua daraja mbele ya Allah, na hatua ya pili inakufutia ovu.

Na Malaika humuombea aliyeingia Msikitini wakisema:

«**Ewe Allah msamehe, ewe Allah mrehemu; [huendelea kumuombea] madamu hajavunja udhu**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Na pamoja na dua za Malaika kwa mwenye kuingojea Swala, huandikiwa yumo ndani ya Swala kwa muda wote anaosubiri Swala, na akiwa ndani ya Swala anaingia katika vipindi vya msamaha:

«**Ambaye kusema kwake amiin kutaafiki kusema amiin kwa Malaika, atasamehewa dhambi zake zilizotangulia**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Na Dhikri ya baada ya kuitekeleza [Swala] inafuta dhambi; basi atakayemsabihi Allah na akamhimidi mara thalathini na tatu baada yake, na akaleta takbira thalathini na nne; atasamehewa dhambi zake zilizotangulia,

Na atakayeimarisha Misikiti ya Allah kwa kuswali ndani yake pamoja na kuwa na uchamngu, atakuwa miongoni mwa waumini, [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿إِنَّمَا يَعۡمُرُ مَسَٰجِدَ ٱللَّهِ مَنۡ ءَامَنَ بِٱللَّهِ وَٱلۡيَوۡمِ ٱلۡأٓخِرِ وَأَقَامَ ٱلصَّلَوٰةَ﴾

{Hakika wanaoamirisha misikiti ya Allah ni wale wanaomuamini Allah, na Siku ya Mwisho, na wakasimamisha Swala}, (At-Taubah: 18).

Na «**atakaye swali ishai katika jamaa, basi ni kama aliye swali usiku wote**», imepokewa na Muslim.

Nayo ni mlango mkubwa wa msamaha ndani ya muda mchache, Nabii

swala na salamu za Allah zimshukie aliushabihisha na mto; akasema:

«**Mnaonaje lau mto unapita katika mlango wa mmoja wenu, anaoga ndani yake kila siku mara tano, je kutabakia kitu katika uchafu wake?** Wakasema: Hakutabakia kitu katika uchafu wake, akasema**: basi hilo ni mfano wa Swala tano, Allah anafuta kwazo dhambi**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Na Nabii swala na salamu za Allah zimshukie:

«**Hakuna mtu yeyote Muisilamu atakayeingiliwa na Swala ya faradhi, basi akaboresha udhu wake, unyenyekevu wake na rukuu yake; ila itakuwa** [Swala hiyo] **ni yenye kufuta dhambi za kabla yake, madamu hajafanya ovu kubwa, na [hali] hii ni katika maisha yote**», imepokewa na Muslim.

Na manufaa yake ya kidunia hayahesabiki: ni yenye kuleta maisha bora, yenye kufungua riziki, yenye kuisahilisha [riziki], na mwisho mwema unapatikana kwa ajili yake; [Allah] aliyetakasika:

﴿وَأۡمُرۡ أَهۡلَكَ بِٱلصَّلَوٰةِ وَٱصۡطَبِرۡ عَلَيۡهَاۖ لَا نَسۡـَٔلُكَ رِزۡقٗاۖ نَّحۡنُ نَرۡزُقُكَۗ وَٱلۡعَٰقِبَةُ لِلتَّقۡوَىٰ﴾

{Na waamrishe watu wako kuswali, na uendelee mwenyewe kwa hayo. Sisi hatukuombi wewe riziki, bali Sisi ndio tunakuruzuku. Na mwisho mwema ni kwa mchamngu}. (Twaha: 132).

Ni yenye kukinga shari, yenye kuita kila kheri; [Mtume] swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**atakayeswali [Swala ya] asubuhi basi atakuwa katika amani na ulinzi wa Allah**», imepokewa na Muslim.

Ibnu Al-Qayyim Allah amrehemu amesema: "Na Swala ina athari ya ajabu katika kukinga na shari, hasa hasa inapopewa haki yake miongoni mwa kuikamilisha kwa dhahiri na siri, basi haijawahi patikana kinga ya shari za dunia na akhera, wala kuvutwa mazuri yake kama vile yanavyopatika hayo kupitia Swala", akasema [tena ibnu Al-Qayyim]: "Na inayo [Swala] athari ya ajabu katika kuhifadhi afya ya mwili na moyo, na kuhifadhi nguvu zao, na kukinga [mwili na moyo] kutokana na mambo mabaya, wala hawajawahi tahiniwa watu wawili kwa ulemavu, au ugonjwa, au msiba, au balaa, isipokuwa mwenye kuswali kati yao huwa na sehemu chache ya hayo, na mwisho wake unakuwa na salama zaidi".

Na balaa haijawahi ondolewa kama vile inavyoondolewa na Tawhidi na Swala, Allah alimuokoa Yunus salamu zimshukie tumboni mwa samaki

kwa ajili ya Swala:

﴿فَلَوۡلَآ أَنَّهُۥ كَانَ مِنَ ٱلۡمُسَبِّحِينَ ۞ لَلَبِثَ فِي بَطۡنِهِۦٓ إِلَىٰ يَوۡمِ يُبۡعَثُونَ﴾

{Na isingelikuwa ya kwamba yeye alikuwa ni miongoni mwa wanaomtakasa [Allah kwa Swala] * Bila ya shaka angelikaa tumboni mwake mpaka siku ya kufufuliwa}, (As-Swaaffaat: 143-144).

Na Daud salamu zimshukie alitahiniwa, basi hakupata pakukimbilia na toba yake na kuomba msamaha ila [ndani ya] Swala:

﴿فَٱسۡتَغۡفَرَ رَبَّهُۥ وَخَرَّ رَاكِعٗا وَأَنَابَ﴾

{Basi akamwomba msamaha Mola wake Mlezi, na akaanguka kusujudu na kutubia} ,( Swad: 24).

Na pindi Allah alipotaka kumtahini Maryam salamu zimshukie, azae bila ya kuwa na mume, alimuamrisha kuswali; ili jambo hilo liwe jepesi kwake:

﴿يَٰمَرۡيَمُ ٱقۡنُتِي لِرَبِّكِ وَٱسۡجُدِي وَٱرۡكَعِي مَعَ ٱلرَّٰكِعِينَ﴾

{Ewe Maryamu! Mnyenyekee Mola wako Mlezi na usujudu na urukuu pamoja na wanao rukuu}. (Al- Imran: 43).

Na [Mtume] swala na salamu zimshukie alikuwa anapofikwa na jambo zito akikimbilia katika Swala.

Allah ameamrisha Waumini kutaka msaada kupitia Swala katika hali zao zote:

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ ٱسۡتَعِينُواْ بِٱلصَّبۡرِ وَٱلصَّلَوٰةِۚ إِنَّ ٱللَّهَ مَعَ ٱلصَّٰبِرِينَ﴾

{Enyi mlioamini! Takeni msaada kwa subira na Swala. Hakika Allah yu pamoja na wanaosubiri} (Al-Baqarah: 153).,

Pindi tunapokumbwa na hamu ya jambo la dunia tunakimbilia kwa Swala ya 'istikhaarah', na pindi mwendo wa dunia unapobadilika [kupatwa kwa jua au mwezi] tunakimbilia kwa Swala ya 'Kusuuf', na wakati wa furaha tunamsujudia Allah kwa kumshukuru aliyotupa,

Na ulikuwa mlango mkuu wa Nabii swala na salamu za Allah zimshukie katika kushukuru ni Swala, basi alikuwa anaposwali [usiku] husimama hadi miguu yake ifure, Aisha Allah amridhie amesema:

«Kwa nini unafanya hivi ewe Mtume wa Allah na hali ushasamehewa dhambi zako zilizotangulia na zitakazokuja? [Mtume] akasema: **Basi hivi nisipende kuwa mja mwenye kushukuru**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Na akhera Swala itazitangulia amali zote zilizobaki, na itakuwa ndio ya

kwanza atakayohesabiwa mja siju ya Kiyama,

Na Swala ni katika sababu za kusuhubiana na Nabii swala na salamu za Allah zimshukie siku ya Kiyama, Mtu mmoja alimujia Nabii swala na salamu za Allah zimshukie, akasema:

«Nakuomba kusuhubiana nawe Peponi, [Mtume] akasema**: Basi nisaidie juu ya nafsi yako kwa kukithirisha sujudu**», imepokewa na Muslim.

Na Waumini watatofautiana na wanafiki kwa sijida; pindi Waumini watakapomuona Mola wao Mlezi [siku ya Kiyama] watapomoka kumsujudia, na wanafiki watakapotakwa kusujudu hawataweza, iwe ni adhabu kwao, [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿يَوۡمَ يُكۡشَفُ عَن سَاقٖ وَيُدۡعَوۡنَ إِلَى ٱلسُّجُودِ فَلَا يَسۡتَطِيعُونَ﴾

{Siku utakapowekwa wazi Mundi [wa Allah usiofanana na chochote], na wataitwa kusujudu, lakini hawataweza}, (Al-Qalam: 42).

Na lau Muisilamu ataingia Motoni kwa dhambi, basi Moto hautagusa shehemu zake za kusujudia.

Nayo ni faradhi adhimu Allah kaifanya kuwa alama [ya kutofautisha] baina ya ukafiri na imani; [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

«**Baina ya mtu na baina ya ushirikina na ukafiri ni kuacha Swala**», imepokewa na Muslim,

Na [Allah] aliyetakasika amewaahidi Jahanamu wale wenye kuipoteza; akasema:

﴿فَخَلَفَ مِنۢ بَعۡدِهِمۡ خَلۡفٌ أَضَاعُواْ ٱلصَّلَوٰةَ وَٱتَّبَعُواْ ٱلشَّهَوَٰتِۖ فَسَوۡفَ يَلۡقَوۡنَ غَيًّا﴾

{Lakini wakaja baada yao walio wabaya, wakaacha Sala, na wakafuata matamanio. Basi watakuja kuta malipo ya ubaya}, (Maryam: 59).

Na makafiri wataambiwa:

﴿مَا سَلَكَكُمۡ فِي سَقَرَ * قَالُواْ لَمۡ نَكُ مِنَ ٱلۡمُصَلِّينَ﴾

{Ni nini kilicho kupelekeni Motoni? * Waseme: Hatukuwa miongoni waliokuwa wakisali}. (Al-Muddathiir: 42-43).

Umar ibnul Khattwaab Allah amridhie amesema: "Yule ambaye ameacha Swala hana sehemu yoyote katika Uisilamu".

Na baada ya haya yaliotangulia, enyi Waisilamu:

La wajibu juu ya kila mwenye akili aliyebaleghe ni ahifadhi Swala, na awaamrishe nayo watu wake, ni hii ndio njia ya Manabii salamu ziwashukie; kwani hiyo ni yenye kumridhisha Mola Mlezi, ni yenye kufuta

dhambi, ni yenye kunyanyua daraja, ni yenye kukusanya kheri, na ni yenye kukataza kila shari, ndani yake mna kutengea kwa hali iliopo na mwisho, kuafikiwa, utulivu wa fikra, maisha makunjufu, baraka ya mali, utulivu wa nyumba na kuwa wema kwa kizazi.

***'Audhu billaahi mina sh-shaitwaani rrajiim'***

﴿أَقِمِ ٱلصَّلَوٰةَ لِدُلُوكِ ٱلشَّمۡسِ إِلَىٰ غَسَقِ ٱلَّيۡلِ وَقُرۡءَانَ ٱلۡفَجۡرِۖ إِنَّ قُرۡءَانَ ٱلۡفَجۡرِ كَانَ مَشۡهُودٗا﴾

{Shika Sala jua linapopinduka mpaka giza la usiku, na Qur'ani ya al fajiri. Hakika Qur'ani ya alfajiri inashuhudiwa [na Malaika] daima} (Al-Isra: 78).

.

Allah anibarikie mimi na nyinyi katika Qur-ani tukufu...

## HOTUBA YA PILI

Sifa njema zote anastahili Allah kwa wema Wake [kwetu], na shukrani zote anastahili Yeye kwa kutuafikia na kutuneemesha, na nashuhudia ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake hana mshirika; ili kuadhimisha shani yake, na nashuhudia ya kwamba Nabii wetu Muhammad ni mja Wake [Allah] na Mtume wake, swala na salamu nyingi za Allah zimshukie yeye, watu wa nyumba yake na Masahaba wake.

**Enyi Waisilamu:**

Allah amewajibishia wanaume kutekeleza Swala ya jamaa Misikitini, [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿وَٱرۡكَعُواْ مَعَ ٱلرَّٰكِعِينَ﴾

{na mrukuu pamoja na wanaorukuu} (Al-Baqarah: 43).

Na Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alitaka kuchoma nyumba za wanaoacha kuswali jamaa, akasema:

«**Hakika Swala nzito zaidi kwa wanafiki ni Swala ya Ishai na Swala ya Alfajiri; na lau wanajua yaliomo ndani yake** [Swala mbili hizi] **wangezijia hata kama ni kwa kutambaa, na hakika nilitaka niamrishe Swala isimamishwe, kisha nimuamrishe mtu awaswalishe watu, kisha niondoke wakiwa pamoja nami watu waliobeba matita ya kuni, kuwaendea watu wasioshuhudia Swala [ya jamaa], niwachomee moto nyumba zao**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea,

Wala Nabii hakumruhusu yule mtu chongo, aliyekosa wa kumuongoza [njia] kuacha Swala ya jamaa; bali alisema kumuambia:

«**Je unasikia mwito wa Swala?** Akasema: Ndio, [Nabii] akasema: **Basi uitikie**», imepokewa na Muslim.

Basi Tuikimbilieni tuikimbilieni Swala ya jamaa! Kwani ni nuru ya uso, na ni dalili ya imani, na kwayo unapatikana ukunjufu wa kifua, na ujuu wa cheo.

Kisha jueni kuwa Allah amewaamrisha kumswalia na kumsalimia Nabii wake...

# UWAJIBU WA SWALA YA JAMAA[1]

Sifa za ukamilifu zote ni za Allah, tunamuhimidi, tunamuomba msaada, tunamuomba msamaha, na tunajilinda na Allah kutokana na shari za nafsi zetu, na kutokana na amali zetu mbovu, yule ataongozwa na Allah, basi hakuna wa kumpoteza, na atakaye mpoteza hakuna wa kumuongoza, nashuhudia ya kwamba hapana apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake, hana mshirika, na nashuhudia kuwa Nabii wetu Muhammad ni mja wake na Mtume wake, swala na salamu za Allah nyingi zimshukie yeye, watu wake, na masahaba wake.

**Ama baada ya himdi hii:**

Basi enyi waja wa Allah mcheni Allah haki ya kumcha, na mchungeni [chungeni amri zake na makatazo yake] katika siri na minong'ono.

**Enyi Waislamu:**

Allah ameamrisha viumbe vyake kumtakasia ibada; basi haikubaliwi amali bila ya Tawhidi, na [Allah] aliyetakasika alifuatisha ibada baada ya kutaja jambo la kumfanyia Yeye Tawhidi, na akakithirisha kulitaja hilo,

Na akaamrisha nalo Mitume; akasema kumuambia Musa salamu zimshukie:

﴿وَأَقِمِ ٱلصَّلَوٰةَ لِذِكۡرِيٓ﴾

{na simamisha swala kwa ajili ya kunitaja na kunikumbuka Mimi} (Twaha: 14)

Na Isa salamu zimshukie alisema:

﴿وَأَوۡصَٰنِي بِٱلصَّلَوٰةِ وَٱلزَّكَوٰةِ مَا دُمۡتُ حَيّٗا﴾

{Na ameniusia Swala na Zaka maadamu ni hai}, (Maryam: 31).

Na Ibrahim salamu zimshukie alimuomba Mola wake Mlezi awe Yeye na kizazi chake ni miongoni mwa wenye kuitekeleza:

﴿رَبِّ ٱجۡعَلۡنِي مُقِيمَ ٱلصَّلَوٰةِ وَمِن ذُرِّيَّتِيۚ رَبَّنَا﴾

{Mola wangu Mlezi! Nijaalie niwe mwenye kushika Sala, na katika dhuriya

[1] Imetolewa siku ya Ijumaa, tarehe nne ya mwezi wa Shaabani, mwaka elfu moja, mia nne na thalathini na moja hijria, ndani ya Msikiti wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie.

zangu pia, ewe Mola wetu} (Ibrahim: 40).

Na [Allah] alimsifu Ismail salamu zimshukie kule kuwaamrisha watu wake nayo:

﴿وَكَانَ يَأۡمُرُ أَهۡلَهُۥ بِٱلصَّلَوٰةِ﴾

{na alikuwa akiwaamrisha watu wake Swala}, (Maryam: 55).

Nayo ni ahadi aliyoichukua Allah juu ya umma zilizotangulia:

﴿وَإِذۡ أَخَذۡنَا مِيثَٰقَ بَنِيٓ إِسۡرَٰٓءِيلَ لَا تَعۡبُدُونَ إِلَّا ٱللَّهَ
وَبِٱلۡوَٰلِدَيۡنِ إِحۡسَانٗا وَذِي ٱلۡقُرۡبَىٰ وَٱلۡيَتَٰمَىٰ وَٱلۡمَسَٰكِينِ وَقُولُواْ لِلنَّاسِ حُسۡنٗا وَأَقِيمُواْ ٱلصَّلَوٰةَ﴾

{Na tulipofunga agano na Wana wa Israili: Hamtamuabudu yeyote ila Allah; na muwafanyie wema wazazi na jamaa na mayatima na masikini, na semeni na watu kwa wema, na simamisheni Swala} (Al-Baqarah: 83).

Nayo ni miongoni mwa wasia wa Luqman kwa mtoto wake,

﴿يَٰبُنَيَّ أَقِمِ ٱلصَّلَوٰةَ﴾

{Ewe mwanangu simamisha Swala} (Luqman: 17).

Na umeamrishwa umma huu kuihifadhi

﴿حَٰفِظُواْ عَلَى ٱلصَّلَوَٰتِ وَٱلصَّلَوٰةِ ٱلۡوُسۡطَىٰ وَقُومُواْ لِلَّهِ قَٰنِتِينَ﴾

{Zilindeni Swala, na hasa Swala ya katikati, na simameni kwa ajili ya Allah nanyi ni wenye kunyenyekea}, (Al-Baqarah: 238).

Na wanawake waliamrishwa kuitekeleza:

﴿وَأَقِمۡنَ ٱلصَّلَوٰةَ وَءَاتِينَ ٱلزَّكَوٰةَ﴾

{na simamisheni Swala na toeni Zaka}, (Al-Baqarah: 238).

Nayo ni miongoni mwa misingi ya Imani; Nabii swala na salamu zimshukie alisema kuwaambia kundi la [kabila la] Bani AbdilQays:

«**Je mnajua ni nini kumuamini Allah? Ni kushuhudia kuwa hapana apasaye kuabudiwa ila Allah, na kuwa Muhammad ni Mtume wa Allah, kusimamisha Swala na kutoa Zaka**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea,

Na cheo chake katika Dini ni baada ya Shahada mbili, na Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alikuwa akiiamrisha mwanzoni mwa ulinganizi wake, 'Hiraqlu' [mfalme wa warumi] alisema kumuambia Abu Sufyani: «Ana waamrisha nini? Yaani: Mtume swala na salamu za Allah zimshukie, Abu Sufyani akasema: nikasema kujibu: Anatuamrisha Swala, Zaka, kuunga kizazi na kujizuia [kutokana na mambo duni na ya aibu]»,

wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Nayo ni amali inayopendeza zaidi kwa Allah; Nabii swala na salamu za Allah zimshukie aliulizwa:

«Ni amali gani inapendeza zaidi kwa Allah? Akasema: **Ni Swala kwa wakati wake**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Na ilihusiwa baina ya ibada zote kwa kufaradhishwa mbinguni, basi hakushuka nayo ardhini Malaika; bali Allah alimzungumzisha Nabii wetu Muhammad swala na salamu zimshukie [wakati anamfaradhishia Swala] bila ya ukati [wa Malaika], [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

«**Kisha nikapelekwa katika 'Sidarat Al-Muntahaa'** [Mkunazi Ulio katika mbingu ya saba], **basi Allah akanifunulia alionifunulia, akanifaradhishia Swala hamsini ndani ya kila mchana na usiku**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Cheo chake kimeadhimishwa, ikafaradhishwa Swala hamsini, kisha ikapunguzwa hadi tano kiidadi, na ikabakia hamsini kithawabu.

Masahaba waliipenda, wakawa wanaitekeleza hata katika sehemu ngumu zaidi; Jaabir Allah amridhie amesema: «Tulipigana vita pamoja na Mtume wa Allah swala na salamu zimshukie na watu [miongoni mwa makafiri], wakatupiga vita vikali, washirikina wakasema: hakika itaiwajia Swala, ambayo inapendeza zaidi kwao kuliko watoto wao...», imepokewa na Muslim.

Na [Masahaba] walimpa Mtume 'bai-ah' juu yake [kuisimamisha Swala], Jarir ibnu Abdillah amesema: «Nilimpa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie 'bai-ah' juu ya kusimamisha Swala, kutoa Zaka, na kumnasihi kila Muisilamu», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Swala ni usaidizi bora katika mambo ya kidini na dunia; inampamba mtu na tabia njema, na inamkomesha na machafu na maovu, ni yenye kufuta makosa na madhambi, Nabii swala na salamu za Allah zimshukie aliifananisha na mto unaotembea wenye kuondosha uchafu (hili wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea). Inamuhifadhi mja kutokana na shari na mangamivu makubwa; [Mtume] swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**atakaye swali** [Swala ya] **asubuhi basi atakuwa katika amani na ulinzi wa Allah**», imepokewa na Muslim.

Inamuondoshea mja misiba, fitina, maafa na yenye kuleta aibu; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿وَٱسۡتَعِينُواْ بِٱلصَّبۡرِ وَٱلصَّلَوٰةِ﴾

{Na takeni msaada kupitia Subira na Swala} ,( Al-Baqarah: 45).

Ibnu Kathiir Allah amrehemu amesema: "Swala ni usaidizi mkubwa juu ya kukita katika jambo [la Dini]».

[Swala] Inafungua milango ya riziki na kuisahilisha; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿فَنَادَتۡهُ ٱلۡمَلَٰٓئِكَةُ وَهُوَ قَآئِمٞ يُصَلِّي فِي ٱلۡمِحۡرَابِ أَنَّ ٱللَّهَ يُبَشِّرُكَ بِيَحۡيَىٰ﴾

{Basi Malaika wakamnadi hali kasimama akiswali ndani ya chumba chake cha ibada: Hakika Mwenyezi Mungu anakubashiria Yahya}, (Al-Imran: 39).

Na alisema kuhusu Maryam salamu zimshukie:

﴿كُلَّمَا دَخَلَ عَلَيۡهَا زَكَرِيَّا ٱلۡمِحۡرَابَ وَجَدَ عِندَهَا رِزۡقٗا﴾

{Kila mara Zakariya alipoingia chumbani kwake alimkuta na vyakula} (Al-Imran: 37).

Inautia mwili nguvu na inakikunjua kifua; pindi mja anapoamka na kumtaja Allah, kisha akatawadha na kuswali rakaa mbili:

«**Basi atakuwa** - siku yake ile - **mchangamfu mwenye nafsi nzuri**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Nabii swala na salamu za Allah zimshukie ameisifu kuwa ni nuru; akasema:

«**Na Swala ni nuru**», imepokewa na Muslim.

Nayo ni miongoni mwa yenye kuwajibisha kuingia Peponi na kupata daraja za juu ndani yake; Thawbani Allah amridhie alimuuliza Nabii swala na salamu za Allah zimshukie akasema:

«Nijulishe amali ambayo Allah atanitia nayo Peponi - au alisema: amali ipendezayo zaidi kwa Allah -? [Mtume] akasema: **Jilazimishe kumsujudia Allah sana, kwani wewe haumsujudii Allah sijida moja isipokuwa Allah hukunyanyua kwayo daraja, na hukufutia kwayo dhambi**», imepokewa na Muslim.

Swala ni katika sababu za kusuhubiana na Nabii swala na salamu za Allah zimshukie ndani ya Pepo; Rabii'a ibnu Ka'b Allah amridhie amesema:

«Mtume wa Allah swala na salamu zimshukie aliniambia: **omba**. Basi nikasema: Nakuomba kusuhubiana nawe ndani ya Pepo. Akasema: **Au isiokuwa hilo?** Nikasema: Ni hilo tu. Akasema**: Basi nisaidie juu ya nafsi yako kwa wingi wa kusujudu**», imepokewa na Muslim.

[Swala] ilikuwa ndio utulivu wa jicho la Nabii swala na salamu za Allah zimshukie, na [Mtume] akaifanya ndio wasia wake wa mwisho wa maisha yake; Anas Allah amridhie amesema:

«Ulikuwa wingi wa wasia wake [Mtume] swala na salamu za Allah zimshukie pindi alipofikwa na mauti ni [kauli yake]: [Nawausia kuhifadhi] **Swala! Na yale yaliomilikiwa na mikono yenu ya kiume!**», imepokewa na Ahmad.

Fadhila zake ni nyingi, na aina za manufaa yake ni nyingi, Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema kuihusu:

«**Na lau wanajua yaliomo ndani yake** [Swala ya Alfajiri na Ishai] **wangezijia hata kama ni kwa kutambaa**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Imefaradhishwa kwa kila Muisilamu kuitekeleza popote pale alipo na kwa hali yoyote ile; [Mtume] swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**Na ardhi yote imefanywa kwangu kuwa ni Msikiti** [sehemu ninayoweza kuswali] **na twahara** [sehemu ninayoweza kujitwahirisha kwa kutayamamu], **basi mtu yeyote ataingiliwa na Swala, ataswali popote alipo**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Na Uisilamu umeifanya [Swala] ndio mizani [ya kutafautisha] baina ya Uisilamu na ukafiri;Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**Baina ya mtu na baina ya ushirikina na ukafiri ni kuacha Swala**», imepokewa na Muslim.

Umar ibnul Khattwaab Allah amridhie amesema: "Hana Uisilamu yule ambaye hakuswali", na ibnu Mas-uud Allah amridhie amesema: "aliyeacha Swala basi hana Dini".

Na kuitekeleza ndani ya wakati wake ni jambo la wajibu; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿فَخَلَفَ مِنۢ بَعۡدِهِمۡ خَلۡفٌ أَضَاعُواْ ٱلصَّلَوٰةَ وَٱتَّبَعُواْ ٱلشَّهَوَٰتِۖ فَسَوۡفَ يَلۡقَوۡنَ غَيًّا﴾

{Lakini wakaja baada yao walio wabaya, wakaacha Swala, na wakafuata matamanio. Basi watakuja kuta malipo ya ubaya}. (Maryam: 59).

Umar ibn Abdul-Aziz Allah amrehemu amesema: "Kuiacha kwao haikuwa ni kuiacha kabisa, lakini waliacha wakati wake [yaani: wakiitoa nje ya wakati wake]",

Is-haaq ibnu Raahooyah Allah amrehemu amesema: "Rai ya wenye elimu - kutoka enzi za Mtume swala na salamu za Allah zimshukie hadi leo

hii -: ni kuwa aliyeacha Swala kimakusudi pasina udhuru hadi wakati wake utoke ni kafiri».

Allah amewajibisha kuitekeleza ndani ya Nyumba [Misikiti] za Allah kwa jamaa; bali Nabii swala na salamu za Allah zimshukie hakumpa udhuru wa kutoiijia [Swala Msikitini] hata yule aliyekosa macho;

«Alikuja chongo kwa Nabii swala na salamu za Allah zimshukie, akasema: Ewe Mtume wa Allah! Hakika mimi ni kipofu, sina wa kuniongoza kuja Msikitini. Mtume swala na salamu za Allah zimshukie akasema: **Je unasikia mwito wa Swala?** Akasema: Ndio, [Nabii] akasema: **Basi uitikie**», imepokewa na Muslim.

Na [Mtume] swala na salamu za Allah zimshukie akasema:

«**Hakika nilitaka niamrishe Swala isimamishwe, kisha nimuamrishe mtu awashwalishe watu, kisha Niondoke wakiwa pamoja nami watu waliobeba matita ya kuni, kuwaendea watu wasioshuhudia Swala [ya jamaa], niwachomee moto nyumba zao**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Na katika riwaya nyingine:

«**Lau majumbani kusingekuwa na wanawake na watoto** [ambao si wajibu kwao Swala ya jamaa]», imepokewa na Ahmad.

Ibnu Hajar Allah amrehemu amesema: «Hadithi hii iko wazi kabisa kuwa Swala ya jamaa ni faradhi ya kila mmoja; sababu lau ingekuwa ni sunnah hangemtishia kumchoma moto aliyeiacha, na lau ingekuwa faradhi ya kutoshelezana [ambayo lau wataifanya baadhi, basi baadhi wengine hawatapata dhambi kuiacha] basi ingekuwa ishapatikana [ishatosha] kwa [kufanywa] na Mtume swala na salamu za Allah zimshukie pamoja waliokuwa naye»

Na kufanya upungufu katika Swala ya jamaa; ni miongoni mwa sababu za shetani kumtwala mja; Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**Hakutakuwa na watatu mjini au mashambani [ambao] hakusimamishi kwao Swala [ya jamaa]; ila shetani hutawala**», imepokewa na Abu Daaud.

Ibnu Mas-uud Allah amridhie amesema: "Hakika nimejua hali ya Masahaba hawakuwa wakiiacha [Swala ya ijumaa] isipokuwa mnafiki unao julikana unafiki wake".

Na kuihudhuria ni alama ya Imani; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿إِنَّمَا يَعۡمُرُ مَسَٰجِدَ ٱللَّهِ مَنۡ ءَامَنَ بِٱللَّهِ وَٱلۡيَوۡمِ ٱلۡأٓخِرِ وَأَقَامَ ٱلصَّلَوٰةَ وَءَاتَى ٱلزَّكَوٰةَ وَلَمۡ يَخۡشَ إِلَّا ٱللَّهَ﴾

{Hakika wanaoamirisha misikiti ya Allah ni wale wanaomuamini Allah, na Siku ya Mwisho, na wakasimamisha Swala na wakatoa Zaka na wasimche ila Allah}, (At-Taubah: 18).

Na Masahaba walikuwa wakiitekeleza [Swala] kwa jamaa hata lau patakuwa na uzito; ibnu Mas-uud Allah amridhie amesema: "Hakika nimemuona mtu akiletwa akiwa anatembea akiwa ameshikiliwa baina ya watu wawili hadi asimamishwe katika safu", Ar-Rabi'i ibnu Khaitham amesema: "Mukiweza kuiijia basi ijieni hata kama ni kwa kutambaa",

Na jambo la mwisho aliloliona Mtume kwa Masahaba zake kabla kufa kwake, aliwaona hali wakiswali kwa jamaa, Anas ibnu Maalik Allah amridhie: «Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alifungua pazia ya chumba chake akiwa katika maradhi aliokufa ndani yake; akaangalia watu wakiwa katika safu wanaswali, akatabasamu kucheka, asema Anas: ukawa mtazamo wa mwisho aliowatazama nao Masahaba wake», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Allah yupo mbele ya uso wa mwenye kuswali, na unyenyekevu ndio roho ya Swala,

na «Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alikuwa akiswali kifua chake kinatoa sauti mfano wa sauti ya chungu kinachotokota kwa kulia», imepokewa na Abu Daaud.

Ibnu Abbaas Allah amridhie amesema: "Hauna katika [thawabu za] Swala yako isipokuwa ile sehemu ulioifahamu», Al-Karimu Allah amrehemu amesema:" alikuwa sheikhul Islaam anapoingia katika Swala viungo vyake vinatetemeka - yaani: kwa ajili ya hofu kubwa ya Allah -,",

Basi ilekeeni [Swala] kwa unyenyekevu na furaha kwa kuitekeleza kwa jamaa; roho zenu zitatwahirika, na madhambi ya ndimi zenu na viungo vyenu yatafutwa, na daraja zenu zitanyanyuliwa.

***'Audhu billaahi mina sh-shaitwaani rrajiim'***

﴿وَأَقِيمُواْ ٱلصَّلَوٰةَ وَءَاتُواْ ٱلزَّكَوٰةَ وَأَطِيعُواْ ٱلرَّسُولَ لَعَلَّكُمۡ تُرۡحَمُونَ﴾

{Na simamisheni Swala, na toeni Zaka, na mt'iini Mtume, ili mpate kurehemewa}. (An-Nur: 56).

Allah anibarikie mimi na nyinyi katika Qur-ani tukufu...

## HOTUBA YA PILI

Sifa njema zote anastahili Allah kwa wema Wake [kwetu], na shukrani zote astahili Yeye kwa kutuafikia na kutuneemesha, na nashuhudia ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake hana mshirika; ili kuadhimisha shani yake, na nashuhudia ya kwamba Nabii wetu Muhammad ni mja Wake [Allah] na Mtume wake, swala na salamu za Allah za ziada zimshukie yeye, watu wa nyumba yake na Masahaba wake.

**Enyi Waislamu:**

Swala ni sababu ya kufaulu, na atakayetembea kuiendea hatapiga hatua ila Allah atamnyanyua nayo daraja, na kumfutia dhambi, na Malaika wanamuombea madamu bado yupo katika sehemu yake aliyoswali ndani yake, wanasema:

«**Ewe Allah msamehe, ewe Allah mrehemu**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Na «**atakayeswali Ishai kwa jamaa ni kana kwamba amesimama nusu usiku [kwa ibada], na atakayeswali Alfajiri kwa jamaa ni kana kwamba ameswali usiku wote**», imepokewa na Muslim.

Na yule ambaye moyo wake utafungamana na Swala, akawa ni mwenye kusubiri mwito wa Swala inayofuatia, atakuwa chini ya kivuli cha 'Arshi' yake [Allah].

Basi zitekelezeni Swala za faradhi ndani ya nyumba za Allah kwa jamaa, hali ya kuwa nafsi zenu zina raha na hilo, na vifua vyenu vina ukunjufu, kwa hilo mtapata thawabu za Mola wenu Mlezi.

Kisha jueni kuwa Allah amewaamrisha kumswalia na kumsalimia Nabii wake…

# ZAKA

# ZAKA[1]

Sifa za ukamilifu zote ni za Allah, tunamhimidi, tunamuomba msaada, tunamuomba msamaha, na tunajilinda na Allah kutokana na shari za nafsi zetu, na kutokana na amali zetu mbovu, yule ataongozwa na Allah, basi hakuna wa kumpoteza, na atakayempoteza hakuna wa kumuongoza, nashuhudia ya kwamba hapana apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake, hana mshirika, na nashuhudia kuwa Nabii wetu Muhammad ni mja wake na Mtume wake, swala na salamu nyingi za Allah zimshukie yeye, watu wake, na masahaba wake.

**Ama baada ya himdi hii:**

Basi enyi waja wa Allah mcheni Allah haki ya kumcha; kwani kwa uchamngu akili na nyoyo zinapata nuru, na makosa na madhambi yanafutwa,

**Enyi Waisilamu:**

Allah ameumba binadamu na majini kwa lengo la kumuabudu Yeye, naye aliyetakasika hana mahitaji kwao, wala viumbe hawana kujitosheleza bila ya kumuhitaji Yeye, kwani Yeye ndiye mwenye kuondoa yenye kuwadhuru, na Yeye ndiye mwenye kuwanufaisha; na kwa ajili ya kumuhitajia kwao ndio akawawajibisha kumuabudu, akasema:

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلنَّاسُ ٱعۡبُدُواْ رَبَّكُمُ ٱلَّذِي خَلَقَكُمۡ وَٱلَّذِينَ مِن قَبۡلِكُمۡ لَعَلَّكُمۡ تَتَّقُونَ﴾

{Enyi watu! Muabuduni Mola wenu Mlezi aliye kuumbeni nyinyi na wale wa kabla yenu, ili mpate kuokoka}, (Al-Baqarah: 21).

Na Uislamu umejengwa juu ya nguzo tano na kusimama juu yake, Shahada mbili ndio ya kwanza, Swala za faradhi ndio ya pili, na Zaka ndio nguzo ya tatu kati ya nguzo kubwa za Uisilamu, nayo ni mwendani wa Swala katika sehemu nyingi katika aya za Qur-ani,

Isa salamu zimshukie aliizungumza [Zaka] hali yuko katika mlezi, akasema:

﴿وَأَوۡصَٰنِي بِٱلصَّلَوٰةِ وَٱلزَّكَوٰةِ مَا دُمۡتُ حَيّٗا﴾

{Na ameniusia Swala na Zaka maadamu ni hai}, (Maryam: 31).

Na [Allah] alimsifu Ismail salamu zimshukie kule kuwaamrisha watu wake nayo:

---

[1] Imetolewa katika hotuba zilizotolewa ndani ya Al-Msjid An-Nabawi.

﴿وَكَانَ يَأۡمُرُ أَهۡلَهُۥ بِٱلصَّلَوٰةِ وَٱلزَّكَوٰةِ وَكَانَ عِندَ رَبِّهِۦ مَرۡضِيّٗا﴾

{na alikuwa akiwaamrisha watu wake Swala na Zaka, na alikuwa mbele ya Mola wake Mlezi mwenye kuridhiwa}. (Maryam: 55).

Na kwa ukubwa wa cheo chake [Zaka] ndio [Allah] akaiwajibisha kwa Manabii na Mitume wake; basi akamteremshia Ibrahim, Is-haaq na Ya'qub amri ya kuisimamisha; akasema:

﴿وَأَوۡحَيۡنَآ إِلَيۡهِمۡ فِعۡلَ ٱلۡخَيۡرَٰتِ وَإِقَامَ ٱلصَّلَوٰةِ وَإِيتَآءَ ٱلزَّكَوٰةِ﴾

{Na tukawafunulia watende kheri, na washike Swala, na watoe Zaka}, (Al-Anbiya: 73).

Nayo ni ahadi aliyoichukua Allah juu ya umma zilizotangulia, [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿وَإِذۡ أَخَذۡنَا مِيثَٰقَ بَنِيٓ إِسۡرَٰٓءِيلَ لَا تَعۡبُدُونَ إِلَّا ٱللَّهَ
وَبِٱلۡوَٰلِدَيۡنِ إِحۡسَانٗا وَذِي ٱلۡقُرۡبَىٰ وَٱلۡيَتَٰمَىٰ وَٱلۡمَسَٰكِينِ وَقُولُواْ لِلنَّاسِ حُسۡنٗا وَأَقِيمُواْ ٱلصَّلَوٰةَ وَءَاتُواْ ٱلزَّكَوٰةَ﴾

{Na tulipofunga agano na Wana wa Israili: Hamtamuabudu yeyote ila Allah; na muwafanyie wema wazazi na jamaa na mayatima na masikini, na semeni na watu kwa wema, na simamisheni Swala, toeni Zaka}, (Al-Baqarah: 83).

Na wanawake waliamrishwa kuitekeleza:

﴿وَأَقِمۡنَ ٱلصَّلَوٰةَ وَءَاتِينَ ٱلزَّكَوٰةَ﴾

{na simamisheni Swala na toeni Zaka}, (Al-Ahzab: 33).

Na Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alikuwa akiiamrisha [Zaka] mwanzoni mwa ulinganizi wake, 'Hiraqlu' [mfalme wa warumi] alisema kumuambia Abu Sufyani: «Anawaamrisha nini? Yaani: Mtume swala na salamu za Allah zimshukie, Abu Sufyani akasema: nikasema kujibu: Anatuamrisha Swala, Zaka, kuunga kizazi na kujizuia [kutokana na mambo duni na ya aibu]», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Na Nabii swala na salamu za Allah zimshukie aliwausia nayo Umma wake, alikuja mbedui [A'raabii] kwa Nabii swala na salamu za Allah zimshukie, akasema:

«Nijulishe amali endapo nitaifanya nitaingia Peponi, [Mtume] akasema: **Muabudu Allah wala usimshirikishe na chochote, usimamishe Swala iliowajibishwa, utoe Zaka iliofaradhishwa, na ufunge Ramadhani**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Mashaba waliipenda wakawa wanaitekeleza, Na walimpa Mtume 'bai-ah' juu yake [kutoa Zaka], Jarir ibnu Abdillah amesema: «Nilimpa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie 'bai-ah' juu ya kusimamisha Swala, kutoa Zaka, na kumnasihi kila Muisilamu», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Nayo ni miongoni mwa misingi ya Imani; Nabii swala ma salamu zimshukie alisema kuwaambia kundi la [kabila la] Bani AbdilQays:

«**Je mnajua ni nini kumuamini Allah? Ni kushuhudia kuwa hapana apasaye kuabudiwa ila Allah, na kuwa Muhammad ni Mtume wa Allah, kusimamisha Swala na kutoa Zaka**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea,

Nayo [Zaka] ni amani kwa yule aliyekuwa mshirikina kabla kisha akasilimu:

﴿فَإِن تَابُواْ وَأَقَامُواْ ٱلصَّلَوٰةَ وَءَاتَوُاْ ٱلزَّكَوٰةَ فَخَلُّواْ سَبِيلَهُمۡ﴾

{Lakini wakitubu, wakasimamisha Swala, na wakatoa Zaka, basi waachilieni}, (At-Taubah: 5).

Nayo ni kinga ya damu na mali, [Nabii] swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**Nimeamrishwa kuwapiga vita watu hadi washuhudie ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah, na kuwa Muhammad ni Mtume wa Allah, na wasimamishe Swala, na watoe Zaka; basi pindi wakifanya hayo watakuwa wamekinga damu zao na mali yao isipokuwa kwa haki ya Uisilamu, na kuwahesabu ni juu ya Allah**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea,

Nayo inawajibisha undugu katika Dini:

﴿فَإِن تَابُواْ وَأَقَامُواْ ٱلصَّلَوٰةَ وَءَاتَوُاْ ٱلزَّكَوٰةَ فَإِخۡوَٰنُكُمۡ فِي ٱلدِّينِ﴾

{Basi wakitubu na wakasimamisha Swala na wakatoa Zaka, basi ni ndugu zenu katika Dini}. (At-Taubah: 11).

Na mafungamano ya mapenzi baina ya Waisilamu yanapata nguvu kwayo, na inavuta baraka, nyongeza na badili [kilikosekana] kutoka kwa Allah, [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿وَمَآ أَنفَقۡتُم مِّن شَيۡءٖ فَهُوَ يُخۡلِفُهُۥ﴾

{Na chochote mnacho kitoa basi Yeye huwapa badala yake.} (Saba: 39).

Na kwa kuitoa [Zaka] kunapatikana usafi wa nafsi na utakatifu wake;

[Allah] aliyetakasikika amesema:

﴿خُذۡ مِنۡ أَمۡوَٰلِهِمۡ صَدَقَةٗ تُطَهِّرُهُمۡ وَتُزَكِّيهِم بِهَا﴾

{Chukua sadaka katika mali zao, uwasafishe na uwatakase kwazo}, (At-Taubah: 103).

Na kusalimika kutokana na Moto ni malipo ya yule aliyeitakasa nafsi yake kwa [kutoa Zaka ya] mali yake, [Allah] aliye mkubwa na aliye juu:

﴿وَسَيُجَنَّبُهَا ٱلۡأَتۡقَى ۞ ٱلَّذِي يُؤۡتِي مَالَهُۥ يَتَزَكَّىٰ﴾

{Na mchamngu ataepushwa nao [Moto] * Ambaye hutoa mali yake kwa ajili ya kujitakasa}, (Al-Lail: 17-18).

Inamkinga mtu na adhabu za dhambi, na inamuepushia misiba na majanga makubwa, [Allah] mwenye ushindi na ukubwa amesema:

﴿فَأَمَّا مَنۡ أَعۡطَىٰ وَٱتَّقَىٰ ۞ وَصَدَّقَ بِٱلۡحُسۡنَىٰ ۞ فَسَنُيَسِّرُهُۥ لِلۡيُسۡرَىٰ ۞ وَأَمَّا مَنۢ بَخِلَ وَٱسۡتَغۡنَىٰ ۞ وَكَذَّبَ بِٱلۡحُسۡنَىٰ ۞ فَسَنُيَسِّرُهُۥ لِلۡعُسۡرَىٰ﴾

{Ama mwenye kutoa na akamchamngu * Na akalisadikisha lilio jema [Neno la Shahada] * Tutamsahilishia yawe mepesi * Na ama mwenye kufanya ubahili, na asiwe na haja ya wenzake * Na akakanusha lilio jema * Tutamsahilishia yawe mazito!} (Al-Lail: 5-10).

Mnao ndani ya Zaka ujuu wa roho na tabia kwa ukarimu na utoaji sana, na kwayo unakamilika uadilifu, uwepesi wa maisha unaenea, na mafukara wanapata maisha ya furaha,

Nayo ni pambo la wakwasi na wachamgu, na ni wasia wa Manabii, kuitekeleza ni dalili ya ukweli wa Imani na sifa ya Ihsani, ni miongoni mwa sababu za kupata radhi, ni alama ya kufaulu, na ni dalili kuwa na Yakini,

Nayo ni miongoni mwa haki za mafukara, mkwasi anaitoa kuwapa bila ya kusimbulia wala kudhalilisha, mtu anakamilisha kwayo Dini yake, na anahifadhi kwayo mali yake.

Na kwayo mja huikurubia Pepo, na huwekwa mbali na Moto,

Alikuja mtu wa kijijini [A'raabi] kwa Nabii swala na salamu za Allah zimshukie, akasema:

«Nihadithie jambo lenye kunikurubisha na Pepo na kuniepusha na Moto, [mpokezi] asema: [Nabii] swala na salamu za Allah zimshukie akanyamaza, kisha akawaangalia Masahaba wake, kisha akasema kuwaambia: **Hakika huyu ameafikiwa** - au alisema: **Hakika huyu ameongozwa**. [Nabii akamgeukia A'raabi] akasema**: Umesemaje?** [mpokezi] asema: Akarudia

[swali], basi Nabii swala na salamu za Allah zimshukie akasema: **Muabudu Allah wala usimshirikishe na chochote, usimamishe Swala, utoe Zaka, na uunge kikazi**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Atakaye itoa hali nafsi inahisi vizuri, Allah atamuonjesha ladha ya Imani na tamu yake, ibnul Qayyim Allah amrehemu amesema: "Na mtoa sadaka kila anapotoa Sadaka, ndio moyo wake unapata ukunjufu, kifua chake kinapata upanufu, furaha yake inazidi nguvu na inakuwa, na lau Sadaka haingekuwa na faida ila hii tu, basi ingekua haki kwa mja akithirishe kuitoa na kuiharakisha».

Na kwa ajili ya umuhimu wa Zaka Allah alitawali mwenyewe kutaja masarifu yake, akasema:

﴿إِنَّمَا ٱلصَّدَقَٰتُ لِلۡفُقَرَآءِ وَٱلۡمَسَٰكِينِ وَٱلۡعَٰمِلِينَ عَلَيۡهَا وَٱلۡمُؤَلَّفَةِ قُلُوبُهُمۡ وَفِي ٱلرِّقَابِ وَٱلۡغَٰرِمِينَ وَفِي سَبِيلِ ٱللَّهِ وَٱبۡنِ ٱلسَّبِيلِۖ فَرِيضَةٗ مِّنَ ٱللَّهِۗ وَٱللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٞ﴾

{Wa kupewa sadaka ni mafakiri, na masikini, na wanao zitumikia, na wa kutiwa nguvu nyoyo zao, na katika kukomboa watumwa, na wenye madeni, na katika Njia ya Allah, na wasafiri. Huu ni wajibu uliofaridhiwa na Allah. Na Allah ni Mwenye kujua Mwenye hikima}, (At-Taubah: 60).

basi haijuzu kuwapa ambao hawakutajwa [katika aya hii].

Na yamekuja makemeo kwa yule aliyeifanyia ubahili [Zaka]; [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿وَٱلَّذِينَ يَكۡنِزُونَ ٱلذَّهَبَ وَٱلۡفِضَّةَ وَلَا يُنفِقُونَهَا فِي سَبِيلِ ٱللَّهِ فَبَشِّرۡهُم بِعَذَابٍ أَلِيمٖ﴾

{Na wanao kusanya dhahabu na fedha, wala hawazitumii katika Njia ya Allah, wabashirie khabari ya adhabu iliyo chungu}, (At-Taubah:34).

Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**Yule ambaye Allah amempa mali, kisha asitoe Zaka yake; mali yake yatamathilishwa nyoka mwenye sumu kali** [Shuja'an aqra'a], **mwenye vitone viwili vyeusi juu ya macho yake, atakayemtatia siku ya Kiyama** [shingoni], **kisha amuume mdomo mwake**, **kisha awe akimuambia: Mimi ni mali yako, mimi ni kanzi yako**, kisha Nabii swala na salamu za Allah zimshukie akasoma: **{Wala wasidhani wale ambao wanafanya ubahili katika aliyowapa Allah katika fadhila zake kuwa ni kheri yao. Bali hiyo ni shari kwao. Watafungwa kongwa za yale waliyoyafanyia ubahili Siku ya Kiyama}**», imepokewa na Bukhari.

**Na baada ya hayo [yaliotangulia], enyi Waisilamu:**

Ibada ya Zaka ni neema Allah kamhusu nayo mkwasi, basi aifurahiye, na aitoe [Zaka] hali nafsi yake ikisikia vizuri, kwani inamridhisha 'Ar-Rahmaan' [Mwingi wa Rehema], inayakuza mali, na inayahifadhi kutokana na maafa na uharibifu.

***'Audhu billaahi mina sh-shaitwaani rrajiim'***

﴿ٱلشَّيۡطَٰنُ يَعِدُكُمُ ٱلۡفَقۡرَ وَيَأۡمُرُكُم بِٱلۡفَحۡشَآءِۖ وَٱللَّهُ يَعِدُكُم مَّغۡفِرَةٗ مِّنۡهُ وَفَضۡلٗاۗ وَٱللَّهُ وَٰسِعٌ عَلِيمٞ﴾

{Shet'ani anakutieni khofu ya ufakiri na anakuamrisheni mambo machafu. Na Allah anakuahidini msamaha na fadhila zitokazo kwake. Na Allah ni Mwenye wasaa, Mwenye kujua}. (Al-Baqarah: 268).

Allah anibarikie mimi na nyinyi katika Qur-ani adhimu...

## HOTUBA YA PILI

Sifa njema zote astahili Allah kwa wema Wake [kwetu], na shukrani zote astahili Yeye kwa kutuafikia na kutuneemesha, na nashuhudia ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake hana mshirika; ili kuadhimisha shani yake, na nashuhudia ya kwamba Nabii wetu Muhammad ni mja Wake [Allah] na Mtume wake, swala na salamu nyingi za Allah zimshukie yeye, watu wa nyumba yake na Masahaba wake.

**Ama baada ya himdi hii, enyi Waislamu:**

Kutokana na Zaka yanalipwa madeni ya mafakiri masikini, yanatekelezwa mahitaji yao, anasaidiwa msafiri aliyekatikiwa na safari yake, na nyoyo zinaingia uzoefu wa Dini. Ni yenye kuwekwa akiba mbele ya Allah, ni mkopo wenye kuzidishwa maradufu kwa mkwasi; [Allah] mwenye ushindi na ukubwa amesema:

﴿وَمَآ أَنفَقۡتُم مِّن شَيۡءٖ فَهُوَ يُخۡلِفُهُۥۖ وَهُوَ خَيۡرُ ٱلرَّٰزِقِينَ﴾

{Na chochote mnachokitoa basi Yeye huwapa badala yake, naye ni mbora wa wanao ruzuku}.(Saba: 39).

Basi kuwa mnyenyekevu kwa maskini, na mpe mali, mkurubie, na mhurumie, wala usimdharau fukara, kwani hakika wengi wa watu wa Peponi ni mafakiri, na toa kwa mkono mkarimu na nafsi karimu, utabarikiwa katika mali na wana. Sadaka ni dawa ya maradhi na alama zake, basi watafuteni madhaifu na wenye haja, na toeni mtaruzukiwa, na warehemuni nanyi mtarehemewa, kwani hajawahi lia shida fukara ila ni kwa sababu ya upungufu wa mkwasi [katika kutoa haki ya Zaka],

Kisha jueni kuwa Allah amewaamrisha kumswalia na kumsalimia Nabii wake...

## UBORA WA SADAKA[1]

Sifa za ukamilifu zote ni za Allah, tunamhimidi, tunamuomba msaada, tunamuomba msamaha, na tunajilinda na Allah kutokana na shari za nafsi zetu, na kutokana na amali zetu mbovu, yule ataongozwa na Allah, basi hakuna wa kumpoteza, na atakaye mpoteza hakuna wa kumuongoza, nashuhudia ya kwamba hapana apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake, hana mshirika, na nashuhudia kuwa Nabii wetu Muhammad ni mja wake na Mtume wake, swala na salamu za Allah nyingi zimshukie yeye, watu wake, na masahaba wake.

Basi enyi waja wa Allah mcheni Allah haki ya kumcha, na mchungeni [chungeni amri zake na makatazo yake] katika siri na minong'ono.

**Enyi waisilamu:**

Mali huondoka yakirudi katika mikono ya waja, wala hayabaki katika hali moja, na yule ambaye hajaondokewa na mali basi ataondoka yeye ayaache kwa kufa, [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿كَمۡ تَرَكُواْ مِن جَنَّـٰتٖ وَعُيُونٖ * وَزُرُوعٖ وَمَقَامٖ كَرِيمٖ﴾

{Mabustani mangapi, na chemchem ngapi waliziacha! * Na mimea na vyeo vitukufu!} (Ad-Dukhan:25).

Nayo [mali] ni fitna ya umma huu. [Mtume] swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**Hakika kila umma uko na fitna, na fitna ya umma wangu ni mali**», imepokewa na Tirmidhi.

Mali ni sahibu asiyeaminika, mara hugeuka kuwa adui, na akamnyima mmiliki wake thawabu, na hakika si mengine mwenye mali huhimidiwa anapoikurubia kheri na kumkurubia fukara kwa kumpa sadaka; Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«[Mali] **ni sahibu mzuri wa Muisilamu yule anayeyatoa kuwapa maskini, yatima, na msafiri** [aliyekatikiwa na safari]», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Nayo ni kama jiwe lilio katika mkono; halinufaishi ila linapofarikiana na kitanga cha mkono, na mwenye kuyazuilia atajuta pindi ajali yake itakapokurubia, [Allah] aliye mkubwa na aliye juu amesema:

[1] Imetolewa katika hotuba zilizotolewa ndani ya Al-Msjid An-Nabawi.

﴿وَأَنفِقُواْ مِن مَّا رَزَقۡنَٰكُم مِّن قَبۡلِ أَن يَأۡتِيَ أَحَدَكُمُ ٱلۡمَوۡتُ فَيَقُولَ رَبِّ لَوۡلَآ أَخَّرۡتَنِيٓ إِلَىٰٓ أَجَلٖ قَرِيبٖ فَأَصَّدَّقَ وَأَكُن مِّنَ ٱلصَّٰلِحِينَ * وَلَن يُؤَخِّرَ ٱللَّهُ نَفۡسًا إِذَا جَآءَ أَجَلُهَاۚ وَٱللَّهُ خَبِيرُۢ بِمَا تَعۡمَلُونَ﴾

{Na toeni katika tulichokupeni kabla hayajamfikia mmoja wenu mauti, tena hapo akasema: Mola wangu Mlezi! Huniakhirishi muda kidogo nipate kutoa sadaka, na niwe katika watu wema? * Wala Allah hataiakhirisha nafsi yoyote inapofika ajali yake; na Allah anazo khabari za mnayoyatenda}. (Al-Munafiqun: 10-11).

Na Allah amewafungulia waja wake mlango wa Sadaka; ili awaridhie, nayo inazima Ghadhabu ya Ar-Rahmaan, na ni dalili ya imani, na ni miongoni mwa amali bora zaidi; Nabii swala na salamu za Allah zimshukie aliulizwa:

«Ni Uisilamu gani ndio bora zaidi? **Akasema: ni ulishe chakula, na utoe salamu kwa umjuaye na usiyemjua**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Na kwayo ujira unakuwa maradufu, na makosa na dhambi zinafutwa, [Mtume] swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**Je nisikujuze milango ya kheri? Saumu ni kinga, Sadaka inafuta athari za dhambi kama vile maji yanavyozima moto, na pia Swala ya mtu ndani ya usiku** - yaani: inafuta athari za dhambi kama vile maji yanavyozima moto-», imepokewa na Tirmidhi.

Nayo [Zaka] inakuza mali na kuyazidisha mara dufu; [Allah] aliye mkuu na aliye juu amesema:

﴿مَّن ذَا ٱلَّذِي يُقۡرِضُ ٱللَّهَ قَرۡضًا حَسَنٗا فَيُضَٰعِفَهُۥ لَهُۥٓ أَضۡعَافٗا كَثِيرَةٗ﴾

{Ni nani atakaye mkopesha Mwenyezi Mungu mkopo mwema ili amzidishie mzidisho mwingi}, (Al-Baqarah: 245). na [Mtume] swala na salamu za Allah zimshukie:

«**Allah aliye mwingi wa baraka na aliyetukuka amesema: Ewe mwanadamu! Toa** [Sadaka kuwapa maskini] **Nami nitoe kukupa**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Na athari zake [Zaka] zinadhihiri katika nafsi, mali na wana, na inazuia balaa, inaleta uwepesi wa maisha, ibnu Al-Qayyim Allah amrehemu amesema: "Na Sadaka inayo athari ya ajabu katika kukinga balaa, na jambo hili linajulikana kwa watu - wenye elimu wao na wasio na elimu -, sababu wameijaribu, wala haijawahi patikana kuvutwa neema za Allah, wala

kukingwa adhabu zake kama vile yanavyopatikana hayo kupitia kumtii Yeye, kujikurubisha kwake na kuwatenda wema waja wake".

Na Sadaka iliyo na ujira mkubwa zaidi:

«**ni utoe Sadaka hali ya kuwa umzima wa afya, unahisi uchoyo, unaogopa ufakiri, na unatarajia ukwasi, wala usicheleweshe Sadaka hadi roho ifike katika gorombo, ndio useme: Fulani apewe mali kadhaa, na fulani apewe mali kadhaa** [kama Sadaka]**, ilihali muda huo mali** [siyako tena] **yashakuwa ni ya fulani** [kati ya warithi wako]», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Na «**Sadaka bora ni iliyotolewa baada ya kubakisha kitu [ili asiwe mhitaji baada ya kutoa Sadaka], na mkono wa juu ni bora kuliko mkono wa chini**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Na kuwafanyia wepesi wenye uzito ni Sadaka, na aliyekopa mali akikusudia kuyalipa basi Allah humlipia [humuwezesha kulipa au humtoa wa kulipia, n.k],

Na «**hakika miongoni mwa wabora wenu ni aliye mzuri zaidi katika kulipa**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea,

Na ni miongoni mwa Sadaka: ni kunywisha maji na kulisha chakula,

Na «**atakaye mfuturisha aliyefunga atakuwa na mfano wa ujira wake, ila hilo halipunguzi chochote katika ujira wa aliyefunga**», imepokewa na Tirmidhi,

Na ibnu Umar Allah amridhie alikuwa akifunga, wala hafuturu ila na maskini.

Mwenye kutoa Sadaka ni mwenye kupata amani duniani na akhera; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿ٱلَّذِينَ يُنفِقُونَ أَمْوَٰلَهُم بِٱلَّيْلِ وَٱلنَّهَارِ سِرًّا وَعَلَانِيَةً فَلَهُمْ أَجْرُهُمْ عِندَ رَبِّهِمْ
وَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ﴾

{Wale wanao toa mali zao usiku na mchana, kwa siri na dhahiri, wana ujira wao kwa Mola wao Mlezi; wala haitakuwa khofu juu yao, wala hawatahuzunika}, (Al-Baqarah: 274).

Na Sadaka yake inakuwa kubwa mbele ya Allah; basi [Sadaka ya] tende Allah anaipokea na kuilea hadi iwe mfano wa jabali.

Na kuificha Sadaka ni bora kuliko kuidhihirisha; kwani inakuwa mbali zaidi na riya, isipokuwa kukifungamana na jambo la kuidhihirisha maslahi makubwa; kama vile wengine [watakao muona] kumuiga kwa kutoa, [Allah]

aliyetakasika amesema:

﴿إِن تُبْدُواْ ٱلصَّدَقَٰتِ فَنِعِمَّا هِيَۖ وَإِن تُخْفُوهَا وَتُؤْتُوهَا ٱلْفُقَرَآءَ فَهُوَ خَيْرٌ لَّكُمْۚ
وَيُكَفِّرُ عَنكُم مِّن سَيِّـَٔاتِكُمْۗ وَٱللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرٌ﴾

{Mkizidhihirisha sadaka ni vizuri; na mkizificha mkawapa mafakiri kwa siri basi hivyo ni kheri kwenu, na yatakuondoleeni baadhi ya maovu yenu. Na Allah anazo khabari za mnayoyatenda} (Al-Baqarah: 271).

Na ni miongoni mwa watu saba watakao kuwa katika kivuli cha Allah:

«**mtu aliyetoa Sadaka; akaificha hadi mkono wa kushoto usijue ulichokitoa mkono wake wa kiume**», imepokewa na Bukhari,

Zainul A’bidiin Allah amrehemu alipokufa, watu wa Madina waliikosa Sadaka ya siri, na pindi walipomuosha walipata athari ya weusi katika mgongo wake, kwa ajili ya kubeba unga [wa chakula] usiku kuwapelekea mafakiri wa Madina.

Na Allah ni Mkarimu anapenda ukarimu, na Nabii wetu swala na salamu za Allah zimshukie «ni mtoaji zaidi kati ya watu, na alikuwa akitoa zaidi ndani ya Ramadhani, pindi anapokutana na Jibrili, akawa akisoma naye Qur-ani, basi alikuwa mtoaji zaidi kuliko upepo wenye kuenda kasi»,

Wala hakuombwa kitu ila alikitoa, Na «Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alikuwa mtoaji kheri zaidi kati ya watu», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Na hakuwa akiona kitu alichokitoa ni kingi, wala hakuwa anamrudisha mwenye kuomba, na ilikua kutoa Sadaka ndio kitu kipendezacho zaidi kwake, na ilikuwa furaha yake kwa ajili ya alichokitoa ni kubwa zaidi kuliko furaha ya aliyechukua kwa alichochukua.

Basi watafuteni maskini hata lau ni kwa kitu kichache; kwani kichache kwa Allah ni kingi, na uchache wa utoaji unasitiri kutokana na Moto; Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**Ewe Aisha! Jisitiri kutokana na Moto hata lau ni kwa** [kutoa Sadaka] **nusu ya tende, kwani inamjaza mwenye njaa vile inavyomjaza aliyeshiba**», imepokewa na Ahmad.

Yahya ibn Muadh Allah amrehemu amesema: "Sijui mbegu moja inayotoshana kiwizani na majabali ya duniani isipokuwa mbegu ya Sadaka»,

Kutoa ni kunyayuka, na ukarimu ni wema, na kila nafsi inapokuwa na hali ya juu basi utoaji unakuwa mkubwa zaidi, na mtu atakuwa chini ya

kivuli cha Sadaka yake siku ya Kiyama.

Na Allah alimjalia mwenye ujamaa [ukaribu wa kizazi] haki [yakutekelezewa] iliyo juu ya shingo [za waja], haki hiyo inatekelezwa kwa kutoa [Sadaka];

﴿وَءَاتِ ذَا ٱلۡقُرۡبَىٰ حَقَّهُۥ﴾

{Na mpe aliye jamaa yako haki yake}, (Al-Isra`:26).

Basi si jambo la fadhila [ya ziada], hakika si mengine ni haki ambayo Allah ndiye aliyeifaradhisha,

Na «**hakika Sadaka kwa maskini ni Sadaka tu, na kwa aliye na kizazi ni mawili: Sadaka na uungaji kizazi**», imepokewa na Nasai.

Na kuwapa Sadaka [wenye kizazi] thawabu zake zimekamilika, na ujira wake ni wenye kuzidishwa; Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema - pindi alipoulizwa kuhusu Sadaka ya Zainab kwa mumewe Abdallah ibn Mas-uud na mayatima wake; alisema:

«**Ndio, ana ujira mara mbili: ujira wa [kuunga] kizazi, na ujira wa Sadaka**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Na kuzuia Sadaka kwa ajili ya kuogopa [mali] kuisha [hilo] ni uharibifu wa mali, [Mtume] swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**Hakuna siku waja wataamka ila hushuka Malaika wawili, basi mmoja wao aseme: Ewe Allah, mpe mwenye kutoa badala, na Yule mwengine anasema: Ewe Allah, mpe mwenye kuzuia uharibifu**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea,

Na mtoaji ameahidiwa ushindi na msamaha.

Na mja hasalimiki na mitihani ila kwa subira na kushikamana na Allah, na aliyepungukiwa na mali mkononi mwake basi ashikamane na uchamngu; kwani kwayo milango ya riziki ya aliye na uzito husahilika, [Allah] mwenye ushindi na ukuu amesema:

﴿وَمَن يَتَّقِ ٱللَّهَ يَجۡعَل لَّهُۥ مَخۡرَجٗا * وَيَرۡزُقۡهُ مِنۡ حَيۡثُ لَا يَحۡتَسِبُ﴾

{Na anayemcha Allah humtengezea njia ya kutokea * Na humruzuku kwa jiha asiyotazamia} ,(At-Twalaq: 2-3).

Na kwa kudumu na istighfaari [kumuomba Allah msamaha] mali yanakithiri; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿فَقُلۡتُ ٱسۡتَغۡفِرُواْ رَبَّكُمۡ إِنَّهُۥ كَانَ غَفَّارٗا * يُرۡسِلِ ٱلسَّمَآءَ عَلَيۡكُم مِّدۡرَارٗا *
وَيُمۡدِدۡكُم بِأَمۡوَٰلٖ وَبَنِينَ وَيَجۡعَل لَّكُمۡ جَنَّٰتٖ وَيَجۡعَل لَّكُمۡ أَنۡهَٰرٗا﴾

{Nikasema: Ombeni msamaha kwa Mola wenu Mlezi; hakika Yeye ni Mwingi wa kusamehe * Atakuleteeni mvua inyeshe mfululizo * Na atakupeni mali na wana, na atakupeni mabustani na atakufanyieni mito}. (Nuh: 10-11).

***'Audhu billaahi mina sh-shaitwaani rrajiim'***

﴿وَمَآ أَنفَقْتُم مِّن نَّفَقَةٍ أَوْ نَذَرْتُم مِّن نَّذْرٍ فَإِنَّ ٱللَّهَ يَعْلَمُهُۥ﴾

{Na chochote mnachotoa au nadhiri mnazoweka basi hakika Allah anajua} (Al-Baqarah: 270).

Allah anibarikie mimi na nyinyi katika Qur'ani tukufu...

## Hotuba Ya Pili

Sifa njema zote astahili Allah kwa wema Wake [kwetu], na shukrani zote astahili Yeye kwa kutuafikia na kutuneemesha, na nashuhudia ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake hana mshirika; ili kuadhimisha shani yake, na nashuhudia ya kwamba Nabii wetu Muhammad ni mja Wake [Allah] na Mtume wake, swala na salamu nyingi za Allah zimshukie yeye, watu wa nyumba yake na Masahaba wake.

**Enyi Waislamu:**

Toeni katika pato lenu zuri, na mtarajie malipo yenu kwa Allah, kwani kwa Sadaka ndio hupatikana baraka ya mali na utwahara wa nafsi,

Na kila mtu siku ya Kiyama atakuwa chini ya kivuli cha Sadaka yake, na ni miongoni mwa atakao watia Allah katika kivuli cha Arshi yake:

«**mtu aliyetoa Sadaka; akaificha hadi mkono wa kushoto usijue ulichokitoa mkono wake wa kiume**», imepokewa na Bukhari,

Na Muumini hachukulii chochote [kati ya mema] kuwa ni kichache, kwani huenda dirhamu moja ikashinda dirhamu elfu moja, na atakaye wafanyia ukarimu waja wa Allah, basi Allah naye atamfanyia ukarimu kwa mambo bora na vipawa, na malipo ni kutokana na jinsi ya matendo.

Kisha jueni kuwa Allah amewaamrisha kumswalia na kumsalimia Nabii wake…

# UBORA WA KUTOA [SADAKA][1]

Sifa njema zote anastahiki Allah mwenye kumpa ushindi anaye mtii na kumcha Yeye, na mwenye kumdhalilisha anayepoteza amri yake na kumuasi, namuhimidi himdi nyingi, zilizo nzuri na zenye baraka, kama anavostahiki na anavoridhia Mola wetu Mlezi. Nashuhudia ya kwamba hapana apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake, hana mshirika naye, wala hatuna Mola ila Yeye, wala hatumuabudu ila Yeye, na nashuhudia ya kwamba Nabii wetu Muhammad ni mja wake na Mtume wake, mkweli zaidi wa wanaolingania kwa Allah, na anayewanasihi zaidi waja wa Allah, ewe Allah mswalie na umsalimu yeye, watu wake, masahaba wake, na kila aliyefuata njia yake na uongofu wake.

**Ama baada ya himdi hii:**

Enyi waja wa Allah, mcheni Allah haki ya kumcha, mtakasieni siri yenu na dhahiri yenu, kimbilieni radhi za Mola wenu Mlezi na vuneni mazuri ya mwezi wenu [huu].

**Enyi Waisilamu:**

Ni miongoni mwa malengo ya Uisilamu: Kujenga jamii yenye kuhurumiana, yenye kusikitikiana, iliotandwa na mapenzi na undugu, iliotawaliwa na kupenda kheri na kutoa, na duara la ukarimu linakunjuka kwa ajili ya kuwa nyoyo zenye Imani zinafurahia kutoa katika [milango] kheri,

Na hakika Uisilamu mtakatifu umependekeza hilo kwa njia yenye kukunjua kifua cha mtu mkarimu, na kutibu ubahili wa mtu mpumbavu, [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿مَّن ذَا ٱلَّذِى يُقۡرِضُ ٱللَّهَ قَرۡضًا حَسَنًا فَيُضَٰعِفَهُۥ لَهُۥٓ أَضۡعَافًا كَثِيرَةً﴾

{Ni nani atakayemkopesha Allah mkopo mwema ili amzidishie mzidisho mwingi}, (Al-Baqarah: 245).

Na «Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alikuwa mtoaji zaidi kati ya watu, na alikuwa akitoa zaidi ndani ya Ramadhani»,

Akitoa hukithirisha, na akizawadia huzawadia kama mtu asiyeogopa umaskini, hakuombwa kitu ila hukitoa, hajamrudisha mwenye kuomba ila

---

[1] Imetolewa katika hotuba zilizotolewa ndani ya Al-Masjid An-Nabawi.

asipokuwa na kitu, [Mtume] swala na salamu za Allah zimshukie aliwapendekezea Masahaba Sadaka, wakatoa mali yao bora; Umar ibnul Khattwaab Allah amridhie alitoa nusu ya mali yake, na Abu Bakar Allah amridhie alitoa mali yake yote. Na [Mtume] swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**Atakaye liandaa jeshi la 'Al-Usrah' atapata Pepo; basi akaliandaa Uthmaan Allah amridhie**», imepokewa na Bukhari,

Na iliposhuka kauli ya Allah:

﴿لَن تَنَالُواْ ٱلۡبِرَّ حَتَّىٰ تُنفِقُواْ مِمَّا تُحِبُّونَ﴾

{Kabisa hamtafikia wema [wa kuingiza Peponi] mpaka mtoe katika vile mnavyovipenda}, (Al- Imran: 92).

Basi akasimama Abu Twalha Allah amridhie akamuedea Mtume swala na salamu za Allah zimshukie akasema: «Ewe Mtume wa Allah! Hakika mali yangu yanayopendeza zaidi kwangu ni 'bayruhaa' [bustani liliojulikana kwa jina hilo], nalo nimelitoa Sadaka kwa ajili ya Allah», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea,

Sadaka chache iliyo na ikhlasi inasalimisha na Moto; Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**Jichukulieni kinga na Moto hata kama ni kwa** [Sadaka ya] **nusu ya tende**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Mali hayaishi kwa utoaji na Sadaka, Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**Hakuna siku waja wataamka ila hushuka Malaika wawili, basi mmoja wao aseme: Ewe Allah, mpe mwenye kutoa badala, na Yule mwengine anasema: Ewe Allah, mpe mwenye kuzuia uharibifu**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea,

Na kuwa na yakini ya ukwasi wa mkarimu, Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**Allah aliyetukuka amesema: Ewe mwanadamu, toa** [Sadaka kuwapa maskini] **Nami nitoe kukupa**», Wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea,

Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema tena:

«**Sadaka haijawahi kupunguza mali yoyote**», imepokewa na Muslim.

Na mali ni amana iliyo katika mkono wako, hauna katika mali ila yale ulioyala ukayamaliza, au uliovaa ukayachakalisha, au uliotoa Sadaka

ukayatanguliza [kwa Allah]; basi kuwa mnyenyekevu kwa maskini, na mpe mali, mkurubie, na mhurumie, wala usimdharau fukara, kwani hakika wengi wa watu wa Peponi ni mafakiri.

Na atakaye wakirimu waja wa Allah, Allah atamkirimu, na atakayefunguliwa mlango wa kheri basi aupatilize, kwani hajui lini atafungiwa. Ukiweza yeyote asikushide katika kujikurubisha kwa Allah basi fanya,

Alipokufa Zainul Abidiin Allah amrehemu watu wa Madina waliikosa Sadaka ya siri, na pindi walipomuosha walipata athari ya weusi katika mgongo wake, kwa ajili ya kubeba unga [wa chakula] usiku kuwapelekea mafakiri wa Madina.

Mwenye kutoa mambo yake ya kimaisha yanakuwa mepesi, [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿فَأَمَّا مَنْ أَعْطَىٰ وَٱتَّقَىٰ * وَصَدَّقَ بِٱلْحُسْنَىٰ * فَسَنُيَسِّرُهُۥ لِلْيُسْرَىٰ * وَأَمَّا مَنۢ بَخِلَ وَٱسْتَغْنَىٰ * وَكَذَّبَ بِٱلْحُسْنَىٰ * فَسَنُيَسِّرُهُۥ لِلْعُسْرَىٰ﴾

{Ama mwenye kutoa na akamchamngu * Na akalisadikisha lilio jema [Neno la Shahada] * Tutamsahilishia yawe mepesi * Na ama mwenye kufanya ubahili, na asiwe na haja ya wenzake * Na akakanusha lilio jema * Tutamsahilishia yawe mazito!} (Al-Lail: 5-10).

Pia [mwenye kutoa] ameahidiwa msamaha na ukwasi; [Allah] mwenye ushindi na ukuu amesema:

﴿ٱلشَّيْطَٰنُ يَعِدُكُمُ ٱلْفَقْرَ وَيَأْمُرُكُم بِٱلْفَحْشَآءِ ۖ وَٱللَّهُ يَعِدُكُم مَّغْفِرَةً مِّنْهُ وَفَضْلًا﴾

{Shetani anakutieni khofu ya ufakiri na anakuamrisheni mambo machafu. Na Allah anakuahidini msamaha na fadhila zitokazo kwake}; (Al-Baqarah: 268).

Bali jambo la kutoa [Sadaka] ni lenye kupewa badala; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿وَمَآ أَنفَقْتُم مِّن شَىْءٍ فَهُوَ يُخْلِفُهُۥ ۖ وَهُوَ خَيْرُ ٱلرَّٰزِقِينَ﴾

{Na chochote mnachokitoa basi Yeye huwapa badala yake, naye ni mbora wa wanao ruzuku}. (Saba`: 39).

Na kutoa kunaleta faraja ya majanga, pindi Wahyi ulipoteremka kwa Nabii swala na salamu za Allah zimshukie kwa mara ya kwanza, alisema kumuambia Khadijah Allah amridhie:

**«Hakika nimejiogopea nafsi yangu**, [Khadija] akasema: Hapana,

wallahi Allah hatakutweza kabisa, hakika wewe unaunga kizazi, unambeba asiyejiweza, unachuma yalioadimika na kuyawasilisha kwa watu, unakirimu mgeni, na unasaidia katika misiba ya haki», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Na [Sadaka] manufaa yake ya kunjuka kufikia mpaka kuleta faraja ya majanga ya siku ya kukusanywa [Kiyama], basi mtoa Sadaka awe chini ya kivuli cha Sadaka yake siku ya Kiyama, na atakayeficha Sadaka yake - hata ikiwa ndogo -, Allah atamkirimu na kivuli chengine kisichokuwa kile cha Sadaka yake, nacho ni kivuli chini ya 'Arshi'.

Na mkwasi mwenye kutoa huwashinda wengine katika ujira. Baadhi ya masahaba Allah awaridhie walisema kumuambia Mtume swala na salamu za Allah zimshukie: «Wenye mali wameondoka na ujira mwingi», imepokewa na Muslim.

Na wakwasi walioafikiwa ni wale wanao jenga akhera yao kwa ukarimu na vipawa pamoja uchamngu, na Nabii swala na salamu za Allah zimshukie aliulizwa:

«Ni Sadaka gani ilio bora zaidi? Akasema**: Ni utoe Sadaka hali ya kuwa umzima wa afya, unapupa, unatarajia ukwasi, na unaogopa ufakiri**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Na kuificha [Sadaka] ni bora kuliko kuidhihirisha, [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿وَإِن تُخۡفُوهَا وَتُؤۡتُوهَا ٱلۡفُقَرَآءَ فَهُوَ خَيۡرٞ لَّكُمۡ﴾

{Mkizidhihirisha sadaka ni vizuri; na mkizificha mkawapa mafakiri kwa siri basi hivyo ni kheri kwenu}, (Al-Baqarah: 271).

Na ni miongoni mwa watu saba watakao kuwa katika kivuli cha Allah:

«**mtu aliyetoa Sadaka; akaificha hadi mkono wa kushoto usijue ulichokitoa mkono wake wa kiume**», imepokewa na Bukhari,

Na atakayekuwa na dhana njema na Allah basi nafsi yake itakuwa karimu, na itatoa mali yake ikiwa na yakini ya kauli Allah:

﴿وَمَآ أَنفَقۡتُم مِّن شَيۡءٖ فَهُوَ يُخۡلِفُهُۥ﴾

{Na chochote mnachokitoa basi Yeye huwapa badala yake.} (Saba`: 39).

Suleiman Addaaraani Allah amrehemu: alisema"Atakaye mtegemea Allah katika riziki yake basi atazidi kuwa na tabia njema, na litamrithisha hilo busara, na nafsi yake itakuwa karimu katika kutoa, na wasiwasi wake ndani ya Swala utapungua",

Na utoaji ni wenye kuzivuta [nyonyo] katika jambo la kutarajia [mema] yalio kwa Allah, kuwa na yakini ya ahadi yake [Allah], na kutenda kheri kwa tamaa ya fadhila zake zilizokuja katika kauli yake [Allah]:

﴿وَمَا يَفْعَلُواْ مِنْ خَيْرٍ فَلَن يُكْفَرُوهُ﴾

{Na kheri yoyote wanayoifanya hawatanyimwa malipo yake}, (Al-Imran: 115).

Na Sadaka bora zaidi ni Sadaka kwa jamaa wa karibu; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿يَسْـَٔلُونَكَ مَاذَا يُنفِقُونَ قُلْ مَآ أَنفَقْتُم مِّنْ خَيْرٍ فَلِلْوَالِدَيْنِ وَٱلْأَقْرَبِينَ﴾

{Wanakuuliza watoe nini? Sema: wastahiki zaidi wa Kheri mnayoitoa ni wazazi na jamaa}, (Al-Baqarah: 215).

Na jamaa yako ni kipande kutokana na wewe, utakapo mfanyia wema basi hakika wajifanyia wema mwenyewe, na ukimfanyia ubahili basi hakika umeifanyia ubahili nafsi yako,

Na Allah alimjalia mwenye ujamaa [ukaribu wa kizazi] haki [yakutekelezewa] iliyo juu ya shingo [za waja], haki hiyo inatekelezwa kwa kutoa [Sadaka], basi usiwafanyie ubahili, wala usimkahiri yatima, wala usimkemee mwenye kuomba, na toa kwa nafsi iliyo na ukarimu; Allah atakubariki katika mali na wana.

Na shetani humtia wasiwasi mwenye kutoa Sadaka, humuamrisha kuzuia, na humpambia hadaa na vitimbi, [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿ٱلشَّيْطَٰنُ يَعِدُكُمُ ٱلْفَقْرَ وَيَأْمُرُكُم بِٱلْفَحْشَآءِ وَٱللَّهُ يَعِدُكُم مَّغْفِرَةً مِّنْهُ وَفَضْلًا وَٱللَّهُ وَٰسِعٌ عَلِيمٌ﴾

{Shetani anakutieni khofu ya ufakiri na anakuamrisheni mambo machafu. Na Allah anakuahidini msamaha na fadhila zitokazo kwake. Na Allah ni Mwenye wasaa, Mwenye kujua.} (Al-Baqarah: 268).

Na Allah aliwakejeli wanafiki kwa ubahili wao katika kutoa kheri, ibnu Al-Qayyim Allah amrehemu amesema: "wao ni wanadamu waovu zaidi, wachafu zaidi, na duni zaidi",

Walimuudhi Mtume swala na salamu za Allah zimshukie na masahaba wake udhia mkubwa, wakamkejeli Mtume swala na salamu za Allah zimshukie katika kigawanyo chake, wakawafanyia shere masahaba zake, wakawafanyia stihizai wenye kutoa Sadaka miongoni mwao, ibnu Kathiir Allah amrehemu amesema: "wala hakusalimka mtu yeyote kutokana na kejeli zao katika hali zote",

Na endapo watatoa mali yao, basi wanatoa kwa kuchukia, kujisifu na kusitasita, na watakapo toa, Sadaka zao hazikubaliwi mbele ya Allah, kwa sababu ya itikadi zao mbaya na uovu wao; [Allah] mwenye ushindi na ukuu amesema:

﴿قُلۡ أَنفِقُواْ طَوۡعًا أَوۡ كَرۡهٗا لَّن يُتَقَبَّلَ مِنكُمۡ﴾

{Sema: Toeni mkipenda msipende. Hakitopokelewa kitu kwenu}, (At-Taubah: 53).

Na mali zao na watoto wao ni adhabu kwao:

﴿فَلَا تُعۡجِبۡكَ أَمۡوَٰلُهُمۡ وَلَآ أَوۡلَٰدُهُمۡۚ

إِنَّمَا يُرِيدُ ٱللَّهُ لِيُعَذِّبَهُم بِهَا فِي ٱلۡحَيَوٰةِ ٱلدُّنۡيَا وَتَزۡهَقَ أَنفُسُهُمۡ وَهُمۡ كَٰفِرُونَ﴾

{Yasikufurahishe mali yao wala wana wao. Hakika Allah anataka kuwaadhibu kwayo hapa duniani, na zitoke roho zao na hali wao ni makafiri}, (At-Taubah:55).

Na mkwasi bahili ni fukara aliyepambwa [na ukwasi], naye ni mtumishi, anawakusanyia wengine mali, hajanufaika nayo kwa nafsi yake, wala hakunyayuka daraja kwa kuwapa mafakiri, na huenda mwenye mali akaingiwa na ubahili katika kutoa:

﴿وَمَن يَبۡخَلۡ فَإِنَّمَا يَبۡخَلُ عَن نَّفۡسِهِۦ﴾

{Na anayefanya ubakhili basi anajifanyia ubakhili mwenyewe}, (Muhamad: 38).

Na Pupa na ubahili hauyahifadhi mali, wala kutoa hakuyapunguzi, Al-Hasan Al-Basri Allah amrehemu amesema: "Dirhamu na Dinari ni marafiki waovu; hawakunufaishi hadi watakapo kuepuka".

***'Audhu billahi mina sh-shaytwani rrwajiim'***

﴿وَأَنفِقُواْ مِن مَّا رَزَقۡنَٰكُم مِّن قَبۡلِ أَن يَأۡتِيَ أَحَدَكُمُ ٱلۡمَوۡتُ

فَيَقُولَ رَبِّ لَوۡلَآ أَخَّرۡتَنِيٓ إِلَىٰٓ أَجَلٖ قَرِيبٖ فَأَصَّدَّقَ وَأَكُن مِّنَ ٱلصَّٰلِحِينَ﴾

{Na toeni katika tulichokupeni kabla hayajamfikia mmoja wenu mauti, tena hapo akasema: Mola wangu Mlezi! Huniakhirishi muda kidogo nipate kutoa sadaka, na niwe katika watu wema?} (Al-Munafiqun:10).

Allah anibarikie mimi na nyinyi katika Qur-ani tukufu…

## HOTUBA YA PILI

Sifa njema zote anastahili Allah kwa wema Wake [kwetu], na shukrani zote anastahili Yeye kwa kutuafikia na kutuneemesha, na nashuhudia ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake hana mshirika; ili kuadhimisha shani yake, na nashuhudia ya kwamba Nabii wetu Muhammad ni mja Wake [Allah] na Mtume wake, swala na salamu nyingi za Allah zimshukie yeye, watu wa nyumba yake na Masahaba wake.

**Enyi Waisilamu:**

Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alikuwa mkarimu wa watu, na mtoaji zaidi, akitoa hukithirisha, na akizawadia huzawadia kama mtu asiyeogopa umaskini, basi muigeni Nabii wenu, na julieni hali nyumba za maskini, mafakiri,wajane na mayatima, kwani mnao katika hilo kuondosha majanga yao, kushibisha njaa zao, kumfurahisha mtoto, na kuitosheleza familia.

Na kutoa kuwapa waja wa Allah mafakiri na kuwafurahisha viumbe wake madhaifu ni katika kumshukuru Allah, na pupa na ubahili hazidumishi mali, wala kutoa hakuyamalizi.

Wala usiwe kama yule bahili muovu; anaitoa nafsi yake duniani kwa [mbio za] kuyakusanya [mali], na akhera atahesabiwa kwa kuzuia, duniani hana amani kutokana na hamu yake, wala akhera hajasalimika na dhambi zake, maisha yake duniani ni maisha ya mafakiri, na hesabu yake akhera ni hesabu ya matajiri.

Kisha jueni kuwa Allah amewaamrisha kumswalia na kumsalimia Nabii wake...

# Saumu Ya Ramadhani

# KUJIANDAA KWA RAMADHANI[1]

Sifa za ukamilifu zote ni za Allah, tunamhimidi, tunamuomba msaada, tunamuomba msamaha, na tunajilinda na Allah kutokana na shari za nafsi zetu, na kutokana na amali zetu mbovu, yule ataongozwa na Allah, basi hakuna wa kumpoteza, na atakaye mpoteza hakuna wa kumuongoza, nashuhudia ya kwamba hapana apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake, hana mshirika, na nashuhudia kuwa Nabii wetu Muhammad ni mja wake na Mtume wake, swala na salamu za Allah nyingi zimshukie yeye, watu wake, na masahaba wake.

**Ama baada ya himdi hii:**

Enyi waja wa Allah, mcheni Allah haki ya kumcha, na kamateni Uislamu katika kishiko madhubuti kabisa.

**Enyi Waislamu:**

Michana na usiku yanaenda mbio mbio, na mwaka unakunja miezi yake mfulilizo, na kawaida ya Allah katika dunia yake ni: kuja na kuondoka, naye Allah amewakirimu waja wake; akawaekea misimu katika zama, Ambayo ndani yake madhambi na makosa yanafutwa, na [watu] hujiandaa ndani yake kwa amali njema.

Na ndani ya mwaka mna mwezi ambao ndio mwezi bora zaidi, ndani yake ndio Allah alimpatia Mtume wake utume, na akamteremshia kitabu chake, Waislamu wanaungojea mwaka mzima hali ya kuwa na raha nao ndani ya vifua vyao, ndani yake wanatekeleza nguzo miongoni mwa nguzo za Uisilamu; inayofanywa kwa ikhlasi, ndani yake [nguzo hii] Muisilamu anahisi ladha hali akiwa na njaa. Mja anatekeleza ndani yake [nguzo hii] maana ya ikhlasi; ili aondoke nayo na kuitekeleza katika ibada zote zilizobaki, akiwa mbali kabisa na riya,

Thawabu za Saumu yake haina kikomo katika kuzidishwa, bali hilo linarudi kwa [Allah] Mkarimu, [Mtume] swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**Allah mwenye ushindi na ukuu amesema: Amali zote za**

---

[1] Imetolewa siku ijumaa, tarehe ishirini na moja ya mwezi wa Shaabani, mwaka elfu moja mia nne na thalathini na mbili wa hijri, ndani ya Msikiti wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie.

**mwanadamu ni zake, ila Saumu, kwani hakika hiyo ni yangu, nami Nitailipa**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Na Saumu inatengeza nyonyo, na inapelekea kuchuma mambo mema na kuwa mbali na ya ufisidifu. Kwayo madhambi yanafutwa; Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**Aliyefunga Ramadhani kwa hali ya kuamini na kutarajia; atasamehewa madhambi yake yaliotangulia**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Ni mwezi wa utiifu, ihsani, msamaha na radhi; Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**pindi Ramadhani inapoingia: milango ya mbingu inafunguliwa, na milango ya Jahanamu inafungwa, na mashetani wanafungwa minyororo**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Ndani yake [Saumu] mna kusubiria moto wa kiu na uchungu wa njaa, na kuilazimisha nafsi juu ya kuyakomesha matamanio. Malipo yao [wenye kufunga] ni mlango miongoni mwa milango ya Pepo, hataingia [Peponi] nao ila wao tu

Mnao ndani yake ukumbusho wa hali ya wenye njaa kati ya maskini na mafakiri, na ndani ya Saumu wanakuwa sawa waliokosa na wenye uwezo, wote wamemfunga kwa ajili ya Mola wao Mlezi, wanaomba msamaha wa madhambi yao, wanaacha kula kwa wakati mmoja, na wanafuturu kwa wakati mmoja, mchana wote wanakuwa sawa kwa njaa na kiu, ila itimie kwa wote kauli ya Allah:

﴿إِنَّ هَٰذِهِۦٓ أُمَّتُكُمۡ أُمَّةٗ وَٰحِدَةٗ وَأَنَا۠ رَبُّكُمۡ فَٱعۡبُدُونِ﴾

{Kwa hakika huu umma wenu ni umma mmoja, na Mimi ni Mola wenu Mlezi. Kwa hivyo niabuduni Mimi}.( Al-Anbiya`: 92).

Na Qur-ani tukufu ndio msingi wa Dini na alama ya Utume, imeteremka ndani ya mwezi bora zaidi:

﴿شَهۡرُ رَمَضَانَ ٱلَّذِيٓ أُنزِلَ فِيهِ ٱلۡقُرۡءَانُ﴾

{Mwezi wa Ramadhani ambao imeteremshwa humo Qur'ani} (Al-Baqarah:185).

Na kuteremka kwake ndani yake [Ramadhani] ni ishara kwa umma huu ukithirishe kusoma Qur'ani na kuizingati [ndani yake], na alikuwa Jibrili salamu zimshukie akishuka kutoka mbinguni, na akisoma [Qur'ani] pamoja na Nabii wetu swala na salamu za Allah zimshukie, na katika mwaka

aliokufa ndani yake alisoma naye Qur'ani mara mbili.

Na alikuwa imamu Malik Allah amrehemu inapoingia Ramadhani anaelekea kusoma Qur'ani, na huacha Hadithi na watu wake.

Na Sadaka ina manufaa makubwa dunia na akhera; kwani inakinga balaa, inasahilisha mambo, inavuta riziki, na inafuta athari za madhambi kama maji yanavyozima moto, nayo ni kivuli cha sahibu yake [aliyeotoa Sadaka] siku ya Kiyama.

Na mali hayapungui kwa Sadaka, bali ni faradhi yenye kudhaminiwa [badala] kwa [Allah] Mkwasi Mkarimu:

﴿وَمَآ أَنفَقۡتُم مِّن شَيۡءٖ فَهُوَ يُخۡلِفُهُۥۖ﴾

{Na chochote mnacho kitoa basi Yeye huwapa badala yake}, (Saba: 39).

anayazidishia baraka na usafi duniani, na anamlipa mtoaji akhera starehe ya kudumu,

Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**Hakuna siku waja wataamka ila hushuka Malaika wawili, basi mmoja wao aseme: Ewe Allah, mpe mwenye kutoa badala, na Yule mwengine anasema: Ewe Allah, mpe mwenye kuzuia uharibifu**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea,

Basi julieni hali za nyumba za mafakiri na maskini, wajane maskini na mayatima maskini; kwani mnao ndani ya hilo kutatua janga lako, kukukinga na balaa, kumshibisha aliye na njaa, furaha kwa mtoto, kuitosheleza familia, na kuwaondolea haja ya kuomba.

Na Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alikuwa mkarimu wa watu, na mtoaji zaidi: akitoa hukithirisha, na akizawadia huzawadia kama mtu asiyeogopa umaskini,

Na alikuwa akiipokea Ramadhani kwa utoaji mwingi, alikua mtoaji wa kheri kuliko upepo ulioaziliwa, na pupa na ubahili haudumishi mali, wala kutoa hakuyamalizi.

Na usiku wa Ramadhani ndio taji la usiku wa mwaka;

«**atakaye simama [usiku wa] Ramadhani [kwa ibada] hali ya kuamini na kutarajia; atasamehewa madhambi yake yaliotangulia**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea,

Na giza lake ni lenye thamani kwa ibada ndani yake; Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**Swala bora zaidi baada ya faradhi ni Swala ya usiku**», imepokewa

na Muslim, na

«**atakayeswali pamoja na imamu hadi [imamu] aondoke; ataandikiwa kisimamo cha usiku kamili**», imepokewa na Tirmidhi,

Na mnao ndani yake usiku mmoja unaozidishwa ujira wake, nao ndio mama wa usiku - 'Usiku wa cheo na utukufu - ni mbora kuliko miezi elfu moja, na ndani ya kila usiku [wa Ramadhani] unafunguliwa mlango wa kuitikiwa maombi mbinguni, na hazina za [Allah] mwenye kutoa zimejaa, basi omba vipawa vya [Allah] Mwenye kukirimu, na rehema za mwenye kurehemu, kwani Ramadhani ni mwezi wa vipawa na tunu, na mtu mlemavu zaidi aliyekosa kuomba.

Na masiku ni kurasa za umri, na aliye mwema ni yule aliyezidumisha na amali njema zaidi, na aliyetolewa na Allah kutoka udhalilifu wa maasi hadi katika utukufu wa utiifu; huyo [Allah] amemtajirisha bila mali, na amempumbaza bila mwendani wa kupumbaza, na aliyetambua Mola wake Mlezi basi atajishughulisha naye kuache matamanio ya nafsi yake.

Baadhi ya watu wamefanya usiku wao ulio na thamani kuwa rahisi, kwa kushughulika na upuzi na yasio na manufaa, pindi mwezi wa Saumu unapoisha, watu wanakuwa wamefaidika hali yeye amepata hasara,

Na wako baadhi ya watu ambao wanafunga wala hawaswali, na Saumu haikubaliwi ila kwa Tawhidi na Swala

Na mwanamke ameamrishwa kukithirisha kusoma Qur'ani, dhikri, istighfari na kukithirisha ibada za sunnah, na Swala ya Tarawehe nyumbani kwake ni bora kuliko msikitini, [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

«**na nyumba za** [wanawake] **ni bora zaidi kwao**», imepokewa na Abu Daaud.

Na ni juu yake kujisitiri na kuwa na haya, na kumchunga Mola wake Mlezi katika hali ya kughibu msimamizi wake au kuwepo kwake, na aliye mwema miongoni mwao ameahidiwa Radhi za Mola Mlezi wa viumbe wote, na kushikamana kwake na Dini yake, kujisitiri kwake, na kutukuza kwake na hijabu; [yote hayo] yananyanyua shani yake, na yanatia nguvu cheo chake, naye [mwanamke] ndio fakhari ya jamii, taji la heshima, na johari la maisha.

***'Audhu billaahi mina sh-shaitwaani rrajiim'***

﴿يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ كُتِبَ عَلَيْكُمُ ٱلصِّيَامُ كَمَا كُتِبَ عَلَى ٱلَّذِينَ مِن قَبْلِكُمْ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ﴾

{Enyi mlio amini! Mmeandikiwa Saumu, kama waliyo andikiwa walio kuwa kabla yenu ili mpate kuchamngu}. (Al-Baqarah: 183).

Allah anibarikie mimi na nyinyi katika Qur’ani tukufu...

## HOTUBA YA PILI

Sifa njema zote anastahili Allah kwa wema Wake [kwetu], na shukrani zote anastahili Yeye kwa kutuafikia na kutuneemesha, na nashuhudia ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake hana mshirika; ili kuadhimisha shani yake, na nashuhudia ya kwamba Nabii wetu Muhammad ni mja Wake [Allah] na Mtume wake, swala na salamu nyingi za Allah zimshukie yeye, watu wa nyumba yake na Masahaba wake.

**Enyi Waisilamu:**

Miongoni mwa mapokezi bora ya Ramadhani ni: kudumu kuomba msamaha, kukithirisha kumuhimidi Allah kwa kufikiwa na Ramadhani,

Na waliotangulia katika mambo ya kheri ndio wenye kutangulia katika daraja za juu Peponi,

Basi tekelezeni sababu za kurehemewa na Allah ndani ya mwezi wake mkarimu, shindaneni katika amali njema na mambo ya kheri, kithirisheni ndani yake aina za ihsani.

Jiwekeni mbali na kusengenya, kuchochea na makosa yote, wala usikose kheri kwa sababu ya kukesha nje ya utiifu, wala usingizi usikuzuilie na ibada, na ukiweza usitanguliwe na yeyote kufika kwa Allah basi fanya.

Kisha jueni kuwa Allah amewaamrisha kumswalia na kumsalimia Nabii wake...

# RAMADHANI IMEINGIA[1]

Sifa zote za ukamilifu ni za Allah, tunamhimidi, tunamuomba msaada, tunamuomba msamaha, na tunajilinda na Allah kutokana na shari za nafsi zetu, na kutokana na amali zetu mbovu, yule ataongozwa na Allah, basi hakuna wa kumpoteza, na atakaye mpoteza hakuna wa kumuongoza, nashuhudia yakwamba hapana apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake, hana mshirika, na nashuhudia kuwa Nabii wetu Muhammad ni mja wake na Mtume wake, swala na salamu za Allah nyingi zimshukie yeye, watu wake, na masahaba wake.

**Ama baada ya himdi hii:**

Enyi waja wa Allah, mcheni Allah haki ya kumcha, na kamateni Uislamu katika kishiko madhubuti kabisa.

**Enyi Waislamu:**

Michana na usiku yanaenda mbio mbio, na mwaka unakunja miezi yake mfulilizo, na katika hilo waja wanaelekea kwa Allah, na karibuni watakutana na amali zao. Na ni katika fadhila za Allah na ukarimu wake kuwa amewateulia waja wake kati ya zama misimu ya ibada, na akachagua masiku na usiku na masaa; ili hamu na bidii ziwe kubwa ndani yake, na uchangamfu uzidi, na washindane wenye kushindana.

Na kila mwezi wa Ramadhani unapodhihiri unatuletea tena vipawa vilivyobarikiwa, basi Waisilamu wanaupokea hali ya kuwa mna raha ndani ya nafsi zao, na vifua vyao vimejaa furaha, huenda kipindi cha kabuli ndani yake kikamdiriki mja, akafikia kwacho daraja za radhi na maisha mema.

Na umetuteremkia mwezi mtukufu zaidi na mtakatifu zaidi, ni msimu mkubwa, Allah ameihusu kwa utukufu na ukarimu, basi ndani yake akamtumiliza Mtume wake swala na salamu zimshukie, akateremsha kitabu chake, na akafaradhisha saumu, ni masaa yaliobarikiwa, na vipindi vyake vimeimarishwa na kheri, kheri ndani zinafuatana, na zinaenea baraka ndani yake.

Ni msimu wa ihsani na sadaka nyingi, na ni zama za msamaha na kufuta maovu; mchana wake ni Saumu, ndani ya usiku wake mna kisimamo

[1] Imetolewa siku ya ijumaa, tarehe mbili, mwezi wa Ramadhani, mwaka elfu moja mia nne na thalathini na tisa, ndani ya Msikiti wa Mtume swala na salamu zimshukie

kinacho imarishwa na Swala na Qur'ani. Ndani yake milango ya Pepo inafunguliwa, na milango ya Moto inafungwa, na mashetani wanafungwa minyororo, na mnao ndani yake Usiku ambao ni bora kuliko miezi elfu moja, aliyenyimwa kheri yake basi huyo ndiye aliyenyimwa hakika.

Ramadhani ni uwanja mkunjufu wa kushindana katika ibada, na zawadi ya kutakasa nafsi kutokana na uchafu na maafa, ni mwezi mkarimu, ndani yake [thawabu za] amali zinadishwa, na makosa na dhambi zinafutwa;

[Mtume] swala na salamu za Allah zimshukie zimshukie alisema:

«**Swala tano** [za faradhi], **Swala ya Ijumaa hadi Ijumaa, na Ramadhani hadi Ramadhani; ni zenye kufuta madhambi yalio baina yao, pindi yakiepukwa madhambi makubwa**», imepokewa na Muslim.

Waisilamu wanatekeleza ndani yake [Ramadhani] nguzo miongoni za Uisilamu, nao ni sura ya kimatendo ya utukufu wa Dini hii, na kuleta kwake umoja wa Waisilamu, na ndani yake inadhihiri kauli yake [Allah] aliyetukuka:

﴿إِنَّ هَٰذِهِۦٓ أُمَّتُكُمۡ أُمَّةٗ وَٰحِدَةٗ وَأَنَا۠ رَبُّكُمۡ فَٱعۡبُدُونِ﴾

{Kwa hakika huu umma wenu ni umma mmoja, na Mimi ni Mola wenu Mlezi. Kwa hivyo niabuduni Mimi}. (Al-Anbiya`: 92).

kufaidika na misimu ya kheri ni futahi kutoka kwa Allah kwa anayempenda miongoni mwa waja wake. Ndani ya Ramadhani zinakusanyika ibada kubwa kubwa za msingi; Swala ni fungamano baina ya mja na Mola wake Mlezi, wala haifarikiani na Muisilamu katika maisha yake yote,

Na swala ya mwanamume katika jamaa ni faradhi, nayo inazidi Swala yake ya nyumbani na sokoni kwa daraja ishirini na saba, na inastahiki kwa muisilamu atake usaidizi juu ya [kuitekeleza] saumu kwa swala, na awe na hadhi kubwa ya Swala ya usiku; kwani

«**Atakayesimama** [usiku wa] **Ramadhani** [kwa ibada] **hali ya kuamini na kutarajia; atasamehewa madhambi yake yaliotangulia**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea,

«**Atakaye swali pamoja na imamu hadi** [imamu] **aondoke; ataandikiwa kisimamo cha usiku kamili**», imepokewa na Tirmidhi,

Na Zaka na Sadaka zinatwahirisha mali ya kuyakuza, na ni ukwasi wa nafsi na utakaso, basi athari yake iko wazi juu ya nafsi, mali na wana, inakinga balaa, inaleta matarajio, na atakayewakirimu waja wake [Allah],

basi Allah naye atamkirimu, [Mtume] swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**Allah aliyetukuka amesema: Ewe mwanadamu, toa** [Sadaka kuwapa maskini] **Nami nitoe kuk**upa», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Na «**kila mtu yuko chini ya kivuli cha sadaka yake**» siku ya Kiyama, basi toa Sadaka hata kama ni kwa kichache, na nafsi yako ihisi vizuri nalo, na mpumbaze nayo [Sadaka] yule aliyenyimwa, na «**atakaye futurisha aliyefunga, atapewa mfano wa ujira wake**», na ilikuwa katika uongofu wake [Mtume] swala za na salamu zimshukie ni: Kutoa na kufanya ukarimu; huzawadia kama mtu asiyeogopa umaskini, akitoa hukithirisha, hamrudishi mwenye kuomba, na hakuombwa kitu ila alikitoa, na [Mtume] swala na salamu zimshukie alikuwa mtoaji zaidi ndani ya Ramadhani; alikuwa ndani yake [Ramadhani] ni kama upepo ulioachiliwa [kwa kutoa sana].

Na Saumu ni ibada kubwa zaidi katika mwezi huu mtukufu, Waislamu wanajiandaa ndani yake na uchamngu:

﴿يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ كُتِبَ عَلَيۡكُمُ ٱلصِّيَامُ كَمَا كُتِبَ عَلَى ٱلَّذِينَ مِن قَبۡلِكُمۡ لَعَلَّكُمۡ تَتَّقُونَ﴾

{Enyi mlio amini! Mmefaradhishiwa Saumu, kama walivyo faradhishiwa waliokuwa kabla yenu ili mpate kuchamngu}, (Al-Baqarah: 183).

[Ibada ya Saumu] thawabu zake hazina idadi wala mipaka:

«**Amali zote za binadamu ni zake, ila Saumu, kwani hakika hiyo ni yangu, nami ndiye mwenye kuilipa**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Na **«atakayefunga Ramadhani hali ya kuamini na kutarajia; atasamehewa madhambi yake yaliotangulia**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea,

Na Saumu inawakinga watu wake na shari na maovu; [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

«**Saumu ni kinga**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Na miongoni mwa amali njema zinazovunwa [ndani ya Ramadhani] ni: Umra; [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

«**Umra ya ndani ya Ramadhani inalingana na Hija**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Na Qur'ani ni Maneno ya Allah na hoja yake juu waja wake, nayo ni chimbuko la hekima, na alama ya Utume, hakuna njia ya kufikisha kwa Allah ila hiyo, wala hatuna kuokoka ila kwayo,

Ni nuru ya akili na macho, anayeikurubia anapata utukufu, na anaye shikana nayo anapata ushindi, kuisoma ni ujira na uongofu, kuidurusu ni elimu na kupata kukita, kuifanyia kazi ni kinga na amani, na kuifunza na kuilingania ni taji lilio juu ya vichwa vya watu wema.

Na Qur'ani iliteremka ndani ya Ramadhani, na inasistizwa kukithirisha kuisoma, kuizingatia, kuisoma, kuisomesha, kuitendea kazi na kuiitikia; [Allah] mwenye ushindi na ukuu:

﴿شَهۡرُ رَمَضَانَ ٱلَّذِيٓ أُنزِلَ فِيهِ ٱلۡقُرۡءَانُ هُدٗى لِّلنَّاسِ وَبَيِّنَٰتٖ مِّنَ ٱلۡهُدَىٰ وَٱلۡفُرۡقَانِۚ﴾

{Mwezi wa Ramadhani ambao imeteremshwa humo Qur'ani kuwa ni uwongofu kwa watu, na hoja zilizo wazi za uwongofu na upambanuzi}, ( Al-Baqarah:185).

Na alikuwa Jibrili salamu zimshukie akisoma [Qur'ani] pamoja na Nabii wetu swala na salamu za Allah zimshukie ndani yake mara moja kwa kila mwaka, na katika mwaka aliokufa ndani yake alisoma naye Qur'ani mara mbili.

Na Dua ni ibada na yenye kukurubisha [kwa Allah], ni ghanima bila ya tabu, na ni faida isio na uzito ndani yake, nayo inaleta ukunjufu wa maisha, na ni adui wa kila balaa, na «**hataangamia yeyote aliyeshikamana na Dua**», kupitia kwayo mja hufikia malengo yake, na anapata matakwa yake;

Ni mangapi ya mbali imeyakurubisha?! mangapi mazito imeyawepesisha?! Na majanga mangapi imeyaletea faraja?! Na Dua yenye kuitikiwa zaidi ni ile iliokuwa ndani ya mwisho wa usiku, na mja anapojidhalilisha mbele ya Mola wake Mlezi Allah humuitikia maombi yake,

Na pindi nafsi inapokuwa na njaa moyo hulainika na husafika, na aliyefunga maombi yake hayarudishwi, ibnu Rajab Allah amrehemu amesema: "Aliyefunga yuko ndani ya ibada usiku na mchana, na maombi yake huitikiwa anapokuwa ndani ya Saumu na anapofuturu, basi yeye katika mchana wake ni mwenye kufunga na kusubiri, na katika usiku wake ni mwenye kula na kushukuru», basi aliyeafikiwa ni yule anayekithirisha kugonga mlango wa mbingu [kwa Dua], na akaichumia nafsi yake akiba ndani ya michana na usiku hii.

Na Dhikri ya Allah [kumtaja na kumkumbuka] ni ibada adhimu ilio nyepesi, na atakayemtaja Allah, Allah naye humtaja, na endapo ulimi wa mja hautashughulika na kumtaja Allah, basi utamshughulisha yeye na

maneno yasio muhimu na ya maasi,

Muamala mwema ni katika Dini, na viumbe wanao stahiki zaidi ihsani yako: ni yule ambaye Allah aliambatanisha haki yao na haki Yake, basi wazazi wawili ima ni Pepo yako au ni Moto wako, nao ndio watu wanao stahiki zaidi usuhuba wako mwema;

[Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

«**limedhalilika pua, kisha limedhalilika pua, kisha limedhalilika pua**, ikasemwa: la nani ewe Mtume wa Allah? Akasema: **atakayewadiriki wazazi wake katika uzee - mmoja wao au wote wawili - kisha asiingie Peponi** [kwa sababu yao]», imepokewa na Muslim,

Na «**kizazi kimeangikwa katika 'Arshi' [ya Allah], kinasema: atakayeniunga, naye Allah amuunge, na atakayenikata, naye Allah amkate**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Na «**atakayependa kukunjuliwa riziki yake, na kuongezewa athari yake; basi aunge kizazi chake**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Na ni katika ukamilifu wa utiifu: Kuihifadhi [Saumu] kutokana na kila lenye kuivunja au lenye kuipunguza, na mwenye kufunga atakiwa kuwa na bidii zaidi ya kuhifadhi ibada yake, na kuhifadhi Saumu yake kutokana na yenye kuivunja na kuifisidi;

[Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

«**Inapokuwa siku ya kufunga mmoja wenu basi asiseme maneno machafu, wala asipige kelele, na endapo mtu atamtusi au ampige vita; basi aseme: Mimi ni mtu aliyefunga**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Na ilikuwa katika mwenendo wa wema waliotangulia Allah awarehemu, wakifunga wanakaa Misikitini, na wakisema: «Tunahifadhi Saumu zetu, wala hatusengenyi mtu»

Imamu Ahmad Allah amrehemu alisema: "inampasa aliyefunga aichunge Saumu yake kutokana na ulimi wake, wala asizozane».

**Na baada ya haya, enyi Waisilamu:**

Wema haukamiliki, wala hausimami juu ya muundi wake na sehemu yake, ila kwa mapenzi yenye kumpeleka mtu katika ikhlaasi, na kwa ukweli unaopelekea katika kumfuata [Mtume] vizuri, na amali haiwi yenye kukurubisha kwa Allah hadi uwe msukumo wa kuifanya ni Imani wala si

mazoea [ada] na matamanio [ya nafsi], au kutaka kusikika na kuonekana, lazima lengo lake liwe ni kutaka thawabu za Allah na radhi zake. Pindi itakusanyika ndani ya amali Imani na kutarajia, basi itapatikana kabuli na msamaha.

***'Audhu billaahi mina sh-shaitwaani rrajiim'***

﴿وَسَارِعُوٓاْ إِلَىٰ مَغۡفِرَةٖ مِّن رَّبِّكُمۡ وَجَنَّةٍ عَرۡضُهَا ٱلسَّمَٰوَٰتُ وَٱلۡأَرۡضُ أُعِدَّتۡ لِلۡمُتَّقِينَ﴾

{Na yakimbilieni maghfira ya Mola wenu Mlezi, na Pepo ambayo upana wake ni mbingu na ardhi, iliyowekwa tayari kwa wachamngu). (Al-Imran: 133).

Allah anibarikie mimi na nyinyi katika Qur'ani tukufu...

## HOTUBA YA PILI

Sifa njema zote astahili Allah kwa wema Wake [kwetu], na shukrani zote astahili Yeye kwa kutuafikia na kutuneemesha, na nashuhudia ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake hana mshirika; ili kuadhimisha shani yake, na nashuhudia ya kwamba Nabii wetu Muhammad ni mja Wake [Allah] na Mtume wake, swala na salamu nyingi za Allah zimshukie yeye, watu wa nyumba yake na Masahaba wake.

**Enyi Waisilamu:**

Dunia pamoja na furaha zake na huzuni zake zitaisha, na umri utaisha kwa urefu wake na ufupi wake, na wote watakutana na Mola wao, na wakati huo

﴿لَا يَنفَعُ مَالٌ وَلَا بَنُونَ * إِلَّا مَنْ أَتَى ٱللَّهَ بِقَلْبٍ سَلِيمٍ﴾

{Siku ambayo kwamba mali hayatofaa kitu wala wana * Isipokuwa mwenye kumjia Mwenyezi Mungu na moyo safi}; (Ash-Shuaraa` :88).

Basi upokeeni mwezi wenu kwa toba ya ukweli, na tieni azima ya kufaidika nao, na kuamirisha nyakati zake kwa utiifu, kwani uhai si kitu ila pumzi za kuhesabiwa, na ajali zenye mipaka, na vuneni nyakati bora.

Na aliyepunjwa ni yule aliyediriki Ramadhani na asisamehewe; [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

«**imedhalilika pua ya mtu aliyeingiliwa na Ramadhani, kisha itoke kabla ya yeye kusamehewa**», imepokewa na Tirmidhi.

Na «**ambaye hajaacha kusema urongo na kuufanyia kazi, basi Allah hana haja na yeye kuacha chakula chake na kinywaji chake**», imepokewa na Bukhari.

Na miongoni mwa mambo makubwa zaidi ya kusiluhisha nyoyo ni: kumdhukuru Allah, kudumu na Qur'ani tukufu, kisimamo cha usiku na kukaa na watu wema.

Kisha jueni kuwa Allah amewaamrisha kumswalia na kumsalimia Nabii wake...

## MASIKU YENYE THAMANI[1].

Sifa za ukamilifu zote ni za Allah, tunamhimidi, tunamuomba msaada, tunamuomba msamaha, na tunajilinda na Allah kutokana na shari za nafsi zetu, na kutokana na amali zetu mbovu, yule ataongozwa na Allah, basi hakuna wa kumpoteza, na atakayempoteza hakuna wa kumuongoza, nashuhudia ya kwamba hapana apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake, hana mshirika, na nashuhudia kuwa Nabii wetu Muhammad ni mja wake na Mtume wake, swala na salamu za Allah nyingi zimshukie yeye, watu wake, na masahaba wake.

**Ama baada ya himdi hii:**

Basi enyi waja wa Allah mcheni Allah haki ya kumcha, na mchungeni [chungeni amri zake na makatazo yake] katika siri na minong'ono.

**Enyi Waisilamu:**

Umetukuzwa umma huu kwa mwezi ambao ndani yake nafsi zinatwahirika kutokana na maasi na madhambi, na kutokana na sifa za kasoro, waisilamu ndani yake wanashughulisha nyakati zao kwa utiifu na kusoma Qur’ani, Saumu inazitakasa nafsi zao, swala [ya usiku] inarekebisha tabia zao, na Qur’ani inalainisha nyoyo zao, wanashindana kwa mambo mema ndani ya usiku wake, na kwa utoaji ndani ya michana yake.

Na katika kumi lake la mwisho, amali zinazidi na matarajio yanafikiwa, na usiku wake unahuishwa kwa ibada na Swala ya usiku, Aisha Allah amridhie alisema: «Nabii Swala na salamu za Allah zimshukie alikuwa pindi liingiapo kumi la mwisho, akihuisha usiku wake, akiamsha watu wake [usiku ili wafanye ibada], na akifanya bidii na akibana kibwebwe», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea,

Na [Mtume] swala na salamu za Allah zimshukie huzidisha amali zake njema ndani ya mwezi wa Ramadhani, na analihusu kumi lake la mwisho kwa kuzidisha [amali], Aisha Allah amridhie alisema: «Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie alikuwa akijitahidi ndani ya kumi la mwisho, jitihada ambayo hakuwa akiifanya katika masiku mengineo»,

[1] Imetolewa siku ya Ijumaa, tarehe kumi na nane ya mwezi wa Ramadhani, mwaka elfu moja, mia nne na ishirini na sita hijria, ndani ya Msikiti wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie.

imepokewa na Muslim.

Hakika huo [mwezi wa Ramadhani] ni soko wanaloshindana ndani yake wachangamfu, na ni mtihani unaotahini hima [za waja], na mnao ndani ya kumi la mwisho usiku uliobarikiwa, ambao ndio taji la usiku wa mwaka, ulio mwingi wa baraka, masaa yake ni yenye cheo na thamani, amali kidogo ndani yake ni nyingi [katika thawabu], na amali nyingi ina inalipwa mara dufu:

﴿لَيۡلَةُ ٱلۡقَدۡرِ خَيۡرٞ مِّنۡ أَلۡفِ شَهۡرٖ﴾

{Laylatul Qadri ni bora kuliko miezi elfu}, (Al-Qadr: 3).

viumbe wakubwa wanateremka kutoka mbinguni ili kuushuhudia usiku huo:

﴿تَنَزَّلُ ٱلۡمَلَٰٓئِكَةُ وَٱلرُّوحُ فِيهَا بِإِذۡنِ رَبِّهِم﴾

{Huteremka Malaika na Roho [Jibrili] katika usiku huo kwa idhini ya Mola wao Mlezi}, (Al-Qadr: 4).

Mwenye kusimama usiku wake kwa kufanya ibada ni mwenye kusamehewa, Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**atakaye simama usiku wa cheo** [laylatul qadr] **hali ya kuamini na kutarajia; atasamehewa madhambi yake yaliotangulia**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea,

Ndani yake milango [ya Pepo] inafunguliwa, na mazungumzo yanasikiwa, na ndani yake Mola mlezi anaunga na kukata, anapatia na kunyima, na anadunisha na kunyanyua,

Aisha Allah amridhie alisema:

«Nilisema: Ewe Mtume wa Allah, waonaje nikijua 'laylatul Qadri' ni usiku gani, nisemeje? [Mtume] **akasema: sema: *'Allahuma innaka afuwwun, tuhibbul afwa, fa'afu annii*** [ewe Mola, hakika wewe ni mwenye kuafu sana, unapenda afua, basi niafi nami]», imepokewa na Tirmidhi.

**Enyi Waisilamu:**

«**Swala bora zaidi baada ya faradhi ni Swala ya usiku**», imepokewa na Muslim,

Na hakuwa Nabii swala na salamu za Allah zimshukie akiacha kisimamo cha usiku safarini au mjini, na alikuwa akiiswali kwa kusimama na kukaa, hadi miguu yake ikifura.

Na msafara wa Masahaba ulifuata uongofu huo, [Allah] aliyetukuka

amesema:

﴿إِنَّ رَبَّكَ يَعۡلَمُ أَنَّكَ تَقُومُ أَدۡنَىٰ مِن ثُلُثَيِ ٱلَّيۡلِ وَنِصۡفَهُۥ وَثُلُثَهُۥ وَطَآئِفَةٞ مِّنَ ٱلَّذِينَ مَعَكَ﴾

{Hakika Mola wako Mlezi anajua ya kuwa hakika wewe unakesha karibu na thuluthi mbili za usiku, na nusu yake, na thuluthi yake. Na baadhi ya watu walio pamoja nawe kadhaalika}, ( Al-Muzzammil: 20).

Na aliyetakasika akasema:

﴿سِيمَاهُمۡ فِي وُجُوهِهِم مِّنۡ أَثَرِ ٱلسُّجُودِ﴾

{Alama zao zi katika nyuso zao, kwa athari ya kusujudu}. ( Al-Fat-h: 29).

Na kusimama katika giza [kufanya ibada usiku] kwa ajili Allah ni katika amali njema:

﴿كَانُواْ قَلِيلٗا مِّنَ ٱلَّيۡلِ مَا يَهۡجَعُونَ﴾

{Walikuwa wakilala kidogo tu usiku}, (Ad-Daariyat: 17).

Na Swala ya usiku ni jambo kubwa linalotarajiwa, na ni jambo takatifu zaidi lenye kutangulizwa [kwa Allah], nayo ni katika sababu za kuingia Peponi, [Mtume] mteule swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**Enyi watu, toeni salamu, lisheni chakula, ungeni kizazi, na swalini usiku hali watu wamelala, mtaingia Peponi kwa salama**», imepokewa na Tirmidhi.

Na mwenye kusimama usiku wa Ramadhani amebashiriwa msamaha wa madhambi; [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

**«atakaye simama** [usiku wa] **Ramadhani** [kwa ibada] **hali ya kuamini na kutarajia; atasamehewa madhambi yake yaliotangulia**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea,

**Enyi Waisilamu:**

Dua ni kamba ilionyoshwa [kuunganisha] baina ya mbingu na aradhi, nayo ni ngawira [inayopatikana] bila ya tabu, na ni miongoni mwa dawa zenye manufaa zaidi katika kutibu maradhi:

﴿أَمَّن يُجِيبُ ٱلۡمُضۡطَرَّ إِذَا دَعَاهُ وَيَكۡشِفُ ٱلسُّوٓءَ﴾

{Au nani yule anayemjibu mwenye shida pale anapo mwomba, na akaiondoa dhiki}, (An-Naml: 62).

Na ndani ya kila usiku mna kipindi cha kuitikiwa maombi, ambacho ndani yake milango [ya mbingu] inafunguliwa, na Mkarimu anatoa, basi omba ndani yake unalotaka.

Kwani hazina za Allah zimejaa, Naye ni Mtoaji na ni Mkarimu sana, na kuwa na yakini ya kuitikiwa; kwani Mola Mlezi ni muweza, na mnushurie mashtaka yako, hakika Yeye ni Mwenye kurehemu, Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema

«**Hakika mnao ndani ya usiku kipindi, hakiafiki Muisilamu yeyote akiwa anamuomba Allah kheri ya dunia na akhera ila Allah humpa, na hilo ni kila usiku**», imepokewa na Muslim.

Na umande wa usiku ni nyakati za kutarajiwa kukubaliwa maombi; ilisemwa kuambiwa Nabii swala na salamu za Allah zimshukie

«ni maombi gani yenye kusikika [kuitikiwa] zaidi? Akasema**: Ndani ya mwisho wa usiku, na mwisho wa Swala za faradhi**», imepokewa na Tirmidhi.

Na mja anahitajia kufuta uchafu wa makosa yake, na kudhihirisha unyonge na mahitaji mbele ya Allah. Na miongoni mwa hali za kujidhalilisha mbele ya Allah zinazotarajiwa zaidi ni: Kufanya itikafu katika nyumba miongoni mwa nyumba za Allah ili kutaka afua Yake. Nabii wetu swala na salamu za Allah zimshukie alikuwa akifanya itikafu katika kumi la mwisho la Ramadhani.

Na pindi mja anapomkurubia Mola wake Mlezi basi Allah atamfanyia upole, na atamfikishia wema kwa njia asizozitarajia, na atamkinga na shari kwa njia asizozitarajia.

**Enyi Waisilamu:**

Zaka ni nguzo kati ya nguzo za Uisilamu, na jengo miongoni mwa majengo yake, kwayo mafungamano baina ya Waisilamu yanapata nguvu, na ndani yake mna kutwahirisha nafsi na kuitakasa kutokana na ubahili;

[Allah] aliyetukuka amesema:

﴿خُذۡ مِنۡ أَمۡوَٰلِهِمۡ صَدَقَةٗ تُطَهِّرُهُمۡ وَتُزَكِّيهِم بِهَا﴾

{Chukua Sadaka katika mali zao, uwasafishe na uwatakase kwazo}, (At-Taubah: 103).

Nayo ni haki ya wajibu, na faradhi ya lazima, mnao ndani yake kuvuta baraka, nyongeza na badala kutoka kwa Allah,

﴿وَمَآ أَنفَقۡتُم مِّن شَيۡءٖ فَهُوَ يُخۡلِفُهُۥ﴾

{Na chochote mnachokitoa basi Yeye huwapa badala yake}. (Saba`: 39).

Mnao ndani ya zaka kuzinyanyua roho na tabia kwa ukarimu na utoaji,

kwayo unakamilika uadilifu na ukunjufu wa maisha, na mafakiri wapata saada, nayo ni pambo la wakwasi na wachamngu, na wasia wa Manabii:

﴿وَٱذۡكُرۡ فِي ٱلۡكِتَٰبِ إِسۡمَٰعِيلَۚ إِنَّهُۥ كَانَ صَادِقَ ٱلۡوَعۡدِ وَكَانَ رَسُولٗا نَّبِيّٗا * وَكَانَ يَأۡمُرُ أَهۡلَهُۥ بِٱلصَّلَوٰةِ وَٱلزَّكَوٰةِ وَكَانَ عِندَ رَبِّهِۦ مَرۡضِيّٗا﴾

{Na mtaje katika Kitabu Ismail. Bila ya shaka yeye alikuwa ni mkweli wa ahadi, na alikuwa Mtume, Nabii * Na alikuwa akiwaamrisha watu wake Swala na Zaka, na alikuwa mbele ya Mola wake Mlezi mwenye kuridhiwa} (Maryam: 54-55),

Na hakika yamekuja makemeo makali kwa yule aliyeifanyia [Zaka] ubahili; [Allah] aliyetukuka anasema:

﴿وَٱلَّذِينَ يَكۡنِزُونَ ٱلذَّهَبَ وَٱلۡفِضَّةَ وَلَا يُنفِقُونَهَا فِي سَبِيلِ ٱللَّهِ فَبَشِّرۡهُم بِعَذَابٍ أَلِيمٖ﴾

{Na wanaokusanya dhahabu na fedha, wala hawazitumii katika Njia ya Allah, wabashirie khabari ya adhabu iliyo chungu} (At-Taubah: 34),

Na imesihi kutoka kwa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie kuwa alisema:

«**Atakaye pewa mali na Allah na asitoe Zaka yake; mali yake yatamathilishwa kuwa Shuja'an aqra'a** - naye ni nyoka wa kiume, nywele za kichwa chake zimeng'oka kwa ajili ya wingi wa sumu yake -, **ana vitone vyeusi viwili juu ya macho yake, atamtatia [shingoni] siku ya Kiyama, kisha amuume mdomo mwake, kisha awe akimuambia: Mimi ni mali yako, mimi ni kanzi yako,** kisha Nabii swala na salamu za Allah zimshukie akasoma: **{Wala wasidhani wale ambao wanafanya ubahili katika aliyo wapa Allah katika fadhila zake kuwa ni kheri yao. Bali hiyo ni shari kwao. Watafungwa kongwa za yale waliyo yafanyia ubahili Siku ya Kiyama}**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Basi kuwa myenyekevu wa moyo kwa maskini, na mnyoshee mkono wa msaada, mkurubie, na mhurumie, wala usimdharau fukara, kwani hakika wengi wa watu wa Peponi ni mafukara. Na toa kwa mkono mkarimu, na nafsi karimu; Allah atakubariki katika mali na wana.

Sadaka ni dawa ya maradhi na ishara zake, basi watafuteni madhaifu na wenye haja, na toeni mtaruzukiwa, na warehemuni nanyi mtarehemewa, kwani hajawahi lia shida fukara ila ni kwa sababu ya upungufu wa mkwasi [katika kutoa haki ya Zaka],

***'Audhu billaahi mina sh-shaitwaani rrajiim'***

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ ٱرۡكَعُواْ وَٱسۡجُدُواْۤ وَٱعۡبُدُواْ رَبَّكُمۡ وَٱفۡعَلُواْ ٱلۡخَيۡرَ لَعَلَّكُمۡ تُفۡلِحُونَ﴾

{Enyi mlio amini! Rukuuni na msujudu, na muabuduni Mola wenu Mlezi, na tendeni mema, ili mfanikiwe} (Al-Hajj: 77).

Allah anibarikie mimi na nyinyi katika Qur-ani tukufu...

## HOTUBA YA PILI

Sifa njema zote anastahili Allah kwa wema Wake [kwetu], na shukrani zote anastahili Yeye kwa kutuafikia na kutuneemesha, na nashuhudia ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake hana mshirika; ili kuadhimisha shani yake, na nashuhudia ya kwamba Nabii wetu Muhammad ni mja Wake [Allah] na Mtume wake, swala na salamu nyingi za Allah zimshukie yeye, watu wa nyumba yake na Masahaba wake.

**Ama baada ya haya:**

Mwezi huu adhimu una utukufu, ni juu ya Muisilamu kuepusha Saumu yake na mambo yenye kuivunja, na ahifadhi macho yake kutokana na kutazama ya haramu, maskio yake kutokana na maovu, na wakati wake kutokana na mambo ya upuzi,

Kwani wakati uliosalia katika huu mwezi unao cheo chake, na mda mchache ndani yake una thamani, ndani yake kunapatika mazingatio [ya kufanya mtu] kulia kwa madhambi. Ni wangapi ambao Mola Mlezi anawaacha huru na Moto?! Na ni mateka wa madhambi wangapi ambao Allah amewaunga baada kukatika, na akawaandikia saada baada uovu uliokuwa mrefu?!

Na ni juu ya mwanamke aepuke vizuizi vya njiani [njia ya kuenda kwa Allah], na asitoke kuenda sokoni ila kwa haja, pamoja na kujilazimisha kujihifadhi, sitara na haya.

Na ni juu ya Muisilamu atangulize katika masiku ya Ramadhani iliyo barikiwa toba ya ukweli, kwa kutenda mema yenye kubaki, kwani uhai si kitu ila pumzi za kuhesabika, na nyakati zilizo na mipaka, na masiku ndio vipando vya kuwafikisha katika [ukomo wa] nyakati hizi.

Basi tendeni [mema], tarajieni thawabu], na tuchukueni bishara njema; na aliyepunjwa hakika ni aliye ondoka au aliye shughulika na yasiokuwa utiifu kwa Allah, na aliyenyimwa hakika ni yule aliyenyimwa 'laylatul qadri', au akadiriki Ramadhani na asisamehewe; [Mtume] swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**imedhalilika pua ya mtu aliyeingiliwa na Ramadhani, kisha ikatoka kabla ya yeye kusamehewa**», imepokewa na Tirmidhi.

Kisha jueni kuwa Allah amewaamrisha kumswalia na kumsalimia Nabii wake...

# FADILA ZA KUMI LA MWISHO[1]

Sifa za ukamilifu zote ni za Allah, tunamhimidi, tunamuomba msaada, tunamuomba msamaha, na tunajilinda na Allah kutokana na shari za nafsi zetu, na kutokana na amali zetu mbovu, yule ataongozwa na Allah, basi hakuna wa kumpoteza, na atakayempoteza hakuna wa kumuongoza, nashuhudia ya kwamba hapana apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake, hana mshirika, na nashuhudia kuwa Nabii wetu Muhammad ni mja wake na Mtume wake, swala na salamu za Allah nyingi zimshukie yeye, watu wake, na masahaba wake.

**Ama baada ya himdi hii:**

Basi enyi waja wa Allah mcheni Allah haki ya kumcha, na mchungeni [chungeni amri zake na makatazo yake] katika siri na minong'ono.

**Enyi Waislamu:**

Allah amewamiminia waja wake neema, na akafuatisha kwao vipawa vyake, na vipawa vyake havina mpaka kiupana na kiwingi; Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**Mkono wa Allah umejaa, kutoa hakuupunguzi**, **Yeye ni mwenye kutoa sana usiku na mchana**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Anatoa mengi ya kheri na mazuri; utoaji wake umewaenea waja wake, kheri zake zimedumu kwao, neema na riziki yake imefulililiza, na anaanza kutoa kabla ya kuombwa, anapoombwa anawapa zaidi ya inavyofikiriwa, wala hakuna yeyote mbinguni wala ardhini aliye kando na vipawa hivyo.

Na Allah ndiye mstahiki zaidi wa wenye kuhimidiwa na kutajwa kwa ajili ya neema zake, [kutajwa] kwa kutakasiwa mapenzi, ibada, kunasibishwa neema kwake, na kutumiwa neema hizo katika kumtii Yeye,

Na ni katika vipawa vyake aliyetakasika: Msamaha wake kwa anayemtaka kati ya waja wake; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿إِنَّ ٱللَّهَ لَعَفُوٌّ غَفُورٌ﴾

[1] Imetolewa katika siku ya ijumaa, tarehe ishirini na moja ya mwezi wa Ramadhani, mwaka wa elfu moja mia nne thalathini na nane hijria, katika Msikiti wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie.

{Hakika Allah ni Msamehevu Mwenye maghfira.}, (Al-Hajj: 60).

Basi hajaacha kuwa Msamehevu wa madhambi ya waja wake kwa kuacha kuadhibu kwa mengi yake.

[Allah] aliyetakasika amesema:

﴿وَيَعۡفُواْ عَن كَثِيرٍ﴾

{na anasamehe mengi}, (Ash-Shuaraa: 30).

Ni msamehevu anapenda kusamehe, na anapenda kutoka kwa waja wake: kufanya sababu za wao kupata msamaha wake, kutaka maghufira, kutubia, kurudi kwake na amali njema.

Na ndani ya Ramadhani vipawa vya Allah vinadhihiri na msamaha wake [pia], ndani yake amali zinakithiri, makosa na madhambi yanafutwa, ni mwezi wa saumu, Qur'ani, kisimamo [cha usiku], wema na ihsani, kufanya biashara na Allah ndani yake ni jambo lenye kuzidishwa maradufu [katika ujira], Ibnul Jawzi Allah amrehemu amesema: "Thawabu za amali zinazidi kwa kuzidi utukufu wa wakati, kama zinavyozidi kwa ajili ya kuhudhuria kwa moyo na kutakasika kwa kusudio [Niya]".

Na Swala ya usiku ndani ya Ramadhani ina shani kubwa, Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**atakaye simama [usiku wa] Ramadhani [kwa ibada] hali ya kuamini na kutarajia; atasamehewa madhambi yake yaliotangulia**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea,

Na atakayedumu na kisimamo cha usiku ataingia Peponi kwa salama; Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**Enyi watu, toeni salamu, lisheni chakula, ungeni kizazi, na mswali usiku hali watu wamelala, mutaingia Peponi kwa salama**», imepokewa na Ahmad.

Na sadaka ni dalili ya imani ya mwenyewe, na siku ya Kiyama kila mtu atakuwa chini ya kivuli cha sadaka yake, na mtoaji ameahidiwa ushindi na msamaha. [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿وَمَآ أَنفَقۡتُم مِّن نَّفَقَةٍ أَوۡ نَذَرۡتُم مِّن نَّذۡرٖ فَإِنَّ ٱللَّهَ يَعۡلَمُهُۥ﴾

{Na chochote mnachotoa au nadhiri mnazoweka basi hakika Allah anajua}, (Al-Baqarah: 270).

Na ndani ya siku bora ujira wake unazidi; «Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alikuwa mtoaji zaidi kati ya watu, na alikuwa akitoa zaidi ndani ya Ramadhani», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Na thawabu za Umra ndani ya Ramadhani ni kubwa; Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**Umra ndani ya Ramadhani inakuwa sawa na Hija**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Na dua ndio ibada yenyewe, na roho lake, na kwayo unavutwa ukunjufu wa maisha na inakingwa balaa, na aliyefunga ana maombi yenye kuitikiwa;

Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**Watu watatu maombi yao hayarudishwi: Anayefunga hadi afungue, kiongozi muadilifu, na maombi ya aliyedhulumiwa, Allah anayanyanyua juu ya mawingu, na anayafungulia milango ya mbingu, na Mola mlezi Anasema: Naapa kwa Ushindi wangu na Utukufu wangu! Nitakunusuru, nitakunusuru, hata kama ni baada ya mda**», imepokewa na Tirmidhi.

Na Qur'ani ni hoja, muombezi, uongofu na ponyo, Allah amemuahidi mwenye kuisomo malipo mazuri, na ziada ya fadhila zake;

[Allah] aliyetakasika amesema:

﴿إِنَّ ٱلَّذِينَ يَتۡلُونَ كِتَٰبَ ٱللَّهِ وَأَقَامُواْ ٱلصَّلَوٰةَ وَأَنفَقُواْ مِمَّا رَزَقۡنَٰهُمۡ سِرّٗا وَعَلَانِيَةٗ يَرۡجُونَ تِجَٰرَةٗ لَّن تَبُورَ * لِيُوَفِّيَهُمۡ أُجُورَهُمۡ وَيَزِيدَهُم مِّن فَضۡلِهِۦٓۚ﴾

{Hakika wale wanaosoma Kitabu cha Mwenyezi Mungu, na wakashika Sala, na wakatoa kwa siri na kwa dhaahiri katika tulivyowaruzuku, hao hutaraji biashara isiyobwaga * Ili Yeye awalipe ujira wao kwa ukamilifu, na awazidishie kutokana na fadhila zake}, (Fatwir: 29-30).

Allah ameiteremsha kwa ajili ya kuizingatia, mnao ndani yake mawaidha na mazingatio, Abu Bakar Swidiiq Allah amridhie anapoongoza watu katika Swala, walio nyuma yake hukurubia kutomsikia, kwa ajili ya hofu ya Allah.

Ramadhani ni uwanja mkunjufu wa wenye kushindana ndani yake, ni zama za wingi wa mambo mema, kheri nyingi na kuunga kizazi, ndani yake nafsi zinakuwa safi, na tabia zinatakasika, na waja wanakurubiana baina yao, na wanahurumiana baadhi yao kwa baadhi.

Ni msimu uliobarikiwa, masiku yake yameshatangaza kuisha, na mwenye akili ni yule atakayepatiliza kumi lake la mwisho, akaliimarisha kwa kujikurubisha kwa Allah na matendo ya utiifu, na akauhifadhi mchana wake na akauhuisha usiku wake; «Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie alikuwa akijitahidi ndani ya kumi la mwisho, jitihada

ambayo hakuwa akifanya katika masiku mengineo», imepokewa na Muslim. Na «kumi la mwisho linapoingia, Nabii Swala na salamu za Allah zimshukie huuhuisha usiku wake, huamsha watu wake [usiku ili wafanye ibada], na hufanyu bidii na hubana kibwebwe», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea,

Na inapendekezwa ndani ya usiku hizi zilizobarikiwa kukithirisha kumdhukuru Allah na kusoma Qur'ani, Ibnu Rajab Allah amrehemu amesema: "ama nyakati zilizo bora - kama mwezi wa Ramadhani, hasa hasa usiku ambayo ndani yake inatafutwa 'laylatul qadr' -, basi inapendekezwa kukithirisha kusoma Qur'ani, ili kuupatiliza wakati».

Na inastahiki kwa Muisilamu awe na pupa ndani yake [kumi la mwisho la Ramadhani] ya maombi yenye manufaa zaidi na yenye kukusanya [kheri nyingi] zaidi; Aisha Allah amridhie amesema:

«Ewe Mtume wa Allah, waonaje nikiafiki 'laylatu Qadri', nisemeje? [Mtume] akasema: Sema: ***'Allahuma innaka 'afuwwun, tuhibbul 'afawa, fa'afu 'annii*** [ewe Mola, hakika wewe ni mwenye kuafu sana, unapenda afua, basi niafu nami]», imepokewa na Ahmad.

Na itikafu ni katika amali bora zaidi za kufuta madhambi na kunyanyua daraja «Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alikuwa akifanya itikafu katika kumi la mwisho la Ramadhani mpaka Allah mwenye ushindi na utukufu alipomfisha, kisha wake zake nao wakafanya itikafu baada yake», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea,

Az-Zuhri Allah amrehemu amesema: «Ajabu ya Waisilamu! Wameacha itikafu na hali Nabii swala na salamu za Allah zimshukie hakuiacha tokea alipoingia Madina hadi alipofishwa na Allah».

Na inapasa kwa aliye ndani ya itikafu awe faraghani kwa ajili ya ibada, na ajishughulishe na kusudio lake kuu, mbali na tangamano la ziada, mazungumzo ya ziada, na usingizi wa ziada, wala asitoke Msikitini ila kwa haja isiyo na budi, Ibnul Qayyim Allah amrehemu amesema: «na kusudio la itikafu na roho yake ni: Moyo kukaa faragha na Allah aliyetukuka, kukusanyika kwake, kuwa faragha naye [Allah], na kuwacha kujishughulisha na viumbe, na kushughulika naye [aliyetukuka] pekee; kiasi cha kuwa kumdhukuru Yeye, kumpenda, na kuelekea kwake sehemu ya hamu ya moyo na fikra zake».

Na ndani ya kumi la mwisho: Waisilamu wanaitafuta 'laylatul qadr'; Nabii swala na salamu alisema:

«**itafuteni 'laylatul qadr' ndani ya kumi la mwisho la Ramadhani**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea,

Ni usiku mtukufu wenye cheo na sharafu, Allah aliteremsha Sura [kamili] kuihusu; ili kuadhimisha cheo chake, kutukuza jambo lake, na kunyanyua shani yake, akasema:

﴿وَمَآ أَدۡرَىٰكَ مَا لَيۡلَةُ ٱلۡقَدۡرِ﴾

{Na nini kitachokujuulisha nini Laylatul Qadri?}, (Al-Qadr: 2).

[Allah] ameujaalia kuwa wenye baraka, ulio na kheri nyingi; akasema:

﴿إِنَّآ أَنزَلۡنَٰهُ فِي لَيۡلَةٖ مُّبَٰرَكَةٍ﴾

{Hakika tumekiteremsha katika usiku uliobarikiwa}, (Ad-Dukhan: 3).

Na ni miongoni mwa baraka zake: Kuteremka kwa Qur-ani ndani yake; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿إِنَّآ أَنزَلۡنَٰهُ فِي لَيۡلَةِ ٱلۡقَدۡرِ﴾

{Hakika Sisi tumeiteremsha Qur'ani katika Laylatul Qadri, Usiku wa Cheo Kitukufu}, (Al-Qadr: 1).

Na ndani yake Malaika wanateremka ardhini; [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿تَنَزَّلُ ٱلۡمَلَٰٓئِكَةُ وَٱلرُّوحُ فِيهَا بِإِذۡنِ رَبِّهِم مِّن كُلِّ أَمۡرٖ﴾

{Huteremka Malaika na Roho katika usiku huo kwa idhini ya Mola wao Mlezi kwa kila jambo}, (Al-Qadr: 4).

Ibnu Kathiir Allah amrehemu amesema: "Ndani ya usiku huu kunakithiri kuteremka kwa Malaika; kwa ajili ya wingi wa baraka zake, na Malaika huteremka zinapoteremka baraka na rehema, kama wanavyoteremka wakati inaposomwa Qur’ani, na wavizunguka vikao vya dhikri, na wanaweka chini mbawa zao kwa mtafuta elimu [ya sheria] kwa ukweli, ili kumuadhimisha»,

Ni usiku wa salamu, amani na utulivu; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿سَلَٰمٌ هِيَ حَتَّىٰ مَطۡلَعِ ٱلۡفَجۡرِ﴾

{Amani usiku huo mpaka mapambazuko ya alfajiri}, (Al-Qadr:5).

Yaani: Salama kutokana na kila shari. Kuuhuisha kwa ibada ni ghanima kubwa; [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿خَيۡرٞ مِّنۡ أَلۡفِ شَهۡرٖ﴾

{ni bora kuliko miezi elfu}, (Al-Qadr: 3).

Na ndani yake zinakadiriwa kadari za viumbe za mwaka; [Allah] aliye na ushindi na utukufu amesema:

﴿فِيهَا يُفۡرَقُ كُلُّ أَمۡرٍ حَكِيمٍ * أَمۡرًا مِّنۡ عِندِنَآ﴾

{Katika usiku huu hubainishwa na kuandikwa kila amri [ya kikadari na ya kisheria] ambayo Allah kaihukumu * amri itokayo kwetu}, (Ad-Dukhan: 4-5).

**Enyi Waisilamu:**

Basi [jueni] mazingatio ya amali ni mwishoni, na muhimu ni ukamilifu wa mwishoni wala si upungufu wa mwanzoni, na aliyefanya vibaya katika yaliotangulia, basi atubie katika yaliobakia; kwani mlango wa toba uko wazi, na vipawa vya Allah vinatolewa:

﴿وَمَن يَتَّقِ ٱللَّهَ يَجۡعَل لَّهُۥ مَخۡرَجًا﴾

{Na anayemcha Allah, humtengezea njia ya kutokea}. (At-Twalaq: 2).

***'Audhu billaahi mina sh-shaitwaani rrajiim'***

﴿يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓاْ إِن تَتَّقُواْ ٱللَّهَ يَجۡعَل لَّكُمۡ فُرۡقَانٗا وَيُكَفِّرۡ عَنكُمۡ سَيِّـَٔاتِكُمۡ وَيَغۡفِرۡ لَكُمۡۗ وَٱللَّهُ ذُو ٱلۡفَضۡلِ ٱلۡعَظِيمِ﴾

{Enyi mlio amini! Mkimcha Allah, atakupeni kipambanuo, na atakufutieni makosa, na atakusameheni, na Allah ni Mwenye fadhila kubwa} .(Al-Anfal: 29).

Allah anibarikie mimi na nyinyi katika Qur-ani tukufu...

## HOTUBA YA PILI

Sifa njema zote anastahili Allah kwa wema Wake [kwetu], na shukrani zote anastahili Yeye kwa kutuafikia na kutuneemesha, na nashuhudia ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake hana mshirika; ili kuadhimisha shani yake, na nashuhudia ya kwamba Nabii wetu Muhammad ni mja Wake [Allah] na Mtume wake, swala na salamu nyingi za Allah zimshukie yeye, watu wa nyumba yake na Masahaba wake.

**Enyi Waislamu:**

Dunia ni masaa na masiku, nayo ni katika kurasa za umri, na umri wa mtu ni amali yake, basi mwema ni yule atakayedumisha siku zake kwa amali njema.

Na aliyefuzu ni yule aliyepatiliza muda wake kwa mambo ya kheri, wala hakupoteza chochote katika wakati wake, na aliyepunjwa ni yule jambo lake limesambaratika, moyo wake ukaghafilika, na akafuata matamanio yake,

Na aliyenyimwa hakika ni yule aliyenyimwa kheri ndani ya Ramadhani, Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**imedhalilika pua ya mtu aliyeingiliwa na Ramadhani, kisha ikatoka kabla ya yeye kusamehewa**», imepokewa na Tirmidhi.

Kisha jueni kuwa Allah amewaamrisha kumswalia na kumsalimia Nabii wake...

# USIKU WA CHEO (LAYLATUL QADR)[1]

Sifa za ukamilifu zote ni za Allah, tunamhimidi, tunamuomba msaada, tunamuomba msamaha, na tunajilinda na Allah kutokana na shari za nafsi zetu, na kutokana na amali zetu mbovu, yule ataongozwa na Allah, basi hakuna wa kumpoteza, na atakayempoteza hakuna wa kumuongoza, nashuhudia ya kwamba hapana apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake, hana mshirika, na nashuhudia kuwa Nabii wetu Muhammad ni mja wake na Mtume wake, swala na salamu nyingi za Allah zimshukie yeye, watu wake, na masahaba wake.

**Ama baada ya himdi hii:**

Enyi waja wa Allah, mcheni Allah haki ya kumcha, na kamateni Uislamu katika kishiko madhubuti kabisa.

**Enyi Waislamu:**

Allah amewaumba binadamu na majini kwa ajili ya kumuabudu Yeye, naye aliyetakasika hawahitajii wao, wala wao hawaachi kumuhitajia Yeye, na kumuabudu Yeye peke yake ni sababu ya kuingia Pepo za neema;

«alikuja mtu kwa Nabii swala na salamu za Allah zimshukie akasema: Nijulishe amali endapo nitaifanya nitaingia Peponi, [Mtume] akasema: **Muabudu Allah wala usimshirikishe na chochote, usimamishe Swala iliowajibishwa, utoe Zaka iliofaradhishwa, na ufunge Ramadhani**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Na kumuabudu Yeye aliyetukuka ni kila sehemu na wakati; Na [Allah] aliyetakasika amejaalia Ramadhani ni msimu wa kumfanyia Ibada; basi alikuwa [Mtume] swala na salamu za Allah zimshukie akiihusu [Ramadhani] na ibada asio zihusu nazo miezi mingineo, na Masahaba Allah awaridhie walikuwa na bidii ya kupatiliza [kwa ibada] nyakati zake, na Abu Huraira na masahibu zake Allah awaridhie «wanapofunga wanakaa Msikitini, na wakisema: Tunaitwahirisha Saumu yetu», imepokewa na Abu Nueim.

Na ni katika fadhila za Allah aliyetakasika [juu ya waja]: kuwa amejaalia

---

[1] Imetolewa siku ya ijumaa, tarehe ishirini ya mwezi wa Ramadhani, mwaka elfu moja mia nne na thalathini na tano hijria, ndani ya Msikiti wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie.

ndani ya msimu wa Ramadhani mna misimu; amefadhilisha kumi la mwisho juu ya usiku wote wa mwezi, na akajaalia 'Laylatul qadr' ni usiku bora zaidi katika mwezi wa Ramadhani, na Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alikuwa akilihusu kumi la mwisho la Ramadhani na amali, ambazo hakuwa akizifanya katika Miezi iliosalia, basi «kumi la mwisho linapoingia, Nabii Swala na salamu za Allah zimshukie huuhuisha usiku wake, huamsha watu wake [usiku ili wafanye ibada], na hufanya bidii na hubana kibwebwe», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea,

[Allah] aliyetakasika amenyanyua shani yake [Laylatul qadar] na akaiadhimisha, akasema aliyetakasika:

﴿وَمَآ أَدۡرَىٰكَ مَا لَيۡلَةُ ٱلۡقَدۡرِ﴾

{Na nini kitachokujulisha nini Laylatul Qadri?}, (Al-Qadr: 2).

Amali chache ndani yake ni nyingi [katika ujira], na nyingi ndani yake inazidishwa maradufu, ibada ndani ni bora kuliko ibada za miezi elfu, na kitabu bora zaidi kati ya vitabu vya mbinguni kimeteremka ndani yake:

﴿إِنَّآ أَنزَلۡنَٰهُ فِي لَيۡلَةِ ٱلۡقَدۡرِ﴾

{Hakika tumekiteremsha katika usiku uliobarikiwa}.( Al-Qadr: 1).

Na ni katika kuitukuza Qur’ani tukufu: kukithirisha kuisoma ndani ya mwezi ilioteremka ndani yake:

﴿شَهۡرُ رَمَضَانَ ٱلَّذِيٓ أُنزِلَ فِيهِ ٱلۡقُرۡءَانُ﴾

{Mwezi wa Ramadhani ambao imeteremshwa humo Qur'ani},(Al-Baqarah:185).

Na Jibrili salamu za Allah zimshukie alikuwa akiisoma Qur’ani na Nabii swala na salamu za Allah zimshukie ndani ya kila usiku wa Ramadhani, na ilipokuwa mwaka ambao [Mtume] alikufa ndani yake, alisoma naye Qur’ani ndani ya Ramadhani mara mbili; basi inastahiki kwa Muisilamu akithirishe kukisoma kitabu cha Allah ndani ya mwezi wa fadhila; ili apate fadhila za Qur’ani ndani ya mwezi wa Ramadhani.

'Laylatul qadr' ni usiku mtukufu, Allah ametueleza kuwa miongoni mwa yanayojiri ndani yake: ni kuwa hubainisha ndani yake kila jambo - yaani: Qadari ya mwaka na yatakayojiri yake miongoni mwa: ajali, riziki, kheri na shari, na mengineo, hunukuliwa kutoka *'lauh Mahfuudh'* hadi kwa waandishi,

An-Nawawi Allah amrehemu amesema: "Imeitwa Al-Qadr': Yaani

Usiku wa hukumu na upambanuzi", Mola mlezi anaunga ndani yake na kukata, anadunisha na kunyanyua, na apatia na kunyima; kama alivyosema aliyetukuka:

﴿فِيهَا يُفۡرَقُ كُلُّ أَمۡرٍ حَكِيمٍ﴾

{Katika usiku huu hubainishwa na kuandikwa kila amri [ya kikadari na ya kisheria] ambayo Allah kaihukumu}, (Ad-Dukhan: 4)

Yaani: anayoyakadiria Allah ndani yake ni yenye kukita, haibadilishwi.

Ni usiku unaoshuka ndani yake Malaika kwa ajili ya wingi wa baraka zake - na Malaika huteremka pamoja na baraka na rehema -, ni usiku ambao ni salama itokayo kwa Allah, basi wote ni kheri, hamna shari ndani yake, hadi kuchomoza kwa alfajiri, na imefichwa mda wake ndani ya kumi la mwisho, ili wajitahidi wenye kuitaka katika kuitafuta, na waislamu huzidisha ibada ndani ya kumi lote.

Na inapendekezwa kwa mja ndani ya kumi [la mwisho] kuzidisha Dua, Swala, na kutenda kheri, ibnu Mas-uud Allah amridhie amesema: "kila kitu kina matunda, na matunda ya Swala ni Dua",

Aisha Allah amridhie amesema:

«Nilisema: Ewe Mtume wa Allah, waonaje nikijua 'laylatu Qadri' ni usiku gani, niseme nini? [Mtume] akasema: **sema: *'Allahuma innaka afuwun, tuhibbul afawa, fa'afuannii*** ' [ewe Mola, hakika wewe ni mwenye kuafu sana, unapenda afua, basi niafu nami]», imepokewa na Tirmidhi,

Na aliyesimama usiku wake kwa ibada ni mwenye kusamehewa madhambi; [Mtume] swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**Atakayesimama usiku wa cheo [laylatul qadar] hali ya kuamini na kutarajia; atasamehewa madhambi yake yaliotangulia**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Na [Mtume] swala na salamu zimshukie alikuwa akifanya itikafu ndani ya kumi la mwisho ili kuitafuta 'Laylatul qadr'; Aisha Allah amridhie amesema: «Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alikuwa akifanya itikafu katiku kumi la mwisho la Ramadhani hadi Allah alipomfisha», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea. Ibnu Battwaal Allah amrehemu amesema: "Basi hili linajulisha kuwa itikafu ni miongoni mwa sunnah zilizosisitizwa; sababu ni kati ya yale aliyodumu nayo Nabii swala na salamu za Allah zimshukie, basi inapasa kwa waumini kumuiga Nabii wao katika hilo".

Mnao ndani ya itikafu kukata mafungamano na viumbe ili kuwa faragha kwa kumuabudu Muumba, na pindi mafungamano na Allah yatapata nguvu basi Mola Mlezi atamridhia mja, ibnu Shihaab Allah amrehemu: "Ajabu ya Waisilamu! Wameacha itikafu, na hali Nabii swala na salamu za Allah zimshukie hakuacha itikafu kutoka aingie Madina hadi Allah alipomfisha".

Na mwenye kufanya itikafu anakaa faragha kwa kumtii Allah, na anakaa katika hali hiyo muda wote wa itikafu yake, akiwa ndani ya sehemu ipendezayo zaidi kwa Allah - Misikiti -, anakaa ndani yake katika utiifu na ibada, unyenyekevu na utulivu, na maombi, basi haiwi hamu yake ila ni Allah, wala hana anayemkusudia ila Yeye, wala hana matakwa ila ni Yeye mwenye ushindi na utukufu, na atoke katika itikafu [anapomaliza] ikiwa moyo wake umefanya itikafu kwa kumtii Allah, na awe ndiye mwenye kutubia sana na mwenye kurudi sana kwa Allah aliyetakasika.

Na Ramadhani ni msimu wa watoaji sadaka; wakwasi wanashindana ndani yake kwa kutoa na kutumia katika mambo ya kheri, kufanya mema, kunyoosha mkono wa usaidizi, kutoa Sadaka kwa maskini na mafukara;

basi «**tibuni wagonjwa wenu kwa sadaka**»,

Hakika inakinga maradhi na alama zake, na watafuteni madhaifu na wenye haja, na toeni mtaruzukiwa, na warehemuni nanyi mtarehemewa, kwani hajawahi lia shida fukara ila ni kwa sababu ya upungufu wa mkwasi [katika kutoa haki ya Zaka],

Na miongoni mwa sifa za watu wema: ni kuwa wanavyo vitoa wanavitakasia Uso wa Allah, hawataki kutoa kwa mafukara sifa wala Dua, basi usijaaliye Sadaka yako ni kwa ajili ya kutarajia fukara akuombee, lakini iwe ni kutarajia Radhi za Allah pekee;

[Allah] aliyetakasika amesema:

﴿وَيُطْعِمُونَ ٱلطَّعَامَ عَلَىٰ حُبِّهِۦ مِسْكِينًا وَيَتِيمًا وَأَسِيرًا ۞

إِنَّمَا نُطْعِمُكُمْ لِوَجْهِ ٱللَّهِ لَا نُرِيدُ مِنكُمْ جَزَآءً وَلَا شُكُورًا﴾

{Na huwalisha chakula, juu ya kukipenda kwake, masikini, na yatima, na wafungwa * Hakika sisi tunakulisheni kwa kwa kukusudia Uso wa Allah. Hatutaki kwenu malipo wala shukrani}, (Al-Insan: 8-9).

Sheikhul Islaam Allah amrehemu amesema: «atakayetaka kutoka kwa mafukara Dua au sifa atakuwa ametoka katika aya hii».

**Na baada ya haya, enyi Waisilamu:**

Ndani ya Ramadhani ujira unakuwa maradufu, na milango ya Pepo inafunguliwa, na kuja kwake ni mapito yasiokubali kungojea, na mwezi wake ni mfupi haukubali kufanya upungufu [katika ibada], basi kimbilia katika mambo ya kheri, na ukiweza yeyote asikushide katika kujikurubisha kwa Allah basi fanya.

***'Audhu billaahi mina sh-shaitwaani rrajiim'***

﴿مَنْ عَمِلَ صَٰلِحًا مِّن ذَكَرٍ أَوْ أُنثَىٰ وَهُوَ مُؤْمِنٌ فَلَنُحْيِيَنَّهُۥ حَيَوٰةً طَيِّبَةً ۖ

وَلَنَجْزِيَنَّهُمْ أَجْرَهُم بِأَحْسَنِ مَا كَانُوا۟ يَعْمَلُونَ﴾

{Mwenye kutenda mema, mwanamume au mwanamke, naye akawa ni Muumini, tutamhuisha maisha mema; na tutawapa ujira wao kwa bora ya waliyokuwa wakiyatenda}. (An-Nahl: 97).

Allah anibarikie mimi na nyinyi katika Qur-ani tukufu...,

## HOTUBA YA PILI

Sifa njema zote astahili Allah kwa wema Wake [kwetu], na shukrani zote astahili Yeye kwa kutuafikia na kutuneemesha, na nashuhudia ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake hana mshirika; ili kuadhimisha shani yake, na nashuhudia ya kwamba Nabii wetu Muhammad ni mja Wake [Allah] na Mtume wake, swala na salamu nyingi za Allah zimshukie yeye, watu wa nyumba yake na Masahaba wake.

**Enyi Waislamu:**

Ramadhani ni sehemu ya kuvuna toba na kurudi kwa Allah, ndani yake Allah anasamehe telezo, na anafuta ndani yake makosa na maovu; basi muelekeeni Allah kwa kujutia upungufu, na kuazimia kuepuka madhambi,

Naye [Allah] aliyetakasika anampenda mwenye kurudi kwake, na anafurahia toba ya mwenye kutubia; basi tekelezeni sababu za kupata rehema za Mola wenu Mlezi, na takeni kuteremshiwa riziki kwa kuleta istighfari, na mwenye akili ni yule atakayepatiliza mda uliosalia wa mwezi wake huu, aushughulishe kwa utiifu, na ibada kubwa, na abadilishe maovu kwa mema.

Na endapo utakuwa mvivu wa kufanya ya kheri; basi kumbuka kauli yake aliyetukuka:

﴿أَيَّامًا مَّعْدُودَاتٍ﴾

{siku maalumu za kuhisabika}, (AL-Baqarah: 184).

Na atakayekuwa ni mwenye kutubia sana ndani ya mwezi wake, na katika amali yake ni mwenye kusibu, basi alithibitishe vizuri jengo, na amshukuru Allah kwa neema, wala asiwe kama mwanamke anaye uzongoa uzi wake baada ya kwisha kuusokota ukawa mgumu.

Kisha jueni kuwa Allah amewaamrisha kumswalia na kumsalimia Nabii wake...

## KUONDOKA KWA RAMADHANI[1]

Sifa za ukamilifu zote ni za Allah, tunamhimidi, tunamuomba msaada, tunamuomba msamaha, na tunajilinda na Allah kutokana na shari za nafsi zetu, na kutokana na amali zetu mbovu, yule ataongozwa na Allah, basi hakuna wa kumpoteza, na atakayempoteza hakuna wa kumuongoza, nashuhudia ya kwamba hapana apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake, hana mshirika, na nashuhudia kuwa Nabii wetu Muhammad ni mja wake na Mtume wake, swala na salamu nyingi za Allah zimshukie yeye, watu wake, na masahaba wake.

**Ama baada ya himdi hii:**

Enyi waja wa Allah, mcheni Allah haki ya kumcha, na kamateni Uislamu katika kishiko madhubuti kabisa.

Allah anawateremshia waja wake misimu ya kheri ili wajiandae na ibada, na kwa hikma yake aliyetakasika siku zilizobarikiwa hazidumu; ili washindane wenye kushindana katika wakati wake, na mwenye mapungufu anyimwe fadhila zake.

Na Waislamu wameingiliwa na wakati bora: mchana wake ni saumu na kutoa, na usiku wake ni Tahajudi, Qur'ani na Dua, ni wangapi waliofanya maovu wamesamehewa?! Ni wangapi walikuwa wamenyimwa wamepewa?! Na ni wangapi waliokuwa waovu wameandikiwa saada?! Na ni maombi mangapi yameitikiwa?! Na ni amali ngapi njema zimekuwa sababu ya kuingia Peponi?!

Masiku yaliobarikiwa yametangaza kuondoka, na yamekaribia kumalizika, Waisilamu wanauaga msimu huu. Ni wangapi waliohai hawatarudiwa tena na Ramadhani, na wameshaandikwa katika idadi ya watu wa makaburini, na anakuwa rahani ya amali yake?! [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿كُلُّ نَفْسٍ بِمَا كَسَبَتْ رَهِينَةٌ﴾

{Kila nafsi imo rahanini kwa mabaya iliyoyachuma}. (Al-Muddathir: 38)

Na mwenye akili ni yule anayepatiliza muda uliosalia wa mwezi wake

---

[1] Imetolewa siku ya ijumaa, tarehe ishirini na tisa ya mwezi wa Ramadhani, mwaka elfu moja mia nne na thalathini na tatu hijria, ndani ya Msikiti wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie.

huu, aushughulishe kwa utiifu, na ibada kubwa, na akabadilisha maovu kwa mema. Sheikul Islam Allah amrehemu amesema: "Mazingatio ni ukamilifu wa mwishoni, wala si upungufu wa mwanzoni",

Basi atakaye kuwa ni mwenye kutubia sana ndani ya mwezi wake, na katika amali yake ni mwenye kusibu, basi alithibitishe vizuri jengo, na amshukuru Allah kwa neema, wala asiwe kama mwanamke anaye uzongoa uzi wake baada ya kwisha usokota ukawa mgumu.

Na atakayekuwa muovu; basi atubie kwa Allah madamu mlango wa toba uko wazi, na Ramadhani ni msimu wa waasi kutubia.

**Enyi Waisilamu:**

Istighfari ndio hatima ya amali njema, zinahitimishwa nayo Swala, Hija, na mwisho wa Usiku, na miongoni mwa mambo bora kabisa ya kuhitimishiwa nayo Ramadhani ni: wingi wa istighfari, kusoma Qur-ani, na Dua; kwani amali zinazingatiwa mwisho wake.

Na pindi mja atakamilisha amali na kuitimiza, inabaki juu yake kuogopa kutokubaliwa, au kufisidika baada ya kukubaliwa; Ali Allah amridhie amesema: "kuweni na hamu zaidi ya kukubaliwa amali kuliko hamu yenu ya kufanya amali", [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿إِنَّمَا يَتَقَبَّلُ ٱللَّهُ مِنَ ٱلۡمُتَّقِينَ﴾

{Hakika Allah huwapokelea wachamngu}, (Al-Maidah: 27).

Salama ibnu Diinaar Allah amrehemu amesema: "Hofu ya amali isije kukubaliwa ni zito zaidi kuliko amali yenyewe".

Na mtu ameamrishwa kumuabudu Ar-Rahmaan katika kila wakati; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿وَٱعۡبُدۡ رَبَّكَ حَتَّىٰ يَأۡتِيَكَ ٱلۡيَقِينُ﴾

{Na muabudu Mola wako Mlezi mpaka ikufikie Yakini [mauti]}, (Al-Hijr: 99).

Na aliyekuwa akifanya mema ndani ya Ramadhani, basi adumu nayo [hata nje yake], Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**amali ipendezao zaidi kwa Allah ni yenye kudumu zaidi hata ikiwa chache**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

An-Nawawi Allah amrehemu amesema: «amali chache yenye kudumu ni bora kuliko nyingi yenye kukatika, na chache yenye kudumu imekuwa bora kuliko nyingi yenye kukatika; kwa sababu kwa kudumu amali unadumu

utiifu, dhikri, kumchunga [Allah katika amri zake na makatazo yake], nia, ikhlasi, na kumuelekea Muumba aliyetakasika, na chache yenye kudumu inatoa matunda, kiasi kwamba inazidi ile nyingi yenye kukatika kwa ziada nyingi".

Na ni katika ukarimu wa Allah kuwa amali njema za ndani ya Ramadhani ni zenye kudumu mwaka mzima; basi ni sheria kufunga siku sita za Shawwali, na atakayezifunga huwa ni kama kufunga mwaka, na kufunga jumatatu, alhamisi na siku tatu katika kila mwezi ni jambo linalopendekezwa, na kusoma Qur’ani tukufu ni jambo lililoamrishwa daima, na kisimamo cha usiku ni sheria kila usiku linalokuchwa jua la mchana wake, na Sadaka ni mlango uliofunguliwa, na nayo Dua, mja hana ukwasi nayo katika maisha yake yote.

Na aliyefanya amali, basi [ajue kuwa] alama ya kukubaliwa ni: aiunganishe na ibada nyengine, na alama ya kukataliwa ni: afuatishe maasi baada ya ibada ile, na ni uzuri ulioje wa jema linalofanywa baada ya ovu likalifuta [ovu lile], na uzuri zaidi kuliko huo ni jema linalofuata baada ya jema, na ni uovu ulioje wa ovu baada ya jema linaofuta athari yake, basi zitakaseni nafsi zenu kwa kufanya utiifu na kuwa na ikhlasi katika ibada, na kutubia kwa Allah kikweli; yote hayo mukitumai msamaha wake mkuu, rehema yake kunjufu, na vipawa vyake vingi.

***'Audhu billaahi mina sh-shaitwaani rrajiim'***

﴿وَرَحۡمَتِي وَسِعَتۡ كُلَّ شَيۡءٖۚ فَسَأَكۡتُبُهَا لِلَّذِينَ يَتَّقُونَ وَيُؤۡتُونَ ٱلزَّكَوٰةَ وَٱلَّذِينَ هُم بِـَٔايَٰتِنَا يُؤۡمِنُونَ﴾

{Na rehema yangu imeenea kila kitu. Lakini nitawaandikia khasa wanao mchamngu, na wanaotoa zaka, na wale ambao wanaziamini alama zetu} (Al-A'raf: 156).

Allah anibarikie mimi na nyinyi katika Qur-ani tukufu...

## HOTUBA YA PILI

Sifa njema zote anastahili Allah kwa wema Wake [kwetu], na shukrani zote anastahili Yeye kwa kutuafikia na kutuneemesha, na nashuhudia ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake hana mshirika; ili kuadhimisha shani yake, na nashuhudia ya kwamba Nabii wetu Muhammad ni mja Wake [Allah] na Mtume wake, swala na salamu nyingi za Allah zimshukie yeye, watu wa nyumba yake na Masahaba wake.

Enyi Waislamu:

Allah ameamrisha Zaka ya Fitri mwishoni mwa mwezi huu, ili iwe twahara kwa aliyefunga kutokana na upuzi na maneno machafu, na chakula kwa maskini,

Ibnu Umar Allah amridhie yeye na babake amesema: «Mtume wa Allah swala na salamu zimshukie amefaradhisha Zaka ya Fitri: swa'a ya tende, au swa'a ya ngano, juu ya kila mtumwa na aliye huru, mume na mke, mdogo na mkubwa katika waislamu», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea,

Na inapendekezwa kumtolea Zaka aliye tumboni, wala hakuna ubaya kupeleka Zaka mji mwingine, na kuitoa sehemu uliyo ndio bora, na inajuzu kuitoa kabla ya Eid kwa siku au siku mbili, na inapendekezwa kuitoa pindi unapotoka kuenda kwa Swala ya Eid.

Na Eid ni furaha na fali njema ya kukubaliwa amali njema ndani ya mwezi wa baraka; basi ni sheria kuleta Tabira kutokea usiku wake hadi kufikia Swala ya Eid,

Na Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alikuwa akitoka kuenda kuswali na nguo zake mzuri zaidi, na «siku ya Fitri hatoki hadi ale tende», imepokewa na Bukhari, na «inapokuwa siku ya Eid alikuwa akibadilisha njia - yaani: hutoka akitumia njia kuenda uwanjani wa kuswali, na akirudi na njia nyengine -», imepokewa na Bukhari.

Na aliyekosa Swala ya Eid (na imamu), basi ataiswali kwa sifa yake ile ile, sawa akiwa uwanja wa kuswali au penginepo - kwa jamaa au bila ya jamaa -, Bukhari Allah amrehemu amesema: «akikosa Eid ataswali rakaa mbili».

Na Eid ni furaha na kuwa na bishara ya fadhila ya Allah alizowajalizia waja wake; basi mja akithirishe siku ya Eid kumdhukuru Allah; Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**na hakika siku hizi: ni siku za kula, kunywa, na kumdhukuru Allah mwenye ushindi na utukufu**», imepokewa na Abu Daaud.

Na Muisilamu atahadhari siku ya Eid kuvuka mpaka aliouweka Allah; akavunja alioyajenga ndani ya Ramadhani, na iwe na juu ya uso wake nuru ya utiifu na utulivu wa ibada, siku ya Eid na nyenginezo.

Kisha jueni kuwa Allah amewaamrisha kumswalia na kumsalimia Nabii wake...

# KUISHA KWA RAMADHANI[1]

Sifa za ukamilifu zote ni za Allah, tunamhimidi, tunamuomba msaada, tunamuomba msamaha, na tunajilinda na Allah kutokana na shari za nafsi zetu, na kutokana na amali zetu mbovu, yule ataongozwa na Allah, basi hakuna wa kumpoteza, na atakayempoteza hakuna wa kumuongoza, nashuhudia ya kwamba hapana apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake, hana mshirika, na nashuhudia kuwa Nabii wetu Muhammad ni mja wake na Mtume wake, swala na salamu nyingi za Allah zimshukie yeye, watu wake, na masahaba wake.

**Ama baada ya himdi hii:**

Basi enyi waja wa Allah mcheni Allah haki ya kumcha, na mchungeni [chungeni amri zake na makatazo yake] katika siri na minong'ono.

**Enyi Waislamu:**

Ndani ya mwezi huu mtukufu waislamu wameishi zama zilizo bora, mchana wake ni Saumu na usiku wake kisimamo [cha ibada], ndani yake misikiti imeimarishwa kwa utiifu na Qur'ani, wanageuka geuka katika vipindi vyake baina ya Dhikri, Dua, na kutoa [Sadaka], na hali nyoyo zina utulivu na unyenyekevu, na viungo vimeelekea [kwa Allah]; basi waumini wakaonja ndani yake tamu ya Imani na ladha yake,

Na hizi ndizo siku zake, zimeshatangaza kuondoka, na zimekaribia kumalizika, na aliyeafikiwa ni yule atakaye patiliza vipindi vyake vilivyosalia; kwani mazingatio ya amali ni mwishoni, na ukamilifu wa mwishoni, na atakayekuwa ni mwenye kutubia sana ndani ya mwezi wake, na katika amali yake ni mwenye kusibu, basi alithibitishe vizuri jengo, na amshukuru Allah kwa neema, wala asiwe kama mwanamke anayeuzongoa uzi wake baada ya kwisha usokota ukawa mgumu.

Kuihifadhi ibada ni uzito zaidi kuliko kuifanya, na ni miongoni mwa maombi ya watu wema: "Ewe Allah, mimi nakuomba [uniafikie kufanya] amali njema na kuihifadhi".

Na aliyekuwa na kasoro basi akimbilie kutubia toba iliotakaswa; kwani

---

[1] Imetolewa siku ya ijumaa, tarehe ishirini na sita ya mwezi wa Ramadhani, mwaka elfu moja mia nne na arubaini hijria, ndani ya Msikiti wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie.

mlango bado uko wazi. [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

«**imedhalilika pua ya mtu aliyeingiliwa na Ramadhani, kisha ikatoka kabla ya yeye kusamehewa**», imepokewa na Ahmad.

Kuweni na hamu zaidi ya kukubaliwa amali kuliko hamu yenu ya kufanya amali:

﴿إِنَّمَا يَتَقَبَّلُ ٱللَّهُ مِنَ ٱلۡمُتَّقِينَ﴾

{akasema: Hakika Allah huwapokelea wachamngu}, (Al-Maidah: 27). na muumini hukusanya baina ya kutenda wema na kuogopa, hali yake ni kama alivyosema [Allah] aliyetakasika:

﴿وَٱلَّذِينَ يُؤۡتُونَ مَآ ءَاتَواْ وَّ قُلُوبُهُمۡ وَجِلَةٌ أَنَّهُمۡ إِلَىٰ رَبِّهِمۡ رَٰجِعُونَ﴾

{Na wale ambao wanatoa walichopewa, na hali nyoyo zao zinaogopa kwa kuwa watarejea kwa Mola wao Mlezi}, (Al-Mu`minun: 60).

Aisha Allah amridhie alisema:

«Ewe Mtume wa Allah, Wao ni wale wanaokunywa khamri na wanaiba? [Mtume] akasema: **Hapana, ewe binti wa as-siddiiq! Lakini wao ni wale wanaofunga, wanaoswali na wanaotoa Sadaka, na hali wao wanaogopa zisije zikakataliwa kutoka kwao: {Basi wote hao ndio wanaokimbilia katika mambo ya kheri, na ndio watakaotangulia kuyafikia}**», imepokewa na Tirmidhi.

Na mwezi wa Ramadhani ungaisha; lakini kwa hakika wakati wa kufanya amali haishi ila kwa kufa; [Allah] mwenye ushindi na utukufu amesema:

﴿وَٱعۡبُدۡ رَبَّكَ حَتَّىٰ يَأۡتِيَكَ ٱلۡيَقِينُ﴾

{Na muabudu Mola wako Mlezi mpaka ikufikie Yakini [mauti]}, (Al-Hijr: 99).

Na amali chache yenye kudumu ni bora kuliko nyingi yenye kukatika; [Mtume] swala na salamu zimshukie:

«**amali inayopendeza zaidi kwa Allah ni yenye kudumu zaidi hata ikiwa chache**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Na miongoni mwa alama za kukubaliwa jema: ni kufanya jema baada yake, na ni uzuri ulioje wa jema linalofanywa baada ya ovu likalifuta [ovu lile], na uzuri zaidi kuliko huo ni jema linalofuata baada ya jema,

Na ni katika fadhila za Allah kuwa amali za Ramadhani zinadumu mwaka mzima; miongoni mwa kusoma Qur-ani, Sadaka, Saumu, Umra,

Dua, kisimamo [cha usiku], na mengineo aliyowaamrisha Allah waja wake kwa njia ya kudumu.

Na mnao katika kudumu kwa utiifu na kurefuka muda wake neema kwa waja wema, na utulivu wa jicho kwa waumini; [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿إِنَّ ٱلَّذِينَ قَالُواْ رَبُّنَا ٱللَّهُ ثُمَّ ٱسۡتَقَٰمُواْ تَتَنَزَّلُ عَلَيۡهِمُ ٱلۡمَلَٰٓئِكَةُ أَلَّا تَخَافُواْ وَلَا تَحۡزَنُواْ وَأَبۡشِرُواْ بِٱلۡجَنَّةِ ٱلَّتِي كُنتُمۡ تُوعَدُونَ﴾

{Hakika walio sema: Mola wetu Mlezi ni Allah! Kisha wakanyooka sawa, hao huwateremkia Malaika wakawaambia: Msiogope, wala msihuzunike; nanyi furahini kwa Pepo mliyokuwa mkiahidiwa}. (Fusswilat: 30).

Na mnao mwishoni mwa Ramadhani bishara kwa watu wa Saumu na kisimamo cha usiku; [Mtume] swala na salamu,zimshukie alisema:

«**atakayefunga Ramadhani hali ya kuamini na kutarajia; atasamehewa madhambi yake yaliotangulia, na atakayesimama usiku wa cheo [laylatul qadr] hali ya kuamini na kutarajia; atasamehewa madhambi yake yaliotangulia**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea,

na «**atakayesimama [usiku wa] Ramadhani [kwa ibada] hali ya kuamini na kutarajia; atasamehewa madhambi yake yaliotangulia**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea,

Na «**aliyefunga anazo furaha mbili: furaha wakati wa kufungua kwake, na furaha atakapokutana na Mola wake**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Maisha ni pumzi za kuhesabika, na nyakati zilizo na kikomo, na hakika umri unaokisiwa na pumzi ni haraka kumalizika, na mnao katika kumalizika Ramadhani mazingatio ya kuondoka kwa dunia na vilivyomo ndani yake, kana kuwa nyinyi mnazingatiwa kwa amali, na zishapita, na kwa dunia na ishaisha, na wakati huo kila mja ni rahani wa matendo yake, na mwenye kufaulu ni aliyeitikia mwito wa Mola wake Mlezi, na akawa miongoni mwa watenda mema.

***'Audhu billaahi mina sh-shaitwaani rrajiim'***

﴿مَنۡ عَمِلَ صَٰلِحٗا مِّن ذَكَرٍ أَوۡ أُنثَىٰ وَهُوَ مُؤۡمِنٞ فَلَنُحۡيِيَنَّهُۥ حَيَوٰةٗ طَيِّبَةٗۖ وَلَنَجۡزِيَنَّهُمۡ أَجۡرَهُم بِأَحۡسَنِ مَا كَانُواْ يَعۡمَلُونَ﴾

{Mwenye kutenda mema, mwanamume au mwanamke, naye akawa ni Muumini, tutamhuisha maisha mema; na tutawapa ujira wao kwa bora ya waliyokuwa wakiyatenda}, (An-Nahl: 97).

Allah anibarikie mimi na nyinyi katika Qur-ani tukufu...

## HOTUBA YA PILI

Sifa njema zote anastahili Allah kwa wema Wake [kwetu], na shukrani zote anastahili Yeye kwa kutuafikia na kutuneemesha, na nashuhudia ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake hana mshirika; ili kuadhimisha shani yake, na nashuhudia ya kwamba Nabii wetu Muhammad ni mja Wake [Allah] na Mtume wake, swala na salamu nyingi za Allah zimshukie yeye, watu wa nyumba yake na Masahaba wake.

**Enyi Waisilamu:**

Allah ameuhusu mwisho wa mwezi [wa Ramadhani] na Zaka ya Fitri ili iwe tohara kwa waliofunga na lishe kwa maskini, na kiwango chake ni: Pishi [moja] ya chakula cha mjini, mtu huitolea nafsi yake na anaowasimamia, na wakati wa kuitoa unaopendekezwa ni: Kabla ya Swala ya Eid, na inajuzu kuitanguliza kabla ya hapo kwa siku au mbili.

Na inapoisha Ramadhani kwa kuchwa kwa jua la siku ya mwisho, inasisitizwa kuleta Takbira hadi kufika wakati wa Swala ya Eid; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿وَلِتُكۡمِلُواْ ٱلۡعِدَّةَ وَلِتُكَبِّرُواْ ٱللَّهَ عَلَىٰ مَا هَدَىٰكُمۡ وَلَعَلَّكُمۡ تَشۡكُرُونَ﴾

{Na mtimize hiyo hisabu, na mumtukuze Allah kwa kuwa amekuongoeni ili mpate kushukuru}, (Al-Baqarah: 185).

Na «**atakayefunga Ramadhani na akaifuatiza na [kufunga siku] sita za Shawwali, basi ni kama aliyefunga mwaka wote**», imepokewa na Muslim.

Kisha jueni kuwa Allah amewaamrisha kumswalia na kumsalimia Nabii wake...

# HIJA

# SAFARI YA HIJA[1]

Sifa za ukamilifu zote ni za Allah, tunamhimidi, tunamuomba msaada, tunamuomba msamaha, na tunajilinda na Allah kutokana na shari za nafsi zetu, na kutokana na amali zetu mbovu, yule ataongozwa na Allah, basi hakuna wa kumpoteza, na atakayempoteza hakuna wa kumuongoza, nashuhudia ya kwamba hapana apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake, hana mshirika, na nashuhudia kuwa Nabii wetu Muhammad ni mja wake na Mtume wake, swala na salamu za Allah nyingi zimshukie yeye, watu wake, na masahaba wake.

**Ama baada ya himdi hii:**

Basi enyi waja wa Allah mcheni Allah haki ya kumcha, na mchungeni [chungeni amri zake na makatazo yake] katika siri na minong'ono.

**Enyi Waislamu:**

Misimu ya kheri kwa waja ni yenye kufululiza; haiishi ibada ila hujitokeza kwao nyengine. Haya ndio mawimbi ya mahujaji yameelekea katika nyumba kale ya Allah, wakiitikia mbia ya kipenzi cha Allah [Ibrahim] salamu zimshukie,

﴿وَأَذِّن فِي ٱلنَّاسِ بِٱلۡحَجِّ يَأۡتُوكَ رِجَالٗا وَعَلَىٰ كُلِّ ضَامِرٖ يَأۡتِينَ مِن كُلِّ فَجٍّ عَمِيقٖ﴾

{Na watangazie watu Hija; watakujia kwa miguu na juu ya kila ngamia aliyekonda, wakija kutoka katika kila njia ya mbali}. (Al-Hajj: 27).

Ni nyumba ambayo Allah ameijaalia kuwa pahala pa kukusanyikia watu na pahala pa amani. Kingizoni mwake mnatarajiwa kushuka rehema na vipawa kutoka kwa [Allah] Mkarimu. Eneo takatifu lililobarikiwa, ndani yake mna uongofu, kheri nyingi, na alama za dhahiri:

﴿إِنَّ أَوَّلَ بَيۡتٖ وُضِعَ لِلنَّاسِ لَلَّذِي بِبَكَّةَ مُبَارَكٗا وَهُدٗى لِّلۡعَٰلَمِينَ ۞

فِيهِ ءَايَٰتُۢ بَيِّنَٰتٞ مَّقَامُ إِبۡرَٰهِيمَۖ وَمَن دَخَلَهُۥ كَانَ ءَامِنٗاۗ﴾

{Hakika Nyumba ya kwanza walio wekewa watu kwa ibada ni ile iliyoko Bakka [Makkah], iliyobarikiwa na yenye uwongofu kwa

[1] Imetolewa siku ya ijumaa, tarehe tatu mwezi wa 'Dhul-Hijjah', mwaka wa elfu moja mia nne na ishirini na tano hijria, katika Msikiti wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie.

walimwengu wote * Ndani yake zipo Ishara zilizo wazi - masimamio ya Ibrahim -, na mwenye kuingia humo anakuwa katika amani}, ( Al- Imran: 96-97).

Kuihiji ni katika nguzo za Uisilamu; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿وَلِلَّهِ عَلَى ٱلنَّاسِ حِجُّ ٱلۡبَيۡتِ مَنِ ٱسۡتَطَاعَ إِلَيۡهِ سَبِيلٗاۚ

وَمَن كَفَرَ فَإِنَّ ٱللَّهَ غَنِيٌّ عَنِ ٱلۡعَٰلَمِينَ﴾

{Na kwa ajili ya Allah imewajibikia watu wahiji kwenye Nyumba hiyo, kwa yule awezae njia ya kwendea. Na atakayekanusha basi Allah si mhitaji kwa walimwengu}, (Al-Imran: 97).

Sheria imeamrisha kufika katika viwanja vyake ili kutekeleza faradhi ya Dini; [Mtume] swala na salamu zimshukie:

«**Enyi watu! Hakika Allah amefaradhisha juu yenu Hija; basi fanyeni hija**», imepokewa na Muslim.

Kuhiji [nyumba hii] ni katika amali tukufu zaidi mbele ya Allah, mnao ndani yake kutoa [juhudi], uchovu na malipo; Abu Huraira Allah amridhie amesema:

«Nabii swala na salamu za Allah zimshukie aliulizwa: Amali gani ni bora zaidi? Akasema: **Kumuamini Allah na Mtume wake**. Ikasemwa: Kisha ni gani? [Mtume] Akasema: **Jihadi katika njia ya Allah**. Ikasemwa: Kisha ni gani? Akasema: **Hija 'Mabruur'**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Na mnao katika kutekeleza nguzo ya tano ya Uisilamu: kusamehewa madhambi, na kuoshwa uchafu wa makosa na maasi; Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**Atakayehiji na asiseme maneno machafu na asitende maovu; basi atarudi** [kutoka hija yake] **kama siku aliozaliwa na mamake** [akiwa hana dhambi kabisa]», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Na atakayejifunga na uchamngu katika Hija yake, Allah atamuandalia Pepo kuwa mashukio yake, [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

«**Umra hadi Umra ni yenye kufuta [madhambi] yalio baina yake, na Hija 'Mabruur' haina malipo ila Pepo**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea,

An-Nawawi Allah amrehemu amesema: «Malipo ya mwenye kuifanya hayakomeki na [jambo la] kufuta baadhi ya madhambi yake, bali hakuna budi aingie Peponi».

Na amali zinapimwa kwa Ikhlasi, pindi zinapochanganyika na shirki au riya basi hayo huiharibu; [Allah] aliyetukuka na aliye juu amesema:

﴿وَلَقَدۡ أُوحِيَ إِلَيۡكَ وَإِلَى ٱلَّذِينَ مِن قَبۡلِكَ لَئِنۡ أَشۡرَكۡتَ لَيَحۡبَطَنَّ عَمَلُكَ وَلَتَكُونَنَّ مِنَ ٱلۡخَٰسِرِينَ﴾

{Na kwa yakini yamefunuliwa kwako na kwa waliokuwa kabla yako: Bila ya shaka ukimshirikisha Allah amali zako zitaanguka, na lazima utakuwa miongoni mwa wenye kukhasiri}, (Az-Zumar: 65).

na wala hautimii wema wa Hija isipokuwa kwa chumo zuri lililotakasika kutokana na uchafu wa mambo ya haramu na uchafu wa mambo ya utata.

Na usuhuba mwema katika safari ni msaada katika kufanya utiifu na uzuri wa ibada, na utu katika safari ni kutoa [akiba yako ili kusaidia] na kuwa mchache wa kuwahalifu wendani [safarini], na kuwafanyia wema wenzi safarini ni ibada yenye manufaa ya ziada, Mujaahid Allah amrehemu amesema: "Nilisuhubiana na ibnu Umar Allah amridhie katika safari ili ni mhudumie; [badala yake] akawa yeye ndiye anihudumia mimi", ibnu Rajab Allah amrehemu amesema: "Na walikuwa wengi katika 'Salaf' [wema waliotangulia] akishurutiza kwa wendani wake safarini awe yeye ndiye mwenye kuwahudumia, ili wapatilize ujira wa hilo".

Na maandalizi bora atakayobeka hujaji ni: maandalizi ya uchamngu, [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿وَتَزَوَّدُواْ فَإِنَّ خَيۡرَ ٱلزَّادِ ٱلتَّقۡوَىٰ﴾

{Na jichukulieni maandalizi. Na hakika maandalizi bora ni uchamngu}, (Al-Baqarah: 197).

Na miongoni mwa nyasia za Nabii swala na salamu za Allah zimshukie kwa Muadh Allah amridhie:

«**mche Allah popote ulipo, na fuatisha jema baada ya ovu, basi litalifuta, na tangamana na watu kwa tabia njema**», imepokewa na Tirmidhi.

Na ni miongoni mwa wema katika Hija: kulisha chakula, kutoa salamu, maneno mazuri, na kuwaamili watu kwa kuwafanyia ihsani, basi usidharau jema lolote katika Hija yako,

«**Na mtu bora zaidi ni mwenye kuwanufaisha watu zaidi**», na mwenye ushindi zaidi ni msubirifu zaidi wa udhia wao, na mwenye kuhudumia mahujaji kwa akiwa na ikhlasi katika kuwachunga, atakuwa mshirika wao katika ujira na thawabu; [Mtume] swala na salamu zimshukie anasema:

«**Hakika Allah anawaingiza watu watatu Peponi kwa ajili ya chembe kimoja: aliyekitengeneza - akitarajia ujira kwa hilo -, mwenye kukirusha na mwenye kukipeana**», imepokewa na Tirmidhi.

Na aliyesafiri kuielekea Nyumba [Kaaba] anastahiki kujifunga na mambo matatu: uchamngu utakao mzuilia na kumuasi Allah, upole atakaojikinga nao na hasira zake [kukasirika], na usuhuba mwema kwa anayesuhubiana naye.

**Enyi Waislamu:**

Bora zaidi wanayo jikurubisha nayo waja kwa Mola wao Mlezi ni: Kudhihirisha Tawhidi katika ibada zao, na kumtakasia Allah amali zote zenye kuwakurubisha kwake, na zitakazokuwa kwa ajili ya asiyekuwa Allah basi zitafifia; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿وَأَتِمُّوا۟ ٱلْحَجَّ وَٱلْعُمْرَةَ لِلَّهِ﴾

{Na timizeni Hija na Umra kwa ajili ya Allah}. (Al-Baqarah: 196).

Na mnao ndani ya kuidhihirisha ibada [ya Hija] kwa kauli umoja wa Muumba;

«**Labbayka llaahumma labbayk, labbayka laa shariika lak** [ewe Mola! Nakuitikia baada ya kukuitikia. Nakuitikia hauna mshirika nawe]»,

Na [maneno] bora wanayotamka watamkaji siku ya Arafa ni Neno la Tawhidi; [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

«**Dua bora zaidi ni Dua ya siku ya Arafa, na bora zaidi niliyoyasema mimi na Manabii kabla yangu: *'Laa ilaaha illa llaahu wahdahuu laa shariika lah, lahul mulku, walahul hamd, wa huwa alaa kulli shay-in qadiir'*, Hapana apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake hana mshirika naye, ni wake ufalme, ni zake sifa njema zote, Naye ni muweza wa kila kitu**» imepokewa na Tirmidhi.

Na kumtegemea Allah ni katika ibada kubwa zaidi; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿فَٱعْبُدْهُ وَتَوَكَّلْ عَلَيْهِ﴾

{basi muabudu Yeye, na umtegemee Yeye}, (Hud: 123).

Na kukata tamaa si katika Dini ya Allah kabisa; [Allah] aliyetukuka na aliye juu amesema:

﴿إِنَّهُۥ لَا يَا۟يْـَٔسُ مِن رَّوْحِ ٱللَّهِ إِلَّا ٱلْقَوْمُ ٱلْكَـٰفِرُونَ﴾

{Hakika hawakati tamaa na faraji ya Allah isipokuwa watu makafiri}. (Yusuf: 87).

Na hajawahi mtu kutanguliza haki ya Allah mbele ya matamanio ya nafsi yake na raha zake ila ataona saada ya dunia na akhera; Hajar [mamake Nabii Ismail] alikuwa akitafuta maji yake na ya mwanaye wa kunyonya katika bonde lisilo na mimea, baina ya majabali mawili, kiu imemchosha, na huruma ya mwanaye imemlemea, na baada ya kumtegemea Allah na kufanya sababu; alipata chemchemi yenye kububujika, yake yeye na vizazi vya baada yake,

Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**Allah amrehemu mamake Ismail, lau angeyaacha** [maji ya] **Zamzam** [asiyakusanye]; **yangekuwa chemchemi yenye kububujika na kutemebea juu ya ardhi**», imepokewa na Bukhari.

Na manufaa na madhara yamo Mikononi mwa Allah aliyetukuka na aliye juu, Mleta faraja ya majanga, na mwenye kuondosha mazito, aliyenyanyuka juu ya waja wake, Mkononi mwake ndio mna funguo za hazina za mbinguni na ardhini, aliyesifika na kiburi na utukufu, hayo yote hujaji anayatangaza wazi katika ibada zake za hija - katika Twawafu yake, Sa'yi yake na 'ramyil jamaraat', na ndani ya siku ya kuchinja na siku za 'tashriiq' -; ndio moyo ubaki ukiwa umetakasiwa Allah, umefungamana Naye, na uachane na jambo la kufungamana na yalio katika mikono ya viumbe.

Na mnao katika kurusha vijiwe kuwakumbusha wanadamu adui anayewavizia, na kuwaita Motoni, [Allah] mwenye ushindi na utukufu amesema:

﴿إِنَّ ٱلشَّيۡطَٰنَ لَكُمۡ عَدُوّٞ فَٱتَّخِذُوهُ عَدُوًّاۚ إِنَّمَا يَدۡعُواْ حِزۡبَهُۥ لِيَكُونُواْ مِنۡ أَصۡحَٰبِ ٱلسَّعِيرِ﴾

{Hakika Shetani ni adui yenu, basi mfanyeni kuwa ni adui. Kwani yeye analiita kundi lake liwe katika watu wa Motoni} (Fatwir: 6).

Basi kuwa na hadhari ya kufanya upungufu katika wajibu, au kuingia katika maasi, yatakayo kuingiza katika maangamivu.

Jua kuwa vipindi vya Hija ni vitukufu, na masaa yake ni yenye thamani, [Allah] mwenye ushindi na utukufu amesema:

﴿وَٱذۡكُرُواْ ٱللَّهَ فِيٓ أَيَّامٖ مَّعۡدُودَٰتٖ﴾

{Na mtajeni Allah katika zile siku zinazo hisabiwa}; (Al-Baqarah: 203).

Basi kimbilia katika kila kheri na yenye kukukurubisha kwa Allah ndani yake [Hija], miongoni mwa Dhikri, Istighfari, Takbira, na kusoma Qur-ani; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿فَإِذَآ أَفَضۡتُم مِّنۡ عَرَفَٰتٖ فَٱذۡكُرُواْ ٱللَّهَ عِندَ ٱلۡمَشۡعَرِ ٱلۡحَرَامِۖ وَٱذۡكُرُوهُ كَمَا هَدَىٰكُمۡ﴾

{Na mtakapo miminika kutoka ‘Arafat, basi mtajeni Allah penye Mash'aril Haram. Na mkumbukeni kama alivyo kuongoeni}. (Al-Baqarah: 198).

Na baada ya kumalizika ibada za Hija: Mhimidi Allah kwa uongofu aliokupa, na mshukuru kwa Ibada aliokuezesha:

﴿فَإِذَا قَضَيۡتُم مَّنَٰسِكَكُمۡ فَٱذۡكُرُواْ ٱللَّهَ كَذِكۡرِكُمۡ ءَابَآءَكُمۡ أَوۡ أَشَدَّ ذِكۡرٗا﴾

{Na mkishatimiza ibada zenu basi mtajeni Allah kama mlivyokuwa mkiwataja baba zenu au mtajeni zaidi}. (Al-Baqarah: 200).

Na katikati ya ibada za Hija: mna kuomba msamaha, na kurejea kwa Allah; [Allah] mwenye ushindi na utukufu amesema:

﴿ثُمَّ أَفِيضُواْ مِنۡ حَيۡثُ أَفَاضَ ٱلنَّاسُ وَٱسۡتَغۡفِرُواْ ٱللَّهَۚ إِنَّ ٱللَّهَ غَفُورٞ رَّحِيمٞ﴾

{Kisha miminikeni kutoka pale wanapomiminika watu, na muombeni Allah msamaha: hakika Allah ni Mwenye kusamehe Mwenye kurehemu} (Al-Baqarah: 199).

Sheikhul Islaam Allah amrehemu amesema: "Istighfari ni miongoni mwa mema makubwa zaidi, na ni mlango mpana, basi atakayehisi upungufu katika kauli yake, amali yake, hali yake, riziki yake au kugeuka kwa moyo; basi ni juu yake kushikana na Tawhidi na Istighfari, kwani ndani yake mna ponyo pindi zitatekelezwa kwa ukweli na ikhlasi".

Na waja katika Hija wanakuwa kwa kiwango cha hima zao, miongoni mwao mna wanaotafuta pato la dunia la haraka, na miongoni mwao mna wanaotafuta Radhi za Allah na nyumba ya mwisho [Pepo], [Allah] aliyetasika amesema:

﴿فَمِنَ ٱلنَّاسِ مَن يَقُولُ رَبَّنَآ ءَاتِنَا فِي ٱلدُّنۡيَا وَمَا لَهُۥ فِي ٱلۡأٓخِرَةِ مِنۡ خَلَٰقٖ﴾

{Na wapo baadhi ya watu wanaosema: Mola wetu Mlezi, tupe duniani! Naye katika Akhera hana sehemu yoyote}. (Al-Baqarah: 200).

Na aliyeafikiwa ni yule aliyetekeleza Hija yake kwa nia njema ya ikhlasi, na kwa matumizi mazuri [yalitokana na pato la halali], na akaupamba ulimi wake kwa kumtaja Allah, na akaiambatanisha ibada yake na ihsani na kunufaisha viumbe; basi kuweni hivyo katika Hija zenu, itakaseni Dini yenu kwa Allah, jitahidini katika amali njema na shindaneni katika Pepo za Mola wenu Mlezi.

***'Audhu billaahi mina sh-shaitwaani rrajiim'***

﴿ٱلۡحَجُّ أَشۡهُرٞ مَّعۡلُومَٰتٞۚ فَمَن فَرَضَ فِيهِنَّ ٱلۡحَجَّ فَلَا رَفَثَ وَلَا فُسُوقَ وَلَا جِدَالَ فِي ٱلۡحَجِّۗ
وَمَا تَفۡعَلُواْ مِنۡ خَيۡرٖ يَعۡلَمۡهُ ٱللَّهُۗ وَتَزَوَّدُواْ فَإِنَّ خَيۡرَ ٱلزَّادِ ٱلتَّقۡوَىٰۖ وَٱتَّقُونِ يَـٰٓأُوْلِي ٱلۡأَلۡبَٰبِ﴾

{Hija ni miezi maalumu. Na anayekusudia kufanya Hija katika miezi hiyo, basi asiseme maneno machafu wala asifanye vitendo vichafu wala asibishane katika Hija. Na kheri yoyote mnayo ifanya Allah anaijua. Na jitengezeeni maandalizi. Na hakika bora ya maandalizi ni uchamngu. Na nicheni Mimi, enyi wenye akili!}. (Al-Baqarah: 197).

Allah anibarikie mimi na nyinyi katika Qur’ani tukufu...

## HOTUBA YA PILI

Sifa njema zote anastahili Allah kwa wema Wake [kwetu], na shukrani zote anastahili Yeye kwa kutuafikia na kutuneemesha, na nashuhudia ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake hana mshirika; ili kuadhimisha shani yake, na nashuhudia ya kwamba Nabii wetu Muhammad ni mja Wake [Allah] na Mtume wake, swala na salamu nyingi za Allah zimshukie yeye, watu wa nyumba yake na Masahaba wake.

**Ama baada ya himdi hii, enyi Waislamu:**

Mumeingiliwa na siku kumi zilizobarikiwa, amali zifanywazo ndani yake ni bora zaidi, Nabii swala na salamu za Allah zimshukie anasema:

«**Hakuna siku zozote amali njema ndani yake zinapendeza zaidi kwa Allah kuliko siku hizi** - yaani siku kumi [za Dhul Hijjah] -, wakasema: Ewe Mtume wa Allah! Hata Jihadi katika njia ya Allah? [Mtume] Akasema: **Hata Jihadi katika njia ya Allah, ila mtu aliyetoka kwa nafsi yake na mali yake, na asirudi na chochote katika hayo**», imepokewa na Abu Daaud;

Basi kithirisheni ndani yake [kumi la Dhul Hijjah] Takbira, kumhimidi Allah, kusoma Qur-ani, kuunga kizazi, Sadaka, kuwatenda wema wazazi wawili, kufariji [wenye] majanga, kukidhi haja [za wahitaji], na ibada zilizosalia, sheikhul Islaam Allah amrehemu amesema: "Michana ya kumi la Dhul Hijjah ni bora kuliko michana ya kumi [la mwisho] la Ramadhani, na usiku kumi za mwisho la Ramadhani ni bora kuliko usiku za kumi la Dhul-hijjah".

Walikuwa Masahaba ndani ya kumi [la Dhul-hijjah] wakihuisha sunnah ya Takbira baina ya watu; «Ibnu Umar na Abu Huraira Allah awaridhie walikuwa wakitoka katika siku za kumi hili kuenda sokoni, wakileta Takbira, na watu wakileta Takbira kwa kusikia Takbira zao», imepokewa na Bukhari.

Na katika kumi hili kheri inafuatana, kwa kuchinja wanyama wa Udh-hiya siku ya Eid na siku za Tashriiq, Na «Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alichinja Udh-hiya wa kondoo wawili wa kiume, wa rangi nyeupe iliochangamana na weusi, wenye pembe; aliwachinja kwa mkono wake, na akasema 'bismi llaah' na akapiga takbira», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Na wanyama bora kwa Udh-hiya: ni walio ghali zaidi kithamani, na walio bora zaidi kwa wamiliki wao, na mbuzi mmoja anamtosheleza mtu na familia yake, na ni haramu kwa mwenye kuchinja Udh-hiya - ndani ya kumi hili - kukata chochote katika nyele zake, au kucha zake, au ngozi yake, hadi achinje.

Basi kuweni na nafsi tulivu yenye kufurahia jambo hili [Udh-hiya], kuleni, lisheni na toeni Sadaka, na tafuteni kwa Sadaka zenu mafakiri, na tafuteni vizazi vyenu na jirani zenu kwa zawadi zenu kutokana na huo [Udh-hiya], na zilindeni Eid zenu kutokana na yenye kumghadhibisha Muumba wenu, na shirikianeni na mahujaji katika Dua, Tahlili na Takbira.

Na aliyebaki mjini kwake na akatanguliwa mahujaji katika viwanja vya hija; ni sheria kwake kufunga siku ya Arafa; [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

«**Saumu ya siku ya Arafa, naitarajia kwa Allah ifute madhambi ya mwaka wa kabla yake na mwaka wa baada**», imepokewa na Muslim.

Basi ipatilizeni misimu ya ibada kabla ya kuisha kwake, kwani uhai ni ghanima, na siku ni za kuhesabika, na umri ni mfupi.

Kisha jueni kuwa Allah amewaamrisha kumswalia na kumsalimia Nabii wake …

# MALENGO YA HIJA[1]

Sifa za ukamilifu zote ni za Allah, tunamhimidi, tunamuomba msaada, tunamuomba msamaha, na tunajilinda na Allah kutokana na shari za nafsi zetu, na kutokana na amali zetu mbovu, yule ataongozwa na Allah, basi hakuna wa kumpoteza, na atakayempoteza hakuna wa kumuongoza, nashuhudia ya kwamba hapana apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake, hana mshirika, na nashuhudia kuwa Nabii wetu Muhammad ni mja wake na Mtume wake, swala na salamu za Allah nyingi zimshukie yeye, watu wake, na masahaba wake.

**Ama baada ya himdi hii:**

Basi enyi waja wa Allah mcheni Allah haki ya kumcha, na mchungeni [chungeni amri zake na makatazo yake] katika siri na minong'ono.

**Enyi Waislamu:**

Allah anawafululizia viumbe vyake misimu ya ibada; ili waoshe ndani yake uchafu wao, na daraja zao zinyayuke ndani yake, na nguzo kati ya nguzo za Uisilamu ambayo Allah ameapa na wakati inayotekelezwa ndani yake:

﴿وَلَيَالٍ عَشْرٍ﴾

{na [naapa] naapa kwa masiku kumi}, (Al-Fajr:2).

Na ameapa na sehemu inayotekelezwa ndani yake; akasema:

﴿لَآ أُقۡسِمُ بِهَٰذَا ٱلۡبَلَدِ﴾

{Naapa kwa Mji huu!}, (Al-Balad: 1-2).

Ibnu Kathiir Allah amrehemu amesema: "Hichi ni kiapo kutoka kwa Allah, anaapa na Makkah mama wa vijiji, katika hali ya kuwa msafiri ameshukia ndani yake; ili atanabahishe juu ya utukufu wa cheo chake katika hali ya kuwemo watu wake ndani ya ihramu",

Nayo [Hija] ni miongoni mwa amali bora zaidi mbele ya Allah, Nabii swala na salamu za Allah zimshukie aliulizwa:

«Ni amali gani ndio bora zaidi? Akasema: Kumuamini Allah na Mtume wake. Ikasemwa: Kisha ni gani? [Mtume] Akasema: **Jihadi katika njia ya**

[1] Imetolewa siku ya ijumaa, tarehe sita, mwezi wa Dhul-hijjah, mwaka elfu moja mia nne na thalathini na nne hijria, katika Msikiti wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie.

**Allah**. Ikasemwa: Kisha ni gani? Akasema**: Hija 'Mabruur'**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Ibnu Battwaal Allah amrehemu amesema: "Uisilamu unapodhihiri na kuenea, na ikawa Jihadi ni faradhi ya kutoshelezana juu ya atakayesimama kuitekeleza; basi Hija wakati huo ni bora zaidi",

Na katika siku miongoni mwa siku zake [Hija], Allah anajigamba na mahujaji wa nyumba yake mbele ya wanaoishi mbinguni; [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

«**Hakuna siku ambayo hupatikana kwa wingi ndani yake Allah kuacha huru mja na Moto kuliko siku ya Arafa, na hakika Yeye hukurubia, kisha hujigamba nao** [watu walio katika uwanja Arafa] **kwa Malaika, akisema: wanataka nini hawa?**», imepokewa na Muslim.

Kuitekeleza kwake kunaosha madhambi na makosa, [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

«**Atakayehiji nyumba hii, asiseme machafu wala asitende machafu; atarudi akiwa kama siku aliozaliwa na mamake** [yaani: akiwa hana dhambi kabisa]», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea,

Ibnu Hajar Allah amrehemu amesema: "na dhahiri yake [hadithi hii]: ni kufuta madhambi madogo, makubwa na yanayoandama hayo", na kwa Hija maovu na madhambi yanavunjwa, [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

«**kwani haukujua kuwa Uislamu unavunja [madhambi] yaliokuwa kabla yake?! Na kuwa Hijra inavunja yaliokuwa kabla yake?! Na kuwa Hija inavunja yaliokuwa kabla yake?!**», imepokewa na Muslim.

An-Nawawi amesema: "yaani: inayaporomosha na inafuta athari zake".

Ni nguzo iliyojaa mafunzo na mazingatio, lengo kubwa zaidi ndani yake ni: kumfanyia Allah Tawhidi na Kumpwekesha kwa ibada. Kuingia ndani yake ni kwa kutangaza Tawhidi na kujitakasa kutokana na Shirki: «***Labbayka llahumma labbyka, labbayka laa shariika lak***»; na Kaaba imejengwa ili kudhihirisha Tawhidi na kujitakasa na Shirki:

﴿وَإِذۡ بَوَّأۡنَا لِإِبۡرَٰهِيمَ مَكَانَ ٱلۡبَيۡتِ أَن لَّا تُشۡرِكۡ بِي شَيۡـٔٗا وَطَهِّرۡ بَيۡتِيَ لِلطَّآئِفِينَ وَٱلۡقَآئِمِينَ وَٱلرُّكَّعِ ٱلسُّجُودِ﴾

{Na pale tulipomweka Ibrahim pahala penye ile Nyumba tukamwambia: Usinishirikishe na chochote; na isafishe Nyumba yangu [kutokana Shirki na maasi] kwa ajili ya wanaoizunguka kwa kutufu, na wanao kaa hapo kwa ibada, na wanaorukuu, na wanaosujudu}, (Al-Hajj: 26).

Na Tawhidi inapodhihiri katika miji; amani inashuka ndani yake, [Allah]

aliyetukuka amesema:

﴿وَإِذۡ جَعَلۡنَا ٱلۡبَيۡتَ مَثَابَةً لِّلنَّاسِ وَأَمۡنًا﴾

{Na kumbukeni tulipoifanya ile Nyumba (ya Alkaaba) iwe pahala pa kukusanyikia watu na pahala pa amani}, (Al-Baqarah: 125).

Ndani ya Hija inadhihiri Imani ya Mitume na mapenzi yao yanazidi nguvu. Na kuchinja, kurusha vijiwe, na Twawafu, ni sunnah ya baba yetu Ibrahim salamu zimshukie.

Na Dua ndio ibada yenyewe, na Dua za hujaji zinatarajiwa kuitikiwa, na Dua za kipenzi cha Allah Ibrahim salamu zimshukie za kuomba amali zikubaliwe, kuthibiti juu ya Uisilamu, kuonyeshwa ibada za Hija, na kutumilizwe Mtume Makkah atakayewasomea aya za Allah na awafundishe Kitabu na Hekima, na iwe Makkah mji wenye amani, na riziki ndani yake iwe yenye kutiririka, na watu waipende, na kuwa aepushwe Yeye na wanawe ibada za masanamu, na awe Yeye na kizazi chake wenye kusimamisha Swala, na kujiombea kwake msamaha wa nafsi yake na Waumini kwa jumla, yote hayo yalikuwa katika nyumba ya Allah tukufu.

Na Dua za Nabii swala na salamu za Allah zimshukie ziko aina tofauti katika sehemu za Hija yake - kama vile siku ya Arafa -, na juu ya Swafaa na Marwa. Na hujaji atakiwa kupatiliza katika Hija yake jambo la kukithirisha Dua kwa akiwaiga Manabii.

Na kumtegemea Allah ni moja wapo wa nguzo mbili za ibada. Ibrahim salamu zimshukie aliijenga Kaaba akimtegemea Allah:

﴿رَّبَّنَآ إِنِّيٓ أَسۡكَنتُ مِن ذُرِّيَّتِي بِوَادٍ غَيۡرِ ذِي زَرۡعٍ عِندَ بَيۡتِكَ ٱلۡمُحَرَّمِ﴾

{Mola wetu Mlezi! Hakika mimi nimewaweka baadhi ya dhuriya zangu katika bonde lisilokuwa na mimea, kwenye Nyumba yako Takatifu}; (Ibrahim: 37).

Watu wakaona matunda ya kumtegemea kwake Allah:

﴿فَٱجۡعَلۡ أَفۡـِٔدَةً مِّنَ ٱلنَّاسِ تَهۡوِيٓ إِلَيۡهِمۡ﴾

{Basi zijaalie nyoyo za watu zielekee kwao}, (Ibrahim: 37).

mnao katika kukusanyika watu katika sehemu moja ukumbusho wa fadhila ya Umma huu na utukufu wa Dini yake.

Mnao ndani ya Hija kukitisha itikadi ya **'al-wala-i wal bara-i'**; Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alimwamrisha Ali ibnu Abii Twaalib anadi katika msimu wa Hija:

«**Baada ya mwaka huu asifanye Hija mshirikina yeyote**», imepokewa na Bukhari,

Na mnao ndani yake [Hija] kuwahalifu makafiri katika ibada zao za kijahilia – miongoni mwa Talbiya, wakati wa kuondoka Muzdalifah, na wingi wa kumdhukuru Allah pekee baada ya kumalizika ibada za Hija -, ibnul Qayyim Allah amrehemu amesema: "Sheria imestakiri juu ya kuwahalifu washirikina, hasahasa ndani ya ibada za Hija".

Hija ni ibada ya kimwili iliyo ndefu zaidi na iliyo na undani zaidi katika Uislamu, na ibada zilizo ndani yake ni aina tofauti - miongoni mwa Talbiya, Twawafu, Sa'a-yi, kulala [Muzdalifah na Minaa], kurusha vijiwe, kunyoa, na kuchinja -, na kuziadhimisha ibada ndani yake. Na kukamilisha kuabudu ndani yake ni katika uchaji wa nyoyo, ibnul Qayyim Allah amrehemu amesema: "Na roho ya ibada ni: Kutukuza na kupenda, pindi moja wapo litakosekana basi [ibada] itaharibika".

Mnao ndani ibada za Hija kusisitiza jambo la kuiandaa nafsi kwa kusubiri katika utiifu, Aisha Allah amridhie amesema:

«Tunaona kuwa Jihadi ni amali bora zaidi, basi [nasi wanawake] si tupigane Jihadi? [Mtume] akasema**: Hapana, lakini Jihadi bora zaidi ni: Hija ilio mabruur** [iliyotekelezwa vyema]», imepokewa na na Bukhari.

Na ni miongoni mwa wajibu wa kujisalimisha kwa Allah: jambo la kumuitikia Allah - hata kama hekima ya lililoamrishwa haijadhihiri -, Allah alisema kumuambia [Nabii] Ibrahim salamu zimshukie:

﴿وَأَذِّن فِي ٱلنَّاسِ بِٱلۡحَجِّ يَأۡتُوكَ رِجَالٗا﴾

{Na watangazie watu Hija; watakujia kwa miguu}, . (Al-Hajj:27).

Basi akaitikia amri ya Allah na akaitangaza Hija, na watu wakaijia nyumba ya Allah tukufu, hali ya kuwa nafsi zao zina shauku nayo, zikitoa katika safari mali na hali ziko na furaha na bishara, ibnu Kathiir amesema: "Hakuna yeyote katika Waisilamu ila ana shauku ya kuiona Kaaba na kutufu, na watu wanaijia kutoka pande zote na miji yote".

Ni nguzo inayohakikisha jambo la kuandama na kutekeleza amri za Nabii swala na salamu za Allah zimshukie, Umar ibnul Khatwaab Allah amridhie amesema - kuhusu Jiwe leusi -: «Wallahi mimi najua kuwa wewe ni jiwe, haudhuru wala haunufaishi, na lau isingekuwa nimemuona Nabii swala na salamu za Allah zimshukie akikubusu, basi singekubusu», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Na ibada zimejengewa juu ya kufuata, wala hakuna nafasi ya uzushi ndani yake; basi Twawafu na Sa'ayi ni mizunguko saba, na hekima katika idadi yake imefichamana katika akili, ndio Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**chukueni** [someni] **ibada zenu kutoka kwangu**», imepokewa na Muslim,

Na Allah hakuamrisha Twawafu ila katika Kaaba, na kufanya Twawafu kwengine ni maangamivu.

Na wakati kwa Muisilamu ni wenye thamani sana, na inao kila siku katika Hija ibada inayo tofautiana na mwenzake, na kila mojawapo ina wakati unapoisha nayo inaisha; basi kuondoka Arafa ni baada ya kuchwa jua, na mda wa 'mabiit' unaisha kwa kuchomoza jua, na kutovaa nguo za mshono kunakumbusha kukurubia mda wa kuvaa sanda, Allah alileta mwishoni mwa aya za Hija [kauli yake]:

﴿وَٱتَّقُواْ ٱللَّهَ وَٱعۡلَمُوٓاْ أَنَّكُمۡ إِلَيۡهِ تُحۡشَرُونَ﴾

{Na mcheni Allah, na jueni kwamba nyinyi mtakusanywa kwake}, (Al-Baqarah: 203).

ili kuwakumbusha hilo.

Na kutafautiana vyeo vya watu ni kwa uchamngu, na kuupata [uchamngu] katika Hija ndio ghanima bora zaidi,

﴿وَتَزَوَّدُواْ فَإِنَّ خَيۡرَ ٱلزَّادِ ٱلتَّقۡوَىٰ﴾

{Na jitengezeeni maandalizi. Na hakika bora ya maandalizi ni uchamngu}, (Al-Baqarah: 197).

Na nyoyo hupata uhai kwa kumdhukuru Allah, na Allah ameamrisha kukithirisha kumdhukuru Yeye aliyetukuka katika siku zote za Hija, akasema:

﴿وَٱذۡكُرُواْ ٱللَّهَ فِيٓ أَيَّامٖ مَّعۡدُودَٰتٖ﴾

{Na mtajeni Allah katika zile siku zinazohisabiwa}, (Al-Baqarah: 203).

Na [Allah] aliyetukuka alihusu sehemu zinazo kithirishwa ndani yake kumdhukuru Yeye; akasema:

﴿فَإِذَآ أَفَضۡتُم مِّنۡ عَرَفَٰتٖ فَٱذۡكُرُواْ ٱللَّهَ عِندَ ٱلۡمَشۡعَرِ ٱلۡحَرَامِۖ وَٱذۡكُرُوهُ كَمَا هَدَىٰكُمۡ﴾

{Na mtakapo miminika kutoka A'rafat mtajeni Allah penye Masha'ril Haram. Na mkumbukeni kama alivyo kuongoeni}, (Al-Baqarah: 198).

Na akasema:

﴿ثُمَّ أَفِيضُواْ مِنۡ حَيۡثُ أَفَاضَ ٱلنَّاسُ وَٱسۡتَغۡفِرُواْ ٱللَّهَ﴾

{Kisha miminikeni kutoka pale wanapomiminika watu, na muombeni Allah msamaha}. ." (Al-Baqarah: 199).

Na Allah amemuamrisha hujaji anapomaliza ibada zake kukithirisha kumdhukuru, akasema;

﴿فَإِذَا قَضَيۡتُم مَّنَٰسِكَكُمۡ فَٱذۡكُرُواْ ٱللَّهَ كَذِكۡرِكُمۡ ءَابَآءَكُمۡ أَوۡ أَشَدَّ ذِكۡرٗا﴾

{Na mkishatimiza ibada zenu basi mtajeni Allah kama mlivyokuwa mkiwataja baba zenu au mtajeni zaidi}, (Al-Baqarah: 200).

Na [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

«**Hakika si mengine, imewekwa Twawafu katika Kaaba na baina Swafaa na Marwa, na kurusha vijiwe; kwa ajili ya kusimamisha Dhikri ya Allah mwenye ushindi na utukufu**», imepokewa na Ahmad.

Mnao katika Hija kukitisha sifa na tabia njema, na kuhimiza kila kheri, [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿فَمَن فَرَضَ فِيهِنَّ ٱلۡحَجَّ فَلَا رَفَثَ وَلَا فُسُوقَ وَلَا جِدَالَ فِي ٱلۡحَجِّۗ وَمَا تَفۡعَلُواْ مِنۡ خَيۡرٖ يَعۡلَمۡهُ ٱللَّهُ﴾

{Na anayekusudia kufanya Hija katika miezi hiyo, basi asiseme maneno machafu wala asifanye vitendo vichafu wala asibishane katika Hija. Na kheri yoyote mnayoifanya Allah anaijua} (Al-Baqarah: 197).

.Na mnao ndani yake kukitisha msingi wa undugu, na kubadilishana manufaa ya kidini na kidunia; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿لِّيَشۡهَدُواْ مَنَٰفِعَ لَهُمۡ﴾

{Ili washuhudie manufaa yao}, (Al-Hajj: 28).

Al-Qurtubi Allah amrehemu amesema: "Manufaa yao miongoni mwa: ibada, biashara, msamaha, na manufaa ya dunia na akhera", na mnao katika ibada zake uwiyano wa jamii na kushikana kwake; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿فَكُلُواْ مِنۡهَا وَأَطۡعِمُواْ ٱلۡبَآئِسَ ٱلۡفَقِيرَ﴾

{Basi kuleni katika hao na mlisheni mwenye shida aliye fukara}. (Al-Hajj: 28).

**Na baada ya haya, enyi Waisilamu:**

Matunda ya Hija ni kufuzu kupata Pepo ya neema, [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

«**Hija 'Mabruur' haina malipo ila Pepo**», wameafikiana Bukhari na

Muslim kuipokea,

Basi ana Pepo aliye hiji nyumba ya Allah tukufu, akiwa ameitakasa niya yake kwa Allah, na katika ibada yake amemuiga Nabii swala na salamu za Allah zimshukie, akitarajia thawabu za Allah na Siku ya mwisho.

***'Audhu billaahi mina sh-shaitwaani rrajiim'***

﴿إِنَّ ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ وَعَمِلُواْ ٱلصَّـٰلِحَـٰتِ كَانَتۡ لَهُمۡ جَنَّـٰتُ ٱلۡفِرۡدَوۡسِ نُزُلًا﴾

{Hakika wale walio amini na wakatenda mema mashukio yao yatakuwa kwenye Pepo za Firdausi}. (Al-Kahf: 107).

Allah anibarikie mimi na nyinyi katika Qur’ani tukufu...

## HOTUBA YA PILI

Sifa njema zote anastahili Allah kwa wema Wake [kwetu], na shukrani zote anastahili Yeye kwa kutuafikia na kutuneemesha, na nashuhudia ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake hana mshirika; ili kuadhimisha shani yake, na nashuhudia ya kwamba Nabii wetu Muhammad ni mja Wake [Allah] na Mtume wake, swala na salamu nyingi za Allah zimshukie yeye, watu wa nyumba yake na Masahaba wake.

**Enyi Waislamu:**

Allah aliye na ushindi na utukufu ni mwenye upole kwa waja wake, basi asiyeweza kuhiji nyumba yake ya kale amemuwekea kuwashiriki mahujaji kwa Dhikri na Takbira ndani ya kumi hili liliobarikiwa, na Saumu ya Arafa kwa wasiokuwa mahujaji inafuta madhambi, [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

«**Saumu ya siku ya Arafa, naitarajia kwa Allah ifute madhambi ya mwaka wa kabla yake na mwaka wa baada**», imepokewa na Muslim.

Na siku za Waislamu ni siku za furaha, na Allah aliuamrisha Umma huu kudhirisha furaha kwa ibada baada ya kutekeleza nguzo mbili za Uislamu; kuna Eid baada ya Saumu ya Ramadhani, na Eid ya pili baada ya siku ya Arafa, na Allah ameamrisha ndani yake kula, kunywa na kumtaja Yeye aliyetakasika; [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

«**Siku za 'Tashriiq', ni siku za kula, kunywa na kumtaja Allah**», imepokewa na Muslim,

Cheo cha [ibada ya] kumtaja Allah kinanyanyuka pindi watu wanaghafilika na furaha zao, au wanashughulika na starehe zao. Siku ya Eid iliyobora zaidi ni iliyokuwa jambo la kumtaja Allah ndani yake limedhihiri zaidi.

Kisha jueni kuwa Allah amewaamrisha kumswalia na kumsalimia Nabii wake...

# IBADA NDEFU ZAIDI YA KIMWILI: HIJA[1]

Sifa za ukamilifu zote ni za Allah, tunamhimidi, tunamuomba msaada, tunamuomba msamaha, na tunajilinda na Allah kutokana na shari za nafsi zetu, na kutokana na amali zetu mbovu, yule ataongozwa na Allah, basi hakuna wa kumpoteza, na atakayempoteza hakuna wa kumuongoza, nashuhudia ya kwamba hapana apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake, hana mshirika, na nashuhudia kuwa Nabii wetu Muhammad ni mja wake na Mtume wake, swala na salamu za Allah nyingi zimshukie yeye, watu wake, na masahaba wake.

**Ama baada ya himdi hii:**

Basi enyi waja wa Allah mcheni Allah haki ya kumcha, na mchungeni [chungeni amri zake na makatazo yake] katika siri na minong'ono.

**Enyi Waislamu:**

Allah aliyetakasika ndiye Mkwasi Mwenye nguvu, na wasiokuwa Yeye wote ni mafakiri kwake na ni wenye kumuhitaji Yeye; basi hakuumba viumbe ili kupata wingi nao, wala kutia nguvu utukufu wake, bali amewaumba kwa hekima adhimu, nayo ni: kumuabudu Yeye, nao wapata saada kwa kumuabudu Yeye.

Na kwa fadhila na rehema zake kwa waja ndio amewaamrisha amali na kauli watakazo jikurubisha nazo kwake; ujira wao uzidi, na haja zao kwake zitekelezwe,

Naye aliyetakasika alifadhilisha baina ibada zake, akajaalia [ibada ya] kutekelezaTawhidi na kuifanyia kazi, na kuepuka yenye kuivunja ni amali tukufu zaidi kati ya amali anazozipenda Allah, na akajaalia jambo la kuidhihirisha amali hii kikauli ndio kauli takatifu zaidi kwake; [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

«**Maneno yapendezayo zaidi kwa Allah ni manne: *'subhaana llaah, wal hamdu lillaah, wa laa ilaaha illa llaahu, wallahu akbar***», imepokewa na Muslim; bali [Allah] aliyetakasika amejaalia kumfanyia Yeye Tawhidi ni sharti moja la kukubaliwa amali njema, na endapo sharti hili litavunjika, mja

[1] Imetolewa siku ya ijumaa, tarehe moja, mwezi wa Dhul-hijjah, mwaka elfu moja mia nne na thalathini na mbili hijria, katika Msikiti wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie.

hatanufaika na amali yake, atarudishiwa mwenyewe, [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿وَلَقَدۡ أُوحِيَ إِلَيۡكَ وَإِلَى ٱلَّذِينَ مِن قَبۡلِكَ لَئِنۡ أَشۡرَكۡتَ لَيَحۡبَطَنَّ عَمَلُكَ وَلَتَكُونَنَّ مِنَ ٱلۡخَٰسِرِينَ﴾

{Na kwa yakini yamefunuliwa kwako na kwa waliokuwa kabla yako: Bila ya shaka ukimshirikisha Allah amali zako zitaanguka, na lazima utakuwa miongoni mwa wenye kukhasiri} (Az-Zumar: 65)..

Na ili kuhakikisha msingi wa Dini na kuudhihirisha katika maneno ya waja na matendo; Allah ameweka ibada na amali njema tofuti tofauti, apate kuadhimishwa Mola mlezi katika kila kipindi, basi haukomi msimu ila hufuatia msimu mwingine, wanadhihirisha ndani yake kumfanyia [Allah] Tawhidi na kujidhalilisha kwake;

Kwa ajili hiyo, Allah aliyetakasika akaamrisha ibada ya kimwili ndefu zaidi na yenye kufuatana, waja wanachangamana nayo masiku kadhaa ili kudhihirisha kumpwekesha Allah pekee kwa ibada, na kuwa kuabudiwa kwa wengine ni batili, na ili itakasike kwayo miili yao na mali yao, na zitwahirike kwayo nyoyo zao na midomo yao, basi atakayezitekeleza kama alivyoamrisha Allah, zitarudi nyaraka za amali yake kuwa bila ya uchafu wala madhambi, [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

«**Atakayeijia nyumba hii, kisha asiseme machafu wala asitende maovu; atarudi kama siku aliyozaliwa na mamake**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Na hujaji akiwa ndani ya ibada hii huwa katika vipindi vya rehema za Mola wake Mlezi akiwa ndani ya sehemu tukufu, na ndani ya siku ambayo ndio siku inayokithiri zaidi ndani yake kuachwa huru na Moto; Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**Hakuna siku ambayo hupatikana kwa wingi ndani yake Allah kuacha huru mja na Moto kuliko siku ya Arafa, na hakika Yeye hukurubia, kisha hujigamba nao** [watu walio katika uwanja Arafa] **kwa Malaika, akisema: wanataka nini hawa?**», imepokewa na Muslim.

Na atakayeihifadhi Hija yake na yale aliyoyaharamisha Allah, basi Allah amemuahidi Pepo; [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

«**Hija 'Mabruur' haina malipo ila Pepo**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Hija ni nguzo miongoni mwa nguzo za Dini, iliojaa manufaa na mazingatio, [Allah] aliyetakasika ameamrisha kuitekeleza katika sehemu ilio twahara na tukufu zaidi; ili akusanye pamoja baina ya utukufu wa amali

na wa sehemu. Kipenzi cha Allah [Ibrahim salamu zimshukie] alijenga ndani yake nyumba ya Allah, na aliiasisi juu ya uchamngu na ikhlasi, na [Allah] alibakisha aliyojenga Ibrahim salamu zimshukie ili waja waone kuwa haibakii amali ila ile iliotakasiwa Uso wa Allah.

Na mahujaji wanaanza ibada zao kwa kudhihirisha Tawhidi kwa Allah pekee, na kuzikana ibada za wengine: «***Labbayka llaahumma labbayk, labbayka laa shariika lak***».

Na *'Shahadatu Anna Muhammadan rasuulu llah'* haitimii ila kwa kumtii Nabii swala na salamu za Allah zimshukie, na kufuata athari zake. Na kubusu Jiwe leusi ni mfumo [manhaji] katika ibada na kufuata [kumfuata Mtume swala na salamu za Allah zimshukie], basi kulibusu ni ibada [kwa Allah, yaani: kumtii Yeye alipoamrisha hilo] wala si kwa kutaka baraka kutoka kwenye jiwe, kwani halinufaishi wala halidhuru;

Umar Allah amridhie alikuja katika Jiwe [leusi] akalibusu na akasema: «Wallahi mimi najua kuwa wewe ni jiwe, haudhuru wala haunufaishi, na lau isingekuwa nimemuona Nabii swala na salamu za Allah zimshukie akikubusu, basi singekubusu», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Na mnao katika hali ya ihramu kuilingania nafsi katika kuiasi hawaa [matamanio ya nafsi] - hakuna kuvaa nguo ya mshono, wala kugusa manukato, wala kukata kucha, wala kuposa -.

Na weusi wa Jiwe leusi unawakumbusha waja uovu wa maasi hata kwa visivyo na roho, na kuwa athari yake katika moyo ni kubwa zaidi; [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

«**Jiwe leusi lilishuka kutoka Peponi hali yakuwa ni leupe kuliko maziwa; basi likafanywa leusi na makosa ya wanadamu**», imepokewa na na Tirmidhi.

Na hujaji anaona athari ya maasi kwa muasi, kwani iblisi alimdhihirikia Ibrahim salamu zimshukie mara tatu, ili amzuilie kutekeleza amri ya Mola wake Mlezi ya kumchinja mwanaye Ismail, basi kipenzi cha Allah akampiga na jiwe, ili kumdunisha na kumdhihirishia uadui, na kule [iblisi] kujitokeza mara kwa mara kwa kipenzi cha Allah ni ukumbusho kwetu kutoka kwa Allah kuwa iblisi hukariri wasiwasi wake kwa mwanadamu, tena sehemu mbali mbali.

Hija ni tangazo la kuwa Uislamu ndio Dini ya haki, basi hutaona waja wakikusanyika kutoka maeneo ya ardhi, kwa tofauti ya jinsi zao, nchi zao, na tabaka zao, isipokuwa katika Hija, na hili ni katika utukufu wa Uisilamu.

Na mnao ndani ya Hija kudhihirisha maana miongoni mwa maana ya Uola [Ulezi wa Allah], na kuwa Allah anazipelekesha nyoyo za waja anavyotaka, basi hujaji na wengineo watambue kuwa uongofu umo Mkononi mwa Allah peke yake, na kuwa fadhila za Allah humpa amtakaye.

Na mnao katika kutekeleza nguzo hii utaratibu wa ibada baada ya nyengine, na usahihi katika amali na wakati, basi kuna ibada ya usiku - kama vile kulala Muzdalifah -, na nyengine ya mchana - kama kusimama Arafa -, na kuna ibada ya ulimi, kwa kuleta Takbira na 'Talbiya', na nyengine ya viungo - kama kurusha vijiwe na kufanya Twawafu -, na kwenye hili mna ishara ndani yake ya kuwa maisha ya Muisilamu yote ni kwa ajili ya Allah.

Na mazingatio ya amali ni mwishoni, na huenda ikaonekana athari ya hitima yake siku ya kukusanywa [Kiyama]; mtoa Sadaka anabaki kuwa chini ya kivuli cha Sadaka yake siku ya Kiyama, na muadilifu katika hukmu yake atakuwa juu ya mimbari kuliani kwa Ar-Rahmaan, na atakayekufa ndani ya ihramu atafufuliwa akileta 'Talbiya'.

Ni juu ya mja pindi inapopasuka alfajiri ya siku yake aihesabu kuwa ni hatima ya umri wake; huku ni kuitendea kazi kauli ya Nabii swala na salamu za Allah zimshukie:

«**kuwa duniani kana kuwa wewe ni mgeni au mpita njia**», imepokewa na Bukhari,

Na atakayeufunga moyo wake na Allah na nyumba ya Mwisho, na akafupisha matamanio yake ya dunia, na akajiandaa kwa maandalizi ya uchamngu, basi atapata kusalimika na kufaulu.

***'Audhu billaahi mina sh-shaitwaani rrajiim'***

﴿وَأَذِّن فِي ٱلنَّاسِ بِٱلۡحَجِّ يَأۡتُوكَ رِجَالٗا وَعَلَىٰ كُلِّ ضَامِرٖ يَأۡتِينَ مِن كُلِّ فَجٍّ عَمِيقٖ * لِّيَشۡهَدُواْ مَنَٰفِعَ لَهُمۡ وَيَذۡكُرُواْ ٱسۡمَ ٱللَّهِ فِيٓ أَيَّامٖ مَّعۡلُومَٰتٍ عَلَىٰ مَا رَزَقَهُم مِّنۢ بَهِيمَةِ ٱلۡأَنۡعَٰمِۖ فَكُلُواْ مِنۡهَا وَأَطۡعِمُواْ ٱلۡبَآئِسَ ٱلۡفَقِيرَ﴾

{Na watangazie watu Hija; watakujia kwa miguu na juu ya kila ngamia aliye konda, wakija kutoka katika kila njia ya mbali * Ili washuhudie manufaa yao na walitaje jina la Allah katika siku maalumu juu ya wanyama hoa aliowaruzuku. Basi kuleni katika hao na mlisheni mwenye shida aliye fukara}. (Al-Hajj: 27-28).

Allah anibarikie mimi na nyinyi katika Qur-ani tukufu...

## HOTUBA YA PILI

Sifa njema zote anastahili Allah kwa wema Wake [kwetu], na shukrani zote anastahili Yeye kwa kutuafikia na kutuneemesha, na nashuhudia ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake hana mshirika; ili kuadhimisha shani yake, na nashuhudia ya kwamba Nabii wetu Muhammad ni mja Wake [Allah] na Mtume wake, swala na salamu nyingi za Allah zimshukie yeye, watu wa nyumba yake na Masahaba wake.

**Enyi Waislamu:**

Allah amezihusu sehemu kwa utukufu na ubora, na akachagua katika mwaka nyakati ambazo ndani yake amali zinakuwa takatifu na ujira maradufu, basi akachagua katika miezi: miezi ya Hija na Ramadhani, na katika michana na usiku: kumi la mwisho la Ramadhani na kumi na la Dhul-hijjah, na michana ya Dhul-hijjah ni bora kuliko michana ya Ramadhani, [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

«**Hakuna amali ndani ya kumi lolote zitakuwa bora kuliko amali ndani ya hili** [kumi la Dhul-hijjah] -, **wakasema: Hata Jihadi katika njia ya Allah?** [Mtume] **Akasema: Hata Jihadi katika njia ya Allah, ila mtu aliyetoka akihatarisha nafsi yake na mali yake, na asirudi na chochote**», imepokewa na Bukhari;

Na ni katika amali njema ndani yake: kuzidisha kuwatenda wema wazazi wawili, kuunga kizazi, Sadaka, Saumu, Dhikri, kusoma Qur-ani, kuwafariji wenye majanga, na kuleta Takbira, na walikuwa Masahaba Allah awaridhie wakileta Takbira hata ndani ya masoko.

Kisha jueni kuwa Allah amewaamrisha kumswalia na kumsalimia Nabii wake...

# MASIKU YA HIJA[1]

Sifa za ukamilifu zote ni za Allah, tunamhimidi, tunamuomba msaada, tunamuomba msamaha, na tunajilinda na Allah kutokana na shari za nafsi zetu, na kutokana na amali zetu mbovu, yule ataongozwa na Allah, basi hakuna wa kumpoteza, na atakaye mpoteza hakuna wa kumuongoza, nashuhudia ya kwamba hapana apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake, hana mshirika, na nashuhudia kuwa Nabii wetu Muhammad ni mja wake na Mtume wake, swala na salamu nyingi za Allah zimshukie yeye, watu wake, na masahaba wake.

**Ama baada ya himdi hii:**

Mcheni Allah - Enyi waja Allah - haki ya kumcha, na shikamaneni Naye; kwani atakaye shikamana na kamba ya kumtarajia Yeye atamuafikia na amuongoze, na atakayetaka kinga Kwake atamuhifadhi na atamkinga.

**Enyi Waislamu:**

Katika amani yanatimia yanayotamaniwa, na ndani ya mji wa amani zinanyanyuka nafsi za watu wema, na kingizoni mwa nyumba ya Allah wanahisi amani walio na hofu:

﴿وَمَن دَخَلَهُۥ كَانَ ءَامِنًا﴾

{na mwenye kuingia humo anakuwa katika amani}, (Al-Imran: 96-97)

Na utakatifu wa nyumba tukufu umekunjuka zaidi ya hapo; nayo ni haramu kuwinda ndani yake ndege, wala hasutwi mnyama, wala hakukatwi ndani yake mimea, wala hakiokotwi kitu ndani yake ila kwa mwenye kukitangaza.

Na Nyumba tukufu [Kaaba] ndio alama ya kudumu ya [Dini ya] Haniifiyyah [Uisilamu] iliyo nyepesi, na ndio kusudio la mahujaji wa nyumba ya Allah. Misingi yake imenyanyuliwa juu ya ikhlaasi, na ikainuliwa juu ya uchamngu. Imejengwa na mikono ya Nabii, na kwa ushirika wa Nabii, nao hali wanajenga Nyumba tukufu zaidi wanaogopa kutokubaliwa amali hiyo, wakakimbilia kwa Allah:

﴿رَبَّنَا تَقَبَّلۡ مِنَّآۖ إِنَّكَ أَنتَ ٱلسَّمِيعُ ٱلۡعَلِيمُ﴾

---

[1] Imetolewa siku ya ijumaa, tarehe tisa, mwezi wa Dhul-hijjah, mwaka elfu moja mia nne na kumi na tisa, katika Msikiti wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie.

{Ewe Mola Mlezi wetu! Tutakabalie! Hakika Wewe ndiye Msikizi Mjuzi}; (Al-Baqarah: 127).

Basi Nyumba tukufu ikawa ni jengo lililonyanyuka, lenye nguzo thabiti, inadumu muda mrefu katika ulinzi na amani kutoka kwa Allah, vizazi vinaandamana katika kuihiji, na Waisilamu wanashindana katika kufika kwenye viwanja vake.

Katika uwanja wake mna amani na utulivu, na kingizoni mwake mna kheri na matunda:

﴿أَوَلَمۡ نُمَكِّن لَّهُمۡ حَرَمًا ءَامِنٗا يُجۡبَىٰٓ إِلَيۡهِ ثَمَرَٰتُ كُلِّ شَيۡءٖ رِّزۡقٗا مِّن لَّدُنَّا وَلَٰكِنَّ أَكۡثَرَهُمۡ لَا يَعۡلَمُونَ﴾

{Je! Kwani Sisi hatukuwaweka imara katika pahala patakatifu, penye amani, ambapo huletewa matunda ya kila aina kuwa ni riziki itokayo kwetu? Lakini wengi wao hawajui}. (Al-Qaswas: 57).

Katika Nyumba roho zinasafika, na moyo unalainika, hiyo [Nyumba] ni kibula wanacho kielekea, na safu zinaizunguka, wanapata kwake bendera inayowatia uvuli, na wanatembea katika msafara wake, nayo ni bendera ya Imani ambayo zinafichika chini yake tofauti za jinsia na rangi, na za lugha na miji, wanapata nguvu ya kujumuika, na matunda ya kudhaminiana, mlinganizi wa mjumuiko huu mkubwa ni mbia ya kipenzi cha Ar-Rahmaan:

﴿وَأَذِّن فِي ٱلنَّاسِ بِٱلۡحَجِّ يَأۡتُوكَ رِجَالٗا﴾

{Na watangazie watu Hija; watakujia kwa miguu} (Al-Hajj: 27)

.Na malengo ya mkutano huu: ni kutakasa makusudio na amali kwa Allah.

Enyi Waisilamu:

Hija ni mkusanyiko mkubwa wa Uislamu, inakutana ndani yake mijumuiko juu ya maombi ya baba yao Ibrahim, wala hazijaacha nyoyo za Waisilamu kutamani kufika katika Nyumba tukufu, na zina shauku ya kuiona, kuitufu na kufanya itikafu kingizoni mwake.

Na [Hija] inakusanya matukio yaliyopita; basi utamkumbuka Ibrahim [salamu zimshukie] hali anamuaga [mwanawe] Ismail na mamake karibu na Nyumba [tukufu], na anategemeza amri yao kwa Muumba, na anaelekea kwa Allah aliyetukuka na Maombi akimtegemea:

﴿رَّبَّنَآ إِنِّيٓ أَسۡكَنتُ مِن ذُرِّيَّتِي بِوَادٍ غَيۡرِ ذِي زَرۡعٍ عِندَ بَيۡتِكَ ٱلۡمُحَرَّمِ﴾

{Mola wetu Mlezi! Hakika mimi nimewaweka baadhi ya dhuriya zangu

katika bonde lisilokuwa na mimea, kwenye Nyumba yako Takatifu}. ( Ibrahim: 37).

Na utamkumbuka Haajar, akiwa anajitafutia maji yeye na mwanaye wa kunyonya katika bonde, - anakimbia baina ya Swafaa na Marwa- na kiu imemchosha, na shida imemdhoofisha, na huruma ya mwanaye imemtaabisha, na katika hali ile ngumu: Hakuelekea Sanamu, au wanaoombwa kinyume na Allah, au jiwe, ili atawasali nao; bali alinyenyekea kwa Allah na kumtaka uokozi [Allah] Mmoja wa aliye pekee, mara tu maji yakabubujika mbele ya mtoto mchanga, kumbe ni Zamzam - ambayo ni matunda ya kutawakali kwa Allah - chemchemi ya rehema, kheri na baraka katika jangwa la dhiki na ukame:

﴿وَمَن يَتَوَكَّلۡ عَلَى ٱللَّهِ فَهُوَ حَسۡبُهُۥٓ﴾

{Na anayemtegemea Allah Yeye humtosha}. (At-Twalaq: 3).

Na mnao katika tendo ya Haajar [katika tukio hili]: Kutambulisha umuhimu wa Dua na kutawakali kwa Allah, ndani ya uvuli wa Rehema ya Allah na taufiki Yake kwa kufungamana nalo katika kila amali - sawa iwe baina ya Swafa na Marwa, ama iwe katika njia za maisha na mazito yake -.

Kisha matukio yanafuatana katika fikra ya hujaji; akamkumbuka Mtume wa uongofu na Nabii wa rehema - Muhammad swala na salamu za Allah zimshukie – na hali anaishi udogoni mwake katika nyumba za Makkah, akiwa yatima wa wazazi wawili, anachunga mbuzi kingizoni mwa Nyumba hii [Kaaba], mara tu, cheo cha Utume wa milele kinamzunguka, na yakampata kwa sababu yake shere nyingi na maudhi mingi, kisha akaguria Madina, kutafuta nguvu na ngome ya Uisilamu, kisha akarudi Makkah akiwa anaongoza watu katika Hija ya kuaga, na Masahaba wake wakarimu wakiwa kingizoni mwake wakimzunguka kila upande, na inatimia ahadi ya Allah kwa Manabii wake na wafuasi wao:

﴿إِنَّا لَنَنصُرُ رُسُلَنَا وَٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ فِي ٱلۡحَيَوٰةِ ٱلدُّنۡيَا وَيَوۡمَ يَقُومُ ٱلۡأَشۡهَٰدُ﴾

{Bila shaka Sisi tunawanusuru Mitume wetu na walioamini katika uhai wa duniani na siku wataposimama Mashahidi}. (Ghafir: 51).

Enyi Waisilamu:

Mnao ndani ya Hija kuutakasa moyo kutokana na kila hadhi na matamanio, na kuisalimisha nafsi kwa Allah kwa hali ya utumwa; mnao ndani yake kujitakasa na madhambi, na kusalimika na athari zake, na kuokoka na Moto na kujishindia Pepo, na vinapotea ndani yake vitenganishi

vya jinsi, lugha na rangi, na inathibiti ndani yake mizani ya uchamngu ilio imara:

﴿يَـٰٓأَيُّهَا ٱلنَّاسُ إِنَّا خَلَقْنَـٰكُم مِّن ذَكَرٍ وَأُنثَىٰ وَجَعَلْنَـٰكُمْ شُعُوبًا وَقَبَآئِلَ لِتَعَارَفُوٓا۟ ۚ إِنَّ أَكْرَمَكُمْ عِندَ ٱللَّهِ أَتْقَىٰكُمْ ۚ﴾

{Enyi watu! Hakika Sisi tumekuumbeni kutokana na mwanamume na mwanamke. Na tumekujaalieni kuwa ni mataifa na makabila ili mjuane. Hakika aliye mtukufu zaidi kati yenu kwa Allah ni huyo aliye mchamngu zaidi katika nyinyi}. (Al-Hujuraat: 13).

Mnao ndani ya Hija ibada, utiifu na kuandama [mafunzo ya Mtume bila kuzusha], jitihada na subira, kushukuru na kuleta 'Talbiya', utulivu na upole, udhalilifu na unyonge [mbele ya Allah], mnao ndani yake aina tofauti za ibada na mambo yenye kukurubisha kwa Allah; kumdhukuru Allah kuko pamoja na hujaji:

﴿فَإِذَآ أَفَضْتُم مِّنْ عَرَفَـٰتٍ فَٱذْكُرُوا۟ ٱللَّهَ عِندَ ٱلْمَشْعَرِ ٱلْحَرَامِ ۖ وَٱذْكُرُوهُ كَمَا هَدَىٰكُمْ﴾

{Na mtakapo miminika kutoka 'Arafat mtajeni Allah penye al-Masha'ril Haram. Na mkumbukeni kama alivyo kuongoeni},

Na ndani yake mnao kuomba msamaha:

﴿ثُمَّ أَفِيضُوا۟ مِنْ حَيْثُ أَفَاضَ ٱلنَّاسُ وَٱسْتَغْفِرُوا۟ ٱللَّهَ﴾

{Kisha miminikeni kutoka pale wanapo miminika watu, na muombeni Allah msamaha}, (Al-Baqarah: 198).

Kumdhukuru Allah kunasuhubiana nao [mahujaji] kila wanaposhukia na kuondoka, au wanaposhuka jabali au wanapopanda, na utukufu wa mahujaji ni: «***labbayka laa shariika lak***».

**Enyi waja wa Allah:**

Katika siku ya Arafa yenye kushuhudia, ardhi yake inashuhudia makundi ya mahujaji, yanapatikana ndani yake mazingatio, na zinasamehewa ndani yake teleza, na maovu yanafutwa; basi hakuna siku inayokitihiri zaidi ndani yake kuacha huru na Moto kuliko siku ya Arafa, pamoja Mola mlezi kusamehe madhambi na kujigamba mbele ya Malaika wake na watu wa kisimamo [cha Arafa].

Kusimama kwao na kuondoka kwao; ni ukumbusho kwa Muumini wa kisimamo cha waja katika ardhi ya kukusanywa kwa ajili ya kuhukumiwa katika viwanja vya Kiyama, na lau ungewaona walipolala Muzdalifah,

wakalala na nia ya utiifu, na asubuhi wakamkurubia Allah kwa kuleta Dhikri katika al-Mash'ari Al-Haraam [yaani: Muzdalifaj], kisha wakafika Minaa - basi itimie kwa hilo kufikia kwao malengo -, na warushe vijiwe, wanyowe, na wachinje, na waombe uongofu kutoka kwa Allah, na waelekee Nyumba tukufu kwa ajili ya Twawaf ya ifaadhwa na Sa'ayi baina ya Swafaa na Marwa; na kwa hilo watimize Hija yao.

Ni nzuri ilioje amali ilio mabruur [iliotekelezwa vyema], Na ni uzuri ulioje wa Sa'ayi ya kushukuriwa, na juu ya mfumo kama huu ndio watende wenye kutenda, na washindane wenye kushindana katika kufanya juhudi kumtii Allah; basi hongera kwa aliyeitikia mwito wa Mola wake Mlezi, na akatufu katika Kaaba tukufu! Ni kufaulu kulioje kwa aliye simama Arafa, akaleta Talbiya na Takbira; na madhambi yake yakasamehewa, na kupata hadhi kubwa!

***'Audhu billaahi mina sh-shaitwaani rrajiim'***

﴿ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ وَعَمِلُواْ ٱلصَّٰلِحَٰتِ طُوبَىٰ لَهُمۡ وَحُسۡنُ مَـَٔابٖ﴾

{Wale walio amini na wakatenda mema watakuwa na raha na marejeo mazuri}. (Ar-Ra'd: 29).

Allah anibarikie mimi na nyinyi katika Qur’ani tukufu...

## HOTUBA YA PILI

Sifa njema zote anastahiki Allah aliyemuafikia amtakae kuziru nyumba yake tukufu, na akawahusi na shauku ya sehemu zile tukufu, namuhimidi Yeye aliyetakasika kwa fadhila nyingi na kutuneemesha.

Nashuhudia ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake, hana mshirika naye, Mfalme Mjuzi wa kila kitu, na nashuhudia ya kwamba Nabii wetu Muhammad ni mja Wake na Mtume Wake, aliye mwalimu bira kabisa na kiongozi bora kabisha, swala za Allah zimshukie yeye, watu wake na Masahaba wake wema na wakarimu.

**Enyi Waislamu:**

Hakika ni miongoni mwa makusudio ya Uisilamu katika kuamrisha Hija: Kukitisha msingi wa undugu wa kiisilamu chini ya Neno la uchamngu na Shahada ya haki.

Na katika Hija mafungamano ya waislamu yanapata nguvu, inapatikana hisia ya utukufu wa Uisilamu na nguvu na ushindi wa Imani, yanabainika ndani yake maana ya usawa wa kiisilamu wenye kudhihiri katika sura zake za wazi kabisa na maana yake yalio mazuri zaidi, na yanaenea mapenzi na uwiyano.

Unadhihiri umoja na uzoefu; pindi waislamu wanasimama katika kiwanja kimoja, kwa wakati mmoja, na katika nguo aina moja, wakimuomba Mola mmoja, kwa unyonge na unyenyekevu kwa ajili ya Allah, hakuna tofauti baina ya jinsi na jinsi nyengine, wala kipaumbele kwa nafsi juu ya nafsi nyingine, wala kufadhilishwa rangi juu ya rangi nyengine,

Wala hamna ajabu ya Allah kuteremsha katika siku hii – katika hija ya Mtume kuaga - aya ya kukamilisha Dini ya Uislamu:

﴿ٱلۡيَوۡمَ أَكۡمَلۡتُ لَكُمۡ﴾

{Leo nimekukamiliishieni Dini yenu, na nimekutimizieni neema yangu, na nimekupendeleeni UISLAMU uwe ndiyo Dini}, (Al-Maidah: 3).

Na umoja uliojengeka juu ya uongofu wa Kitabu cha Allah na Sunnah ya Mtume wake swala na salamu za Allah zimshukie; unatoa matunda ya kusaidiana juu ya wema na uchamngu, unaofikisha katika kunganisha kauli, na kuufahamu Uisilamu ufahamu wa hakika na kuutendea kazi.

**Enyi waja wa Allah:**

Aliyekosa kutenda amali njema kwa ajili ya udhuru ni mshirika wa mtendaji [katika ujira], na huenda mwenye kutembea kwa moyo wake akawashinda wenye kutembea kwa viwili viwili vyao, kwani ni Nia ngapi zilishinda amali yenyewe?! Na aliyekosa kusimama Arafa basi asimame kutekeleza haki ya Allah aliyoitambua, na aliyeshindwa kulala Muzdalifah; basi alaze azimio [kifuani mwake] la kumtii Allah, na ni sheria kwake kufunga siku ya Arafa; Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**Saumu ya siku ya Arafa, naitarajia kwa Allah ifute madhambi ya mwaka wa kabla yake na mwaka wa baada**», imepokewa na Muslim.

Basi shirikianeni na mahujaji kwa Dua, Tahlili [kusema; laa ilaaha illa llaah], Takbira, Tahmidi [kumhimidi Allah], na aina zote za dhikri; kwani Mola wenu Mlezi ni Mkarimu sana. Na patilizeni misimu ya ibada kabla kuisha kwake; kwani uhai ni ghanima, na siku ni za kuhesabika, na umri ni mfupi.

Kisha jueni kuwa Allah amewaamrisha kumswalia na kumsalimia Nabii wake...

# FAHARISI YA MAUDHUI


UTANGULIZI ........ 7

SHAHADA MBILI ........ 9

Ubora Wa Neno La Tawhidi ........ 11

Mjue Nabii Wako Swala Na Salamu Za Allah Zimshukie ........ 24

SWALA ........ 35

Cheo Cha Swala Katika Uisilamu ........ 37

Cheo Cha Swala Katika Dini ........ 46

Uwajibu Wa Swala Ya Jamaa ........ 57

ZAKA ........ 65

Zaka ........ 67

Ubora Wa Sadaka ........ 74

Ubora Wa Kutoa [Sadaka] ........ 81

SAUMU YA RAMADHANI ........ 89

Kujiandaa Kwa Ramadhani ........ 91

Ramadhani Imeingia ........ 97

Masiku Yenye Thamani. ........ 104

Fadila Za Kumi La Mwisho ........ 111

Usiku Wa Cheo (Laylatul Qadr) ........ 118

Kuondoka Kwa Ramadhani ........ 124

Kuisha Kwa Ramadhani ........ 129

HIJA ........ 135

Safari Ya Hija ........ 137

Malengo Ya Hija ........ 146


Ibada Ndefu Zaidi Ya Kimwili: Hija ........ 154

Masiku Ya Hija ........ 159

FAHARISI YA MAUDHUI ........ 167

TAASISI YA TWALIBUL ILM YA KUNUSHURU NA KUGAWA

00966506090448





# VITABU VYA MTUNZI VILIVYOTOKA


SILSILA YA HOTUBA ZA AL-MASJID AN-NABAWI




NGUZO ZA IMANI




AT-TAWHIID




AL-AKHLAAQ
[TABIA]




NABII SWALA NA SALAMU ZA ALLAH
ZIMSHUKIE NA MASAHABA WAKE